SUPA JACKPOT
TZS.1,037,361,877
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

UKURASA 3



## MBARONI tuhuma kuchoma mikono ya mwanawe kisa kudokoa dagaa




UKURASA 13

Nipashe
Jumamosi Oktoba 8, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581092
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Kikwete afichua mazito

**NI** kuhusu JPM, Mkapa, Membe, Lowassa...

*Endelea ukurasa 2*



Hayati Benjamin Mkapa



Hayati Dk. John Magufuli.



Bernard Membe



Edward Lowassa



Rais mstaafu Dk. Jakaya Kikwete

# Mtifuano kortini kina Mdee na mawakili wa CHADEMA

UKURASA 2

UKURASA WA 4

### WAKULIMA WALIA MFUMO UGAWAJI MBOLEA

WAKULIMA wadogo wameiomba serikali kufuatilia kwa karibu ugawaji wa mbolea ya ruzuku ambao katika baadhi ya maeneo umegeuka maumivu kutokana na mfuko wa kilo 50 kuuzwa zaidi ya Sh.120,000 badala ya bei elekezi ya...

UKURASA WA 4

### MALI ZA M'BIASHARA HATARINI KUPIGWA MNADA KISA KUDAIWA KODI

MAMLAKA ya Mapato Tanzania TRA, Zanzibar imesema mali za mfanyabishara Toufky Salum Turky, zitaendelea kushikiliwa na hatimaye kupigwa mnada iwapo atashindwa kukamilisha malipo ya kodi ya Sh. milioni 308.5. Turky anadaiwa kiasi hicho cha kodi baada...

UKURASA WA 5

### SERIKALI YATOA MAAGIZO SABA KUKABILIUPUNGUFU MVUA ZA VULI

OFISI ya Waziri Mkuu imetoa maelekezo saba kwa kamati za usimamizi wa maafa kwenye mikoa, wilaya, kata na vijiji, kukabiliana na kuwapo...

## Aibuka mshindi gari la mil. 14/- kwa kutoa buku

UKURASA 3

**MICHEZO** IWE JUA, IWE MVUA AL - HILAL HAWATOKI UK. 32

**KATUNI** UK. 6

# Kikwete afichua mazito

Na Romana Mallya

RAIS Mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, amefunguka mazito kuhusu masuala mbalimbali yakiwamo ya siasa za Tanzania, uhusiano na uswahiba wake na baadhi ya wanasiasa mashuhuri.

Kikwete alifunguka hayo jana wakati akihojiwa na Clouds Media Group, ikiwa ni siku yake ya kuzaliwa. Kikwete jana alitimiza miaka 72 tangu kuzaliwa kwake mwaka 1950.

Katika mahojiano hayo, alisema anashangaa kusikia kwamba Waziri wa zamani wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bernard Membe kuwa ni ndugu yake.

"La kwanza ni kwamba, Membe siyo ndugu yangu. Hatuna undugu kabisa. Membe ni Mmwela na mimi ni Mkwere. Hakuna undugu, hata wanapokuja kusema mimi ni ndugu yake wa damu.

"Unajua mengine ni maneno ya siasa, nikawa ninashangaa kweli. Sina uhakika mimi na Membe tunafanana nini? Membe nimekuja kumfahamu baadaye sana maishani," alisema.

Katika mahojiano hayo pia, Kikwete alizungumzia kinyang'anyiro cha urais uliohusisha vyama vingi hasa wa mwaka 1995, 2005 na 2015. Miaka hiyo ilikuwa ya kutafuta wagombea wapya wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutokana na waliokuwapo kumaliza muda wao wa vipindi viwili vya miaka mitano mitano kikatiba.

Kwa mujibu wa Kikwete, mwaka 1995 walikuwa wagombea 17 waliochukua fomu kuwania kuteuliwa na chama, mwaka 2005 walikuwa 11 na mwaka 2015 walikuwapo 42.

"Kwa utaratibu uliowekwa CCM, hatuwezi kupeleka wagombea wote 42. Kazi ya Kamati Kuu ni kuwa na watu watano. Tukawa na wanawake wawili, Balozi Amina Salum Ali na Dk. Asha-Rose Migiro na wanaume walikuwa watatu ambao ni January Makamba, Membe na Dk. John Magufuli ambaye alishinda na baadaye kupeperusha bendera ya CCM hatimaye kuibuka mshindi.

"Kwenye kamati ya maadili, kila mmoja aliangaliwa kwa sifa zake, uwezo wake, afya yake, tabia, makando kando na vitu vingine vingi, hatimaye tukaja na orodha ya watu watano. Tulipokwenda kwenye Kamati Kuu kukawa na mjadala mkubwa kwa nini huyu mmemwacha huyu, kwa nini mmewachukua hawa.

"Wakati huo wanasema, Magufuli hajawahi kuwa kiongozi kwenye chama hiki, kukawa na mjadala mkali kweli. Hajawahi kuwa hata balozi, hata kuwa mwenyekiti wa chama. Nilichofanya pale kila aliyetaka kuzungumza alizungumza.

"Wale wanaomtetea huyu, kwa nini (Edward) Lowassa kaachwa, walikuwa wanasema kwa nini (Dk. Mohamed Gharib) Bilal kaachwa, kwa nini (Mizengo) Pinda kaachwa, kwa nini (Stephen) Wassira hayumo.

"Tukazungumza mpaka tukafika mwisho, nikasema jamani tupige kura. Tukapiga tukapata majina matatu, tukapeleka kule, hakuna la zaidi ya utaratibu wetu wa kawaida.

"Kama mwenyekiti ndiyo kutengeneza ile orodha ya wale watano, orodha niliitengeneza mimi ile ya wale watano, mimi ndiye mwenyekiti. Ninashukuru tulijadiliana vizuri.

**USHINDI WA MKAPA**

Kikwete alisema alipotangazwa Benjamin Mkapa mwaka 1995 kuwa ameshinda kinyang'anyiro cha uteuzi wa urais, mwitikio ulikuwa tofauti, hivyo yeye aliona asiposema kitu chama kitagawanyika.

"Nikaandika kwenye karatasi nikamwambia mtu kampe Katibu Mkuu, Laurence Gama, ampe mwenyekiti ninaomba kuzungumza. Gama akaisoma akaiweka chini, nikaandika ya pili nikampa mtu nikamwambia nenda kampe Mzee (Kingunge) Ngombale (Mwiru), ampe mwenyekiti.

"Ngombale akampa Mzee (Ali Hassan) Mwinyi wakajadiliana kwa sababu tulikuwa watatu, wakajiandaa Msuya aseme lakini kwa sababu alikasirika sana hata maneno aliyokuwa anayasema unaona ana hasira. Ningetoka pale bila ya kuzungumza ingekuwa ngumu baada ya hapo kukiunganisha chama.

"Maana wakati ule ndio ulikuwa unasikia huko nje vijana wamevua mashati CCM 'bye bye'. Ilikuwa mchanganyiko kweli. Ninakumbuka hata baada ya pale tumerudi kwenye kituo chetu, ninazungumza na timu yangu, mmoja akasema (simtaji jina) nipeni Konyagi akasema bora nife, siyo siri. Anna Makinda alisema kungekuwa na utaratibu wa mgombea binafsi, haki ya Mungu tungemsimamisha mgombea binafsi," alisema.

"Wengine wakawa wanashauri tutafute chama kimoja tukajiunge huko. Nikasema mimi huko siendi, wengine wakasema tuchukue Baraza Kuu la Vijana CCM tuitishe mkutano tutangaze wote tumeondoka ndani ya CCM tuunde chama cha siasa, nikawaambia inayosajili hicho chama ni serikali hatutasajiliwa," aliongeza.

Kikwete alisema aliwaeleza kuwa faida waliyo nayo yeye ana umri wa miaka 45 kama uhai upo na Mungu ndiye amemwandikia kuwa Rais miaka 10 ijayo atakuwa na umri wa Mkapa. Baada ya miaka 10 alishinda kwa kishindo ndani ya chama na hatimaye kuwa mgombea na kushinda uchaguzi kisha kuwa Rais wa Awamu ya nne.

"Tulivyokuwa kule hatua ya kwanza tumeshinda na habari ikafika pale, ninakumbuka walitengeneza karatasi fulani hivi zenye kaulimbiu 'Kikwete kiongozi ambaye wakati wake umeshafika'. Ninakumbuka (Ukiwaona) Ditopile (Mzuzuri) alikuwa nayo mengi, baba yake Mange Kimambi (sasa marehemu) rafiki yangu sana, wale ndo walikuwa mashabiki wangu.

"Tumetoka Area D tunakuja mkutanoni wamefurahi vijana, walipofika pale wakaambiwa ndio tunarudia, wakaniuliza wamekuahidi nini nikawaambia hajaniahidi chochote.

"Aliyekwenda kunisimamia kule ni Isdore Shirima, alipotoka kwenye kuhesabu kura, akapita pale akanionyesha ishara kuwa mambo huko siyo mazuri, basi nikatulia tu. Hakukuwapo na mazungumzo sijui Mwalimu (Julius Nyerere) alimwita, akamwambia 'subiri wewe kijana' hayo hayakuwapo. Yale yalikuwa mawazo yangu tupu pale, kama nilivyosema niliandika vikaratasi viwili, cha kwanza nikampa Katibu Mkuu na cha pili Ngombale.



"Ndipo wakaanza kujadili, walikuwa na hofu kweli ninakwenda kusema nini. Waliangalia ile hali ya vijana na hakika ingekuwa ni kitu kimepangwa huko, wangekataa nisiseme," alisema.

**MIAKA 7 URAIS**

Kikwete pia alizungumzia mapendekezo ya baadhi ya wanachama wa CCM kuongeza muda wa Rais kukaa madarakani kutoka miaka mitano hadi saba kwa awamu moja, akiweka wazi kuwa wazee ndani ya chama hicho, akiwamo yeye, waliingilia kati ili kuhakikisha wanaheshimu Katiba ya nchi.

**MAUAJI YANAYOENDELEA**

Akizungumzia kuhusu matukio ya watu kujiua, Kikwete alisema si mambo mapya kwa kuwa yalikuwapo tangu zamani.

"Si kwamba sasa hivi ndiyo yanatokea sana. Yalikuwapo tangu zamani. Hili ni suala la kuhimili, wengine wana uwezo huo ikitokea amekataliwa basi anaendelea na maisha atatafuta mwingine.

"Hata masuala ya ndoa kuvunjika ni kushindwa kuhimili kwa kuwa kila mtu ana uwezo wake katika kuvumilia na kuyachukulia mambo," alisema.

**NDOA YAKE**

Kuhusu ndoa yao, mke wake, Mama Salma (Mbumge wa Mchinga kwa tiketi ya CCM), alisema pamoja na upendo kutawala maisha yao, kikubwa kinachowafanya waendelee kuwa na furaha hadi sasa ni uvumilivu na kuwasisitiza vijana suala la uaminifu.

"Mimi simu yangu anapokea mume wangu kikubwa ni kuaminiana. Jiaminishe wewe ndiyo mke au mume hakuna mwingine zaidi yako," alisema.

# Mtifuano kortini kina Mdeena mawakili wa CHADEMA

Na Grace Gurisha

MBUNGE Viti Maalum, Grace Tendega ameiomba Mahakama Kuu Masjala Kuu Dar es Salaam imlinde iwapo atatoa siri wakati anaulizwa maswali ya dodoso kuhusu hati yake ya kiapo iliyotumika kufungua kesi ya kupinga kuvuliwa uanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Tendega aliwasilisha maombi hayo jana wakati anahojiwa na Peter Kibatala, wakili wa mjibu maombi wa kwanza katika kesi namba 36/2022, Bodi ya Wadhamini ya CHADEMA.

Kesi hiyo iliyofunguliwa na Grace pamoja na wabunge wa viti maalum wengine 18, wakiongozwa na Halima Mdee, inasikilizwa mbele ya Jaji Cyprian Mkeha.

Kufuatia maombi hayo ya Grace, Jaji Mkeha alimweleza ulinzi upo, hivyo akamtaka kujibu maswali aliyokuwa anaulizwa.

Katika mahojiano hayo Wakili Kibatala alimuuliza kama anakumbuka alikokuwa Julai 18 mwaka huu.

"Nina swali, unavyoniona hapa nilikuwa kiongozi mkubwa katika Baraza la Wanawake la CHADEMA (BAWACHA), nilikuwa katibu mkuu na nimeapa hapa nitasema kweli daima.

"Ninaomba Jaji kwa sababu nimeapa nitasema kweli daima, unilinde nitakaposema mengine ambayo yatakuwa siri. Mimi ni kiongozi mkubwa, ninaomba pia hilo nililinde," Grace alidai.

Jaji Mkeha aliingilia mahojiano, akisema: "Hutasema chochote ambacho siyo jibu la swali unaloulizwa, mawakili watauliza maswali, utajibu watakayokuuliza. Ulinzi ni guarantee."

Baada ya Jaji Mkeha kutoa mwongozo huo, Wakili Kibatala aliendelea kumuuliza maswali hayo ya dodoso kuhusu hati yake ya kiapo.

Hatua ya kuwahoji baadhi ya walalamikaji inatokana na maombi ya mawakili wa CHADEMA kuomba siku ya kuanza usikilizwaji wa kesi hiyo wapewe nafasi ya kuwahoji walalamikaji wanane kati yao, akiwamo Mdee na wenzake saba.

Mbali na Mdee, wengine walioitwa ni Nusrati Hanje, Ester Matiko, Ester Bulaya, Jesca Kishoa, Grace, Hawa Mwaifunga na Cecilia Pareso.

Katika shauri hilo wabunge hao pamoja na mambo mengine, wanaiomba mahakama hiyo ipitie mchakato na uamuzi huo wa CHADEMA kuwafukuza, kisha itoe amri tatu.

Mdee na wenzake wanaomba mahakama itengue mchakato na uamuzi wa kuwavua uanachama, iwalazimishe CHADEMA kuwapa haki ya kuwasikiliza na amri ya zuio dhidi ya Spika na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kukuchukua hatua yoyote hadi malalamiko yao yatakapotolewa uamuzi.

**HABARI KITAIFA**

# Mshindi Radio One anyakua gari la mil. 14/-

**Na Halfani Chusi**

MKAZI wa Songea Mji Mwema, Vitus Miti, ameibuka mshindi wa gari aina ya Toyata IST lenye thamani ya Sh. Milioni 14 lililokuwa likishindaniwa kwa kucheza Mchezo Supa unaoendeshwa kupitia Radio One na Capital Radio.

Akizungumza wakati wa kukabidhiwa gari hilo na Mkurugenzi wa Radio One, Deogratius Rweyunga, mshindi huyo alisema haikuwa rahisi kuamini kama ameshinda kutokana na wimbi la utapeli lililopo kwa sasa.

"Nilipopigiwa simu kuambiwa nimeshinda gari. Sikuamini nikamwambia mke wangu naye hakuamini lakini baadaye wakanipigia tena simu wakaniambia nifike katika ofisi zao zilizopo Dar es Salaam, Mikocheni siku ya Ijumaa (jana).

"Baada ya kuambiwa hivyo, ilibidi nianze kujiandaa kuondoka Songea kuja Dar es Salaam, nikamchukua rafiki yangu ambaye anajua kuendesha gari kwa ajili ya kuliendesha wakati wa kurudi nyumbani

Nimecheza mara 12 na nimetumia elfu 12 tu mpaka kushinda gari kwa hiyo niwasihi vijana wenzangu wasikilize radio one na vipindi vyake wanaweza kuibuka washindi kama mimi," alisema.

Miti alisema siku zote anayefanikiwa huwa anakuwa mtu wa kujaribu bila kujali matokeo kwa hiyo kwake hiyo inampa nguvu ya kuendelea kushiriki ili kujiweka katika nafasi ya kushinda vitu vingine.

Baba mdogo wa mshindi huyo, Festo Miti, katika hafla hiyo alimsihi kuitunza mali hiyo akibainisha kuwa katika familia yao hawajawahi kumiliki hata baiskeli kwa hiyo gari kwao ni kitu cha thamani.

"Nimemsihi mwanangu awe makini na marafiki lakini asimsahau mke wake ambaye wamesota wote katika kutafuta. Azidishe heshima kwa watu kupata gari isiwe sababu ya kuwadharau watu wengine," alisema.

Rweyunga alimpongeza Miti kwa kuibuka mshindi katika kinyang'anyiro hicho huku akiwasihi watu kuendelea kuchangamkia fursa hiyo.

"Kwa wale wanaotaka kushinda zawadi zingine wasikilize vipindi vya Radio One wakiwa na laini za simu za mitandao ya Tigo, Vodacom, Airtel na Halotel kwa Sh. 1,000 tu huku wakibonyeza namba za menyu kulingana na mtandao wanaotumia kisha kwenda lipa bili. Baada ya hapo wanaingiza namba ya kampuni ambayo ni 222223 na baada ya hapo wataingiza kumbukumbu namba ambazo ni 111,au neno SUPA.

Tumekuwa na mchezo Supa toka Mei na tumekuwa tukitoa zawadi mbalimbali. Kadri tunavyozidi kwenda, ndivyo tunaboresha zawadi zetu. tulianza na Sh. 100,000 tumepanda mpaka ilifika wakati tunatoa Sh milioni tano mshindi huyo alitoka Mwanza," alisema.




Mkurugenzi wa Radio One, Deogratias Rweyunga (kushoto), akishuhudia wakati mshindi wa Droo ya Buruza ndinga na Radio One, Vitus Paul, akijaribu zawadi ya gari lake aina ya Toyota IST, baada ya kumkabidhi Mikocheni, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mbaroni kwa tuhuma kumchoma mwanawe kisa kudokoa dagaa

**Na Hamisi Nasri,** MTWARA

SOMOE Mohamedi, mkazi wa Kijiji cha Namanjele, Kata ya Dihimba mkoani Mtwara, anashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani hapa kwa tuhuma za kuchoma moto viganja vya mikono vya mtoto wake mwenye umri wa miaka mitano (jina linahifadhiwa).

Inadaiwa kuwa mtoto huyo ambaye ni mwanafunzi wa darasa la awali amekumbana na adhabu hiyo ya kikatili baada ya kudaiwa kuchukua Sh. 250 na kudokoa dagaa waliokuwa wamepikwa kwa ajili ya mboga.

Akithibitisha tukio hilo, Kamanda wa Polisi mkoani Mtwara, Nicodemus Katembo alisema wanamshikilia mtuhumiwa kwa ajili ya mahojiano zaidi kuhusu ukatili huo.

Alisema mtuhumiwa huyo alifanya kitendo hicho kwa kumchoma moto mtoto wake na kumjeruhi katika sehemu za viganja vya mikono katika Kijiji cha Namalenje wanakoishi.

"Ni kweli tunamshikilia mama huyu kwa kosa la kumchoma moto mtoto wake sehemu za mikono na kumsababishia majeraha. Upelelezi ukikamilika tutamfikisha mahakamani kujibu mashtaka yanayomkabili. Kwa sasa mtoto anaendelea na matibabu katika Hospitali ya Ligula mkoani hapa," alisema.

Kamanda Katembo alieleza kuwa kabla ya kutekeleza ukatili huo, mama huyo anadaiwa alichoma kamba mikononi mtoto wake na kuchukua nyasi kavu kisha kuziweka kwenye mikono ya mtoto huyo na baadaye kuwasha moto.

Alisema kuwa baada ya kuwasha moto huo, mtoto huyo alipata majeraha sehemu mbalimbali za mikono yake na kumsababisha maumivu makali.

Kamanda huyo aliendelea kufafanua kuwa moja ya sababu iliyotajwa ya mama huyo kumchoma moto mtoto wake ni mtoto huyo kudaiwa kuchukua fedha Sh. 250 ambazo ni mali ya mama yake mzazi.

Alisema sababu nyingine ambayo inadaiwa na mama huyo kuamua kumfanyia ukatili mwanawe ni mtoto huyo kudaiwa kudokoa mboga iliyokuwa imepikwa na mama yake, jambo ambalo mama yake anajitetea kwa polisi kwamba lilimfanya aingiwe na hasira.

Alisema kuwa kufuatia ukatili huo jeshi hilo lilipata taarifa na kufuatilia kisha kubaini ukweli wa tukio na kumkamata mama huyo kwa ajili ya uchunguzi zaidi na hatua za kisheria.

Kamanda Katembo alitoa rai kwa jamii kuacha mara moja vitendo vya kikatili dhidi ya watoto kwa kuwa serikali haitavumilia kuona vitendo hivyo vikiendelea.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Barua Pepe: ps@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaa wa Mtumba,**
**S.L.P. 2888,**
**40470DODOMA,**
**07 - 10 - 2022**

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kutaarifu umma kuwa siku ya Jumatatu tarehe **10-10-2022** kampuni ya Mainline Carriers Ltd itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM PORT** kuelekea **MBAGALA**, gari hizo zenye namba za usajili:

| | | | |
|---|---|---|---|
| T 178 DFC /T 772 DJB | T 895 BNS / T 328 BYR | T 329 BFH / T 206 DFC | T 694 BNQ / T 830 DJB |
| T 322 BHS / T 221 DFC | T 336 BYR / T 331 BYR | T 691 BJB /T 218 DFC | T 559 BKC / T 687 AUE |
| T 266 BXH /T 893 DJB | T 257 BXH /T 200 DFC | T 922 BTE /T 244 BYM | |

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 18 Upana - mita 4.40 Kimo - mita 4.80**

3. Njia itakayotumika: **BANDARI YA DAR ES SALAAM** kupitia **KILWA ROAD**. Gari litasafiri muda wa mchana (**Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

217082602



**NGOMENI ENTERPRISES**

**NOTISI YA SIKU KUMI NA NNE (14) YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA.**

Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na crdb bank makao makuu Dar es salaam tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) tu ili uweze kulipa deni lako lote unalodaiwa Pamoja na gharama za dalali. Kukaidi au kushindwa kulipa deni hilo tutauza dhamana uliyoweka bank kwa mnada wa hadhara kama inavyoonesha kwenye jedwari hapo chini.

| S/N | JINA LA MDAIWA | DHAMANA / MAHALI | TAREHE/ MUDA |
|---|---|---|---|
| 1. | KENNEDY CHRISTOSIA MATHEMU | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO ENEO LA UKOMBE, MTAA WA MADAFU MANISPAA YA ILALA. | 4.11.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 2. | KASMERY YONATHAN MGWABATI | NYUMBA YA MAKAZI YENYE PLOT NO. 942, BLOCK "B" KIZINGA – KIVULE, MANISPAA YA ILALA. | 10.11.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 3. | KASHEBO JASSONY RWEZAULA | NYUMBA YA MAKAZI PLOT NO. 411 ILIYOPO SAVEI –KINONDONI. | 15.11.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA. |
| 4. | HARUNA AMRAN KANGESA | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO MWANGATA MANISPAA YA IRINGA | 22.11.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 5. | THEMISTOOLES JULIUS CAESAR | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO MTONI KIJICHI YENYE PLOT NO. 1224, BLOCK "C" | 25.11.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 6. | JAPHET LAITON MWANGUPILI | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO MKONGA MANISPAA YA MKURANGA. | 18.11.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA. |
| 7. | PASCHAL PAUL SAMBAI | NYUMBA YA MAKAZI YENYE PLOT NO. 148, BLOCK 28, ILIYOPO BUYUNI – KIGAMBONI | 30.11.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA. |
| 8. | FLORA BERNARD HINJUSON | NYUMBA YA MAKAZI YENYE PLOT NO. 217, BLOCK 23 ILIYOPO GEZAULOLE DAR ES SALAAM. | 2.12.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA. |
| 9. | AGREY SASILE YUSUPH | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO MTAA WA MSUFINI PICHA YA NDEGE-KIBAHA | 25.10.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 10. | CHRISTINA SAMWEL JENERAD | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO PUGU KINYAMWEZI CHANIKA | 28.10.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA. |

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Dhamana itauzwa kama zilivyo.
2. Mnunuzi atakayeshinda atalipa malipo ya awali ya asilimia 25 ya bei itakayofikiwa siku ya mnada na asilimia 75 atalipa ndani ya siku 14.
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la asilimia 75 katika muda uliopangwa hapo juu, hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki, kutwaa nyuma na gharama nyinginezo zitakuwa juu ya mnunuzi.
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua nyumba muda wote isipokuwa usiku.

**MAWASILIANO:**
**CRDB BANK PLC, HEAD QUARTER. NGOMENI ENTERPRISES, DSM.**
**SIMU: 0719974916/ 0784252048**

217082702

# Wakulima walia mfumo wa ugawaji mbolea

**Na Mwandishi Wetu,** SAME

WAKULIMA wadogo wameiomba serikali kufuatilia kwa karibu ugawaji wa mbolea ya ruzuku ambao katika baadhi ya maeneo umegeuka maumivu kutokana na mfuko wa kilo 50 kuuzwa zaidi ya Sh.120,000 badala ya bei elekezi ya Sh. 70,000.

Aidha, wamesema makundi maalum hayapati mbolea hizo huku anayehitaji kuanzia kilo moja kuendelea hawezi kupata hadi aununue mfuko mzima wakati uwezo wake ni mdogo.

Madai hayo yalitolewa jana na wakulima kutoka wilayani Mbeya na Hai, mkoani Kilimanjaro, wanaoshiriki Tamasha la Jinsia Kanda ya Kaskazini lililoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), lililomalizika jana wilayani hapa.

Hobokela Kilindu, mkazi wa kata ya Tembela mkoani Mbeya, alisema mbolea ya ruzuku ni maumivu makubwa kutokana na masharti yaliyowekwa ambayo kwa mtu mwenye ulemavu au mzee hawezi kuzipata kwa urahisi na kwa wakati kwa kuwa wengi wanasema hawana vocha (ruzuku ya serikali) hadi baada ya wiki moja.

"Anaweza kukwambia lete fedha alafu baada ya siku tatu au nne ufuate mbolea. Mkulima nina malengo yangu unahitaji ila unakosa kwa sababu mawakala si waaminifu. Huwezi kupata mbolea kwa Sh. 70,000 lazima uongeze fedha hadi Sh. 90,000 na unaenda kuifuata kilomita mbili au zaidi," alisema.

"Unapofika kwa wakala kuna vijana ambao sielewi wameajiriwa na nani. Hata kama una uwezo wa kupakiza kwenye gari mwenyewe lazima uwalipe hao vijana wakupakilie kila mfuko Sh. 500 na wanakwambia wazi bila hawa hupati mbolea, bado usafiri kutoka kijijini hadi kwa wakala," aliongeza.

Aidha, Kilindu alisema mfumo wa sasa umeondoa wauzaji wadogo ambao wanatakiwa wawe wasomi, uwe na leseni na cheti cha ufaulu ndio wauze viuatilifu na mbolea.

"Walikuja Mbeya wakafundisha watu wakatoa mtihani kwa waliofaulu walipewa vyeti, wakaondoka kwa uliyesoma kama hujafaulu unahama kwenda mkoa mwingine ili ufanye mtihani uwe wakala, hili ni tatizo kama huna ada ya Sh. 300,000 huwezi kusoma na kuwa wakala, hii imeua ajira zetu," alisema.

Kilindu aliishauri serikali ifanye tathimini na kuangalia upya huu mfumo, ingeacha mfumo wa zamani au mawakala wawape elimu ya kutosha kwa sasa wamekuwa miungu watu.

"Nia ya serikali kuleta mapinduzi ya kilimo haitafikiwa mfano eneo letu muda wa kupanda umefika na mbolea hakuna, wanatengeneza mazingira ili ipande bei. Mbolea ya ruzuku inatakiwa Sh. 70,000 lakini hadi sasa ili upate haraka ni 90,000 na nyingine 80,000 hadi 100,000 bado hujaweka usafiri.

"Tunatoka mbali sana unapanda basi kutoka Tembela hadi Mbalizi, kama unaenda kuchukua mfuko mmoja unatumia 10,000 hadi 15,000," alifafanua.

Naye Janeth Barnaba mkazi wa Kata ya Mbalizi, Mbeya, alisema wenye ulemavu na wazee wanapata tatizo kupata ruzuku hiyo kutokana na umbali kutoka kijijini hadi kwa wakala.

"Mzee au mlemavu anaandikishiwa Mshewa alafu anatakiwa kusafiri hadi Sido Mbeya mjini kuweka dole gumba alafu atatakiwa kwenda Mbalizi anatumia nauli ya Sh. 8,000 kwenda na kurudi, akikutana na dalali amlipe 20,000 hivyo anaipata mbolea kwa zaidi ya Sh. 100,000 bado hatujawasaidia wakulima kabisa," alisema.

Naye Mkulima na Mjasiriamali wa wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro, Etropia Assenga, alisema eneo lao kuna utaratibu wa kujiandikisha kwa kata na vijiji, kwa mabalozi kupita kila nyumba ambao wanaandikisha wakulima ambao baada ya pembejeo kufika wanalipia Sh. 70,000 na kupewa mbolea.



Rais mstaafu Dk. Jakaya Mrisho Kikwete, akisikiliza maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Fujin Hexingwang Tanzania Ltd, Xu Xing da (kulia), kuhusu uzalishaji wa nondo na uunganishaji magari, wakati wa maonyesho ya tatu ya viwanda, biashara na uwekezaji, mjini Kibaha, mkoani Pwani juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mali za mfanyabiashara hatarini kupigwa mnada kisa kudaiwa kodi

**Na Mwandishi wetu,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Mapato Tanzania TRA, Zanzibar imesema mali za mfanyabishara Toufky Salum Turky, zitaendelea kushikiliwa na hatimaye kupigwa mnada iwapo atashindwa kukamilisha malipo ya kodi ya Sh. milioni 308.5.

Turky anadaiwa kiasi hicho cha kodi baada ya kuingiza gari la kifahari aina ya Benz tangu Januari, mwaka huu.

Naibu Kamishina wa TRA Zanzibar, Juma Bakary Hassan, alitoa msimamo huo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Kinazini, baada ya maombi kutaka kuruhusiwa kulipa kidogo kidogo kwa awamu tatu kukataliwa Oktoba 3, mwaka huu.

"Tumewataka walipe kwa pamoja na kwa mujibu wa sheria kama watashidwa tutakamata mali kupitia mdhamini wake ili kuhakikisha kodi ya serikali inalipwa." alisema.

Juma alisema, walipokea maombi ya kutaka waruhusiwe kulipa kidogo kidogo Septemba 29, mwaka huu, baada ya kulipa Sh. milioni 138 kati ya Sh. milioni 308.5.

Alisema, kampuni ya Mifuko Turkys mpaka sasa inadaiwa Sh. milioni 170.5 baada ya maombi ya msamaha wa kodi kukataliwa mara mbili na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango licha ya kuidhinishwa na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Uwekezaji Vitengauchumi Zanzibar (ZIPA), Sharif Ali Sharif.

Juma alisema gari hilo ilitolewa bandarini kabla ya kukamilisha taratibu za kodi baada ya kuwekewa dhamana na taasisi moja ya fedha wakati wakiendelea kukamilisha taratibu za msamaha wa kodi kupitia mradi wa Kiwanda cha Mifuko Zanzibar.

Kwa mujibu wa Juma, baada ya maombi kukataliwa, waliomba TRA wafanye tathmini upya ya thamani ya gari na kodi wanayotakiwa kulipa baada ya kutilia wasiwasi lakini thamani ilikuja ile ile kama mwanzo.

"Tulipowaarifu wakalipa Sh. milioni 138 lakini wakaja tena na maombi ya kumalizia deni la milioni 170 kidogo kidogo. Sasa wadhamini wao taasisi moja ya fedha wametaka wapewe nyaraka za gari wapate kujiridhisha baada ya kutakiwa wahusika kulipa deni kwa pamoja," alisema.

Kwa mujibu wa sharia, alisema kama watashindwa kukamilisha malipo kama walivyotakiwa, TRA italazimika kukamata mali za mhusika na kupigwa mnada kufidia malipo ya kodi ya serikali.

Kuhusu gari kuonekana likitembea mitaani kabla ya kukamilisha malipo ya kodi, alisema TRA iliruhusu gari kutoka bandarini na kuhifadhiwa eneo salama na si kutembea kabla ya kukamilisha kodi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum, alisema mhusika tayari ametakiwa kulipa kwa pamoja na kuarifiwa kwa maandishi kwa mujibu wa barua ya Oktoba 3, mwaka huu, baada ya kupokea maombi ya kulipa kidogo kidogo.

Dk. Saada alisema maombi ya msamaha wa kodi yalikataliwa kutokana na kuwasilishwa kinyume cha sheria ya uwekezaji vitengauchumi licha ya kuidhinishwa na ZIPA.

## Kituo magonjwa ya mlipuko kujengwa

**Na Mary Geofrey,** BUKOBA

WIZARA ya Afya imesema itajenga kituo cha magonjwa ya mlipuko katika Mkoa wa Kagera ikiwa ni moja ya mkakati wa serikali katika kukabiliana nayo nchini.

Kwa sasa serikali inajenga kituo hicho katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) Tawi la Mloganzila na Mkoa wa Kagera ambao umeonekana kuwa lango la mwingiliano wa nchi jirani.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu alibainisha hayo juzi wilayani Bukoba mkoani Kagera alipozungumza na wataalamu wa afya wa halmashauri zote kuhusu mipango mikakati ya kukabiliana na ugonjwa wa Ebola.

Alisema magonjwa mengi yanatokea katika mkoa huo ambao umepakana na nchi jirani za Uganda, Kenya, Rwanda, Burundi, Sudan ya Kusini na Demokrasia ya Congo.

"Ipo haja kama serikali kuweka hapa kituo cha kutoa huduma za magonjwa ya milipuko, kitakuwa kikubwa chenye miundombinu mizuri, vifaa vya kisasa na sehemu ya kuwatenga wanaohisiwa, wenye ugonjwa na ambao wanapewa tiba," alisema.

Ummy aliagiza litafutwe eneo kubwa kwa sababu asili ya ukanda wa ziwa una magonjwa ya milipuko ambayo hutokea katika mikoa ya Kigoma au Katavi.

Vilevile, waziri huyo alisema serikali inapitia upya mwongozo wa watoa huduma za afya ngazi ya jamii na kuwapa mikataba ya ajira ya miezi mitatu ili kupima kazi na uwezo wao.

Alisema huo ni msimamo na mtazamo wa Jumuiya ya Kimataifa kuhusu afya unaowatambua watoa huduma za afya ngazi ya jamii hadi madaktari.

Alisema serikali itawapa mafunzo ya awali na endelevu katika maeneo waliyobobea kufanya kazi.

"Mwongozo unasema hawa watoa huduma lazima walipwe, tusidanganyane hakuna anayetaka kufanya kazi bure, wote tunataka tulipwe, hivyo tutawaandalia mikataba ya ajira angalau kwa miezi mitatu mitatu ingawa nilitamani iwe miezi sita na tupime kazi na uwezo, wapewe pia mafunzo ya muda mfupi mfano wa malaria abobee hayo, Ukimwi na siyo unachanganya," alisema.

Ummy pia alisema watabadili mwongozo huo ili kuboresha watoa huduma za afya ngazi ya jamii kuwa wawili katika kila kitongoji tofauti na ilivyo sasa wawili katika kila kijiji.

"Kama kijiji kina vitongoji vitatu ina maana wataalamu wa afya ngazi ya jamii watakuwa sita, huu ni utaratibu wa halamshauri zote za wilaya," alisema Ummy.

# Serikali yatoa maagizo saba kukabili upungufu mvua za vuli

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Waziri Mkuu imetoa maelekezo saba kwa kamati za usimamizi wa maafa kwenye mikoa, wilaya, kata na vijiji, kukabiliana na kuwapo na mvua za vuli chini ya kiwango huku ikitahadharisha hali hiyo itasababisha upungufu wa umeme na chakula.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, George Simbachawene, alitoa maelekezo hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hatua za kuchukua kwa umma, kamati na sekta mbalimbali.

Alitoa tahadhari hiyo kutokana na utabiri wa mvua za msimu wa vuli ambazo hunyesha kati ya Oktoba na Desemba.

Simbachawene alisema kutokana na utabiri wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), kuna baadhi ya maeneo ya nchi ambayo hupata mvua hizo, yatapata kwa kiwango cha chini. "Mvua zinatarajiwa kuwa chini ya wastani katika maeneo mengi ya mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Mara, Shinyanga, Simiyu, Kigoma, Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Dar es Salaam, Pwani, Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba," alisema.

Kutokana na hali hiyo, alisema kutakuwa na vipindi virefu vya ukavu hali itakayosababisha madhara mbalimbali ikiwamo upungufu mkubwa wa unyevunyevu katika udongo katika maeneo mengi unaoathiri ukuaji wa mazao.

"Kina cha maji katika mito, mabwawa na hifadhi ya maji ardhini kinatarajiwa kupungua hususan katika maeneo mengi ya yanayotegemea mvua za vuli hivyo kusababisha upungufu wa maji kwa matumizi mbalimbali na mlipuko wa magojwa unaweza kujitokeza kutokana na upungufu wa upatikanaji wa maji safi na salama," alisema.

"Upatikanaji wa umeme utaathiriwa kutokana na kuwa kiasi kikubwa huzalishwa kwa kutumia maji kwa hiyo tukikosa mvua ya kutosha katika misimu hii ambayo husaidia kujaza mabwawa yetu maji basi umeme tutakuwa na tatizo la umeme pia," alisema.

Kutokana na tahadhari hiyo, alisema ofisi hiyo inaagiza kamati hizo kuandaa mipango ya dharura itakayoelekeza hatua za kuchukua kwa kila taasisi na wananchi.

Alizitaka kamati zishirikishe wadau wa maafa kuhakikisha upatikanaji wa mbegu zinazokomaa kwa muda mfupi pamoja na utunzaji wa chakula cha binadamu na malisho ya mifugo.

"Wadau wote na wananchi wanaelekezwa kuchukua hatua za kuzuia madhara yanayoweza kusababishwa na mvua kuwa ndogo ikiwemo kupanda mazao yanayokomaa mapema na kuvuna maji," alisema.

Pia alizitaka kamati hizo zichukue hatua za kuzuia milipuko ya magonjwa yanayojitokeza kutokana na upungufu wa upatikanaji wa maji safi na salama.

Kadhalika, aliagiza kuimarisha udhibiti wa maeneo ya hifadhi za wanyamapori ikiwa ni pamoja na kuzuia muingiliano kwa kadri inavyowezekana.

Simbachawene alisisitiza kuwa eneo la kilimo ndiyo litaathirika kwa kiasi kikubwa kwa kuwa mvua hizo zinategemea kuongeza kiwango kikubwa cha chakula kwenye maeneo hayo na kushauri yapandwe mazao ya muda mfupi ili kustahimili.



Mkuu wa Kitengo cha wateja wadogo wa Benki ya Afrika, Ninael Mndeme (wa pili kushoto) na Meneja wa Benki hiyo tawi la Mtwara, Timoth Mwakipembe (wa pili kulia), wakiwahudumia wateja waliotembelea tawini hapo, katika kusherehekea wiki ya huduma kwa wateja juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walimu wapigiwa chapuo kutumia benki yao

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

WALIMU nchini wamehimizwa kuweka amana zao kwenye benki ya Mwalimu Commercial kwa ajili ya maisha yao ya baadaye.

Kaimu Rais wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Mwalimu Dinna Mathamani, kwenye Mkutano Mkuu wa Sita wa Wanahisa wa benki hiyo uliofanyika jijini hapa juzi.

"Kwa sisi wanahisa tunaona mwelekeo mzuri wa benki yetu. Mimi kama kiongozi wa Chama cha Walimu nawahimiza walimu kuendelea kuweka amana zenu kwenye benki yetu ili tuendelee kupata manufaa zaidi," alisema.

Kaimu Katibu Mkuu wa CWT, Maganga Japhet, kama chama wamekuwa bega kwa bega na benki kwa sasa watumishi wote ambao ni wanachama wa CWT wanapitishia mishahara yao Mwalimu Commercial Bank.

"Walimu wana hisa asilimia 35, hivyo ni wajibu wetu kuhakikisha tunaiimarisha benki yetu ili kufikia malengo ya kuanzishwa kwake," alisema.

Awali, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Mwalimu Commercial Bank, Francis Ramadhani, aliwapongeza wanahisa wote kwa hatua ambayo benki imefikia kwa sasa kwa kuwa kuanzia Julai, mwaka jana, benki ilianza kutengeneza faida mwezi hadi mwezi.

"Benki pia imekuza thamani ya mali zake kwa asilimia 53 na kufikia Sh. bilioni 58 kutoka Shilingi bilioni 38," alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Richard Makungwa, aliwahakikishia wanahisa na wateja wa benki hiyo kuwa benki imeendelea kuimarisha mifumo ya kidijitali ambapo mteja anaweza kupata huduma za kibenki akiwa mahali popote kwa kutumia simu ya kiganjani au ATM kupitia kadi ya VISA.

"Nipende kusema walimu ni kundi la wateja wazuri sana. Najua wenzetu wanawawinda na sisi pamoja na udogo wetu, tunaweza kushindana na wenzetu walio katika soko. Nitumie fursa hii kuwahimiza walimu karibuni, rudini nyumbani, nyumbani kumenoga ili muone faida na maana ya ninyi kunzisha chombo chenu cha kifedha ambacho nia ilikuwa kuwakwamua kiuchumi," alisema Makungwa.

# Mwekezaji mbolea atimka kisa urasimu

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MWEKEZAJI aliyetaka kujenga kiwanda cha mbolea chenye thamani ya Sh. bilioni 1.2 katika wilaya ya Iramba mkoani hapa, ameondoka na kwenda kuwekeza Misri baada ya kuzungushwa kupata kibali.

Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda, alisema hayo jana kwenye kikao cha kujadili mkakati wa kuongeza uzalishaji wa alizeti ambacho kilihudhuriwa na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, wakuu wa wilaya, wakurugenzi na wenyeviti wa halmashauri na maofisa kilimo.

Mwenda alisema mwaka jana wilaya hiyo ilipata mwekezaji kwa ajili ya kujenga kiwanda cha mbolea na serikali ya wilaya ikampa ushirikiano na kufanya taratibu zote zinazotakiwa za uwekezaji ikiwa ni pamoja na kumpatia eneo la kujenga kiwanda hicho.

Alisema pamoja na jitihada zote zinazofanywa na serikali ya wilaya ambazo zilikamilika, mwekezaji huyo alikwamishwa na wizara inayohusika na masuala ya uwekezaji, hivyo kuondoka na kwenda kuwekeza Misri.

Katika kikao hicho, Bashe alisema katika mwaka wa fedha wa 2023/24 serikali itatenga fedha Sh. bilioni 4.6 kwa ajili ya kununua zana za kilimo katika mkoa wa Singida.

Hatua ya Waziri Bashe kutangaza kutenga fedha hizo ilitolewa baada ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mkakati ya kuongeza uzalishaji wa alizeti katika mkoa wa Singida, Justice Kijazi, kueleza mikakati itakayosaidia kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

Kijazi alisema ili kuongeza uzalishaji wa alizeti kila halmashauri ipatiwe vituo vya kukodisha zana za kilimo ambapo wakulima watakuwa wakifika na kukodisha zana hizo.

Alisema katika msimu wa kilimo wa 2022/23 mkoa wa Singida ekari 631,391 za alizeti zitalimwa ambazo zinatarajia kuzalisha tani 492,485 zitakazozalisha tani 159,110.5 sawa na asilimia 44.2 ya mafuta yanayoingizwa nchini.

Kijazi alisema ili kufikia malengo hayo, mkoa unahitaji kupata tani 1,262.5 za mbegu kwani mkoa una fursa kubwa ya uzalisha alizeti kutokana na hali ya hewa nzuri iliyopo.

Aidha, mkoa una viwanda 221 vya kusindika alizeti vinavyohitaji tani 635, 465 lakini bahati mbaya uzalishaji wa miaka mitano kuanzia msimu wa kilimo wa 2017/2018 hadi 2021/2022 haujawahi kutosheleza viwanda.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hongera Tembo Warriors kuitangaza vizuri Tanzania

**KWA** mara ya kwanza mwaka huu timu mbili za Tanzania kupitia mchezo wa soka zimepata nafasi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia.

Timu ya kwanza kupata tiketi hiyo ilikuwa ni ya walemavu inayojulikana zaidi kwa jina la Tembo Warriors na kufuatiwa na Kikosi cha Wasichana wenye umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls).

Katika kujiandaa na fainali hizo za dunia, Tembo Warriors ilianza kuhudumiwa na serikali katika kambi ya hapa nchini na baadaye ikapelekwa mapema Uturuki ili kuendelea kujifua, lakini pia kupata nafasi ya kucheza michezo ya kimataifa ya kirafiki.

Ikiwa huko iliweza kufanya vyema katika mechi zake za majaribio na baadaye ikaingia rasmi kwenye fainali za Kombe la Dunia.

Ikishiriki kwa mara ya kwanza, Tembo Warriors imefika hadi hatua ya robo fainali, lakini ikashindwa kufurukuta mbele ya wenzao kutoka Haiti kwa kuchapwa mabao 4-1.

Pamoja na kupoteza mchezo huo, Tembo Warriors ilionyesha kiwango kizuri katika mechi hiyo na zile za hatua ya makundi kama vile inaundwa na wachezaji wenye uzoefu na michuano hiyo ya kimataifa kwa kuwavutia mashabiki na wadau mbalimbali waliokuwa wakiifuatilia timu hiyo.

Tunapenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Tembo Warriors kwa mafanikio ambayo wameyapata katika mashindano hayo na kuondolewa kwenye fainali za mwaka huu, iwe ni mwanzo wa maandalizi ya kukata tiketi ya kushiriki fainali zijazo.

Ni wazi timu hiyo iliundwa na wachezaji waliokusanywa kutoka sehemu mbalimbali hapa nchini, lakini umefika wakati viongozi wa chama (TAFF), ambacho kinasimamia mchezo huo kuanzisha ligi za wilaya, mikoa na baadaye Kanda ili kusaka vipaji vipya.

Kwa kuanzisha ligi za wilaya, mikoa na baadaye mashindano ya ngazi ya Taifa, kutasaidia kuzalisha wachezaji wengine ambao wataongeza nguvu katika kikosi cha Tembo Warriors, lakini itatoa nafasi kwa nyota waliopo kujiimarisha na kuwa tayari kupambana kwenye ngazi ya Afrika.

Ili mchezo huo uendelee, ni wakati sahihi kwa TAFF kushirikiana kwa karibu na Baraza la Michezo la Taifa (BMT), kuhakikisha mchezo huo unachezwa katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

Ni wazi kwa kufanya hivyo, Tembo Warriors itaendelea kupata nafasi ya kushiriki mashindano mbalimbali ya kimataifa na isionekane mwaka huu imefuzu kwa kubahatisha.

Timu au wachezaji walioandaliwa kuanzia ngazi za awali, huzaa matunda mazuri kutokana na misingi ambayo wanakuwa wamejengewa na hivyo, isionekane kama kwa kufanya mchakato huo, ni kuwaondoa wachezaji walioko sasa, bali ni mwendelezo wa kutaka kuiona Tembo Warriors ikipeperusha vyema bendera ya Tanzania katika kila michuano ya kimataifa.


Mbali na serikali, huu ni wakati wa makampuni, taasisi na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi kujitokeza kuwekeza katika timu hiyo ambayo sasa inahitaji kuajiri wakufunzi na makocha wenye vigezo vya juu kwa lengo la kuwaimarisha wachezaji na kuwafanya wawe tayari kushindana.

Kama ambavyo, Tembo Warriors imefanya, tunaamini pia Serengeti Girls, ambayo imetoka Uingereza kuweka kambi na sasa inaelekea India katika Fainali za Kombe la Dunia, itapeperusha vyema bendera ya Tanzania.

Maandalizi ya timu zote mbili kushiriki fainali za Kombe la Dunia kwa kiasi kikubwa yamesimamiwa na serikali, kuendelea kujituma kutawafanya wadau wajitokeze kudhamini michezo yao ambayo kwa kiasi kikubwa imesaidia kuwapa ajira wachezaji, makocha, madaktari na maofisa wengine wanaosimamia shughuli za kila siku za timu hizo.

Wachezaji huu ni wakati wenu wa kuendelea kupambana na kumpa heshima, Rais, Samia Suluhu Hassan, ambaye anataka kuona Tanzania inafanya vyema katika michezo na mashindano yote.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Muungwana Lazima Nilonge

# Kazi kuzilinda nafasi nne michuano CAF ianze leo

Na Adam Fungamwango

**TIMU** tatu zinazoiwakilisha Tanzania Bara katika michuano ya kimataifa zitaanza leo kampeni ya kuzitetea nafasi za kupeleka timu nne katika mashindano yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu, Yanga leo watakuwa nyumbani kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kucheza dhidi ya Al Hilal kutoka Sudan kuanzia saa 10:00 jioni , katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika na saa 2:00 usiku, wawakilishi wengine wa Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho, Azam FC watakuwa ugenini Libya kuwakabili wenyeji Al Akhdar SC, mechi ikitarajiwa kupigwa kwenye Uwanja wa Martyrs of February.

Kesho kwenye Uwanja wa Estadio 11 de Novembro, nchini Angola, Simba itashuka kuwavaa Primeiro de Agosto kuanzia saa 12:00 jioni kwa saa za Afrika Mashariki.

Kwenye mechi zote hizi ambazo mbili zinacheza uganini na moja nyumbani, matarajio ya ushindi wa Watanzania ni makubwa kutokana na jinsi timu hizi zilivyojipanga.

Hii inatokana na usajili mkubwa ambao imefanya pamoja na ukweli kuwa ndiyo kwa sasa zinatawala soka la Tanzania.

Zina wachezaji kutoka pande mbalimbali za Afrika ambao wanatarajia kucheza mechi hizo bila hofu yoyote ile.

Wakati ratiba hii inatoka, Rais wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF), Wallace Karia, alikaririwa akisema anatamani timu zote zifanye vyema ili kuzilinda nafasi nne ambazo Tanzania imezipata.

Ukweli ni kwamba ni misimu miwili mfululizo sasa Tanzania inapeleka timu nne, mbili katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na nyingine mbili kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho, lakini hizi si nafasi za kudumu.

Ni nafasi zinazotegemea kufanya vizuri kwa timu zinazoshiriki michuano hiyo ya kimataifa.

Ikumbukwe kufanya vizuri kwa Simba kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ndiko kwa mara ya kwanza kuliifanya Tanzania kuingiza timu nne mwaka 2019, huku zali ikiidondokea KMC ambayo ilicheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza na moja kwa moja ikaenda kucheza kimataifa kabla ya kutolewa na AS Kigali ya Rwnada.

Kutolewa kwa Simba na UD Songo ya Msumbiji mechi ya raundi ya kwanza kuliifanya Tanzania kunyang'anywa tena nafasi ya kuwakilishwa na timu nne kwa sababu kuna klabu za nchi nyingine zilikuwa zimevuna pointi na kuipiku Bongo, lakini msimu uliofuata Wekundu wa Simba walifanya tena vyema na nafasi zikarejea.

Kwa sababu tayari timu, nchi na mashabiki wameshaonja ladha ya kupeleka timu nne, itakuwa ni aibu na simanzi kubwa timu zetu zikatolewa kwenye hatua hii na kuzipa mwanya timu za nyingi zingine kuizidi Tanzania pointi mwakani tukarejea kupeleka timu mbili tu.

Kwa sasa Ligi Kuu Tanzania Bara inatajwa kuwa moja kati ya ligi bora hapa barani Afrika. Kutokana na hali hiyo timu za Simba, Yanga na Azam zina dhima ya kuthibitisha hilo kwa kushinda mechi za leo na kesho, pia kupigana kufa na kupona kusonga mbele ili kuongeza pointi na kuendeleza uwezekano wa kupeleka timu nne msimu ujao.

Ikumbukwe kama Simba na Yanga zikitinga makundi tu, Azam nayo ikapita kwenye hatua hii, si tu Tanzania itaongeza pointi ambazo zitaiwezesha msimu ujao kupeleka timu nne tu, lakini hata misimu miwili mfululizo bila kutegemea matokeo mazuri ya msimu ujao.

Hiki ndicho kinachotakiwa kifanywe kwa timu za Tanzania. Kipindi hiki ambazo timu zinaonekana ziko vizuri ndiyo kipindi cha kukusanya pointi nyingi kiasi kuwa kama nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Misri, Tunisia na Morocco ambao pointi zao hata kama misimu mitatu hakuna timu yoyote itakayoshiriki michuano ya kimataifa, hakuna nchi ya kuzidondosha na kuzipiku zikapeleka timu mbili.

Pia, tunaiombea heri, Kipanga ya Zanzibar ambayo leo inacheza dhidi ya Club Africaine ya Tunisia katika mechi ya hatua ya kwanza ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Kipanga ikiwatoa Waarabu hao, itaweka rekodi ya kutinga hatua ya makundi kwa mara ya kwanza.

Kila la heri timu zote za Tanzania kwenye michuano hii mikubwa barani Afrika.

## Tiketi mwendokasi kuuzwa kidigitali

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), umesema wateja wa mabasi hayo wataanza kutumia kadi janja kununua tiketi kuanzia mapema mwakani.

Meneja wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa DART, Ng'wananashigi Gagaga, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa kilele cha Wiki ya Huduma kwa Wateja, katika stendi ya mabasi yaendayo haraka Kariakoo.

Alisema ununuzi wa tiketi kwa kutumia kadi janja utawarahisishia watumiaji wa usafiri huo kutolazimika kukaa foleni muda mrefu kwa ajili ya kukata tiketi, hivyo kuwaondolea adha ya kupoteza muda kwenye vituo hivyo.

Alisema mfumo huo wa kukusanya nauli kupitia kadi janja, umesanifiwa na kutengenezwa na wataalamu wa ndani kutoka DART, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Fedha na Mipango na Wakala wa Serikali Mtandao.

"Mchakato wa ununuzi wa vifaa kusaidia huo mfumo kama mageti na kadi uko sehemu nzuri na tumeshatia saini mkataba na mkandarasi na ndani ya wiki 16 mfumo huu mpya utaanza kutumika hapa nchini na kwa sababu tunausimamia wenyewe tunaamini utakuwa na ufanisi sana kuliko ule wa zamani ambao ulisimamiwa na mkandarasi aliyeko Ubelgiji.

'Ule mfumo wa zamani ulikuwa ukisumbua unalazimika kupiga simu kwa mkandarasi Ubelgiji lakini huu wa sasa tumeusanifu wenyewe na tutausimamia wenyewe, hivyo ukisumbua inakuwa rahisi kuurekebisha," alisema.

Meneja huyo alisema kadi hiyo janja itakapoanza kutumika itatumika kwa awamu zote mbili za mradi wa mwendokasi awamu ya kwanza na ya pili na kuahidi kuwa awamu ya pili inatarajiwa kukamilika hivi karibuni na wananchi kunufaika na usafiri huo.

Naye Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa (DART), Eliphas Mollel, alisema wameanzisha kituo cha miito ya huduma (Call Center) kwa ajili ya kusikiliza na kutatua changamoto zinazowakuta watumiaji wa usafiri huo.

Alisema watu wamekuwa wakipiga simu na kueleza changamoto mbalimbali kama kuchelewa kwa mabasi na DART imekuwa ikizifanyia kazi changamoto hizo hivyo aliwashauri wananchi wanapoona changamoto kupiga simu ili tatizo hilo lishughulikiwe haraka.

Mollel aliwashukuru watumiaji wa usafiri huo na aliwahidi kuwa DART itaendelea kuboresha huduma hizo kwa kufanyia kazi changamoto zote zinazotolewa ili kuufanya usafiri huo kuwa wa kisasa zaidi.

"Katika wiki hii ya huduma kwa wateja ambayo hufanyika kila wiki ya kwanza ya mwezi Oktoba DART tumewapa fursa wateja wetu waseme wanatuonaje na changamoto wanazopitia na wametueleza na sisi tutazifanyia kazi," alisema Mollel.

Aidha, alisema miongoni mwa changamoto ambazo wananchi wengi wamezielezea ni uchache wa mabasi hali ambayo inawafanya wakae muda mrefu vituoni kusubiri na kushindwa kufika kwenye maeneo yao kwa wakati.



Meneja wa Huduma za Kidigitali wa Halotel, Caroline Majaliwa (kushoto), akishiriki zoezi la uchangiaji damu lililoendeshwa na kampuni hiyo pamoja na wafanyakazi kwa kushirikiana na Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni moja ya msaada wa kurudisha shukrani kwa jamii kuelekea kilele cha kuadhimisha miaka saba ya kutoa huduma za mawasiliano nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampuni yaadhimisha miaka 7 ya huduma ya uchangiaji damu

**Na Mwandishi wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Halotel na wafanyakazi wake, jana ilishiriki uchangiaji damu salama ikiwa sehemu ya kusherekea miaka saba ya utoaji wa huduma za mawasiliano nchini.

Akizungumza wakati wa uchangiaji huo uliofanyika katika ofisi za makao makuu ya Hatolel, Mkuu wa Kitengo cha Bidhaa na Mawasiliano wa kampuni hiyo, Sakina Makabu, alisema jana kuwa katika kuhakikisha wanasaidia sekta ya afya, wameona ni vyema kuchangia damu ili kuokoa maisha ya Watanzania wenye uhitaji katika hospitali mbalimbali nchini. Uchangiaji huo ulifanyika katika makao makuu ya kampuni hiyo, Dar es Salaam.

Alisema, kuchangia damu ni moja ya taratibu ambazo kampuni imejiwekea kama msaada wa kurudisha shukrani kwa jamii pamoja na kuunga mkono jitihada za serikali kupitia sekta ya afya katika kukabiliana na uhaba wa damu katika hospitali au vituo vya kutolea huduma za afya.

Takwimu kupitia Wizara ya Afya zinaonyesha kuwa uhitaji wa damu ni mkubwa kwa wajawazito, watoto, watu waliopata ajali na wanaofanyiwa upasuaji.

"Halotel kwa kushirikiana na Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), tumeendeleza kazi hii ya kuchangia damu kama hitaji maalum na ishara ya upendo kwa vitendo kwa Watanzania ambao pia ndio wateja wetu.

"Tunatambua changamoto mbalimbali zinazoikumba sekta ya afya hasa katika upande wa uhitaji na upatikanaji wa damu katika hospitali na vituo vya afya kwa wagonjwa, hivyo tumeamua kuendelea kuunga mkono juhudi za utatuzi wa changamoto hii, kwa kujali na kutambua umuhimu, kampuni na wafanyakazi tumeamua kurudisha upendo huu kwa jamii," alisema.

Mmoja wa wafanyakazi waliochangia damu, Dalili Musa, alisema: "Tunajisikia furaha sana kushiriki katika zoezi hili kwa sababu huduma hii tuliyoifanya hapa inaweza kuonekana ni kidogo lakini inaenda kuokoa maisha ya watu. Hakika ni kitendo cha kuonyesha upendo na kinaleta faraja sana," alisema.


Licha ya Halotel kupiga hatua kubwa katika kusambaza huduma za mawasiliano na intaneti yenye kasi na ubora wa hali ya juu ya 4G maeneo mengi nchini, pia imekuwa ikijihusisha na kutoa misaada mbalimbali kwa jamii ya watanzania.

Naye Mtaalamu wa Dawa za Usingizi na Ganzi kutoka MOI, Juma Saidi, alishukuru kampuni ya halotel kuwaita na kusaidia wafanyakazi kuchangia damu.

"Tunaomba mashirika ya umma, mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO) na wadau wengine watualike katika ofisi zao ili wapate nafasi ya kuchangia damu kwa sababu uhitaji ni mkubwa sana na kwa siku tunahitaji chupa 40 kila siku," alisema.

Alisema wamefarijika sana kwa kampuni hiyo kuchangia damu, hivyo akawashukuru kwa kuthamini afya za wananchi pia kwa kuunga mkono jitihada za kuisaidia sekta ya afya nchini.

## KABWELA



# Abood amshukuru Samia kupunguza vifo vya uzazi

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

MBUNGE wa Jimbo la Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood, amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kusaidia kupunguza vifo vya kina mama wajawazito na watoto baada ya kutoa vifaa vya kisasa katika jengo la upasuaji la Hospitali ya Sabasaba iliyoko Manispaa ya Morogoro.

Abood alitoa shukrani hizo jana wakati akikabidhi vifaa hivyo kwa hospitali hiyo, vikijumuisha meza ya kisasa kwa ajili ya upasuaji na taa mbili za kufanyia upasuaji ambavyo vimekuwa vikitumika katika hospitali nyingine za rufani.

Akizungumza baada ya kukabidhi vifaa hivyo, Abood alisema Rais Samia amekuwa akiguswa na vifo vya kina mama vinavyotokana na uzazi na mkakati alionao kwa sasa ni kuhakikisha vifo hivyo nchini vinakwisha.

"Rais wetu Mama Samia anaumizwa sana na vifo vinavyotokana na uzazi, hivyo kwa sasa amekuwa akihakikisha vifo hivyo vinapungua na hata kwisha, ndiyo maana ametupatia hivi vifaa vyenye thamani kubwa kwa ajili ya operesheni katika Hospitali yetu ya Manispaa ya Morogoro," alisema Abood.

Aliongeza kuwa katika kumuunga mkono Rais Samia, yeye kama mbunge wa jimbo hilo, atahakikisha anatafuta vifaa vingine vilivyosalia ikiwamo mashine ya usingizi ambayo inatumika kwa ajili ya kutoa huduma za upasuaji na kukamilisha ujenzi wa jengo lake.



Mbunge wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood (mwenye miwani) akikabidhi vifaa kwa ajili ya upasuaji kwa Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Sabasaba jana, Dk. Enry Mungia. Wa kwanza kushoto ni Mganga Mkuu wa Manispaa hiyo, Dk. Charles Rashid. **PICHA: ASHTON BALAIGWA.**

Mbunge huyo alisema katika kuhakikisha anaboresha huduma za afya, ameamua kutoa vifaa vya nishati ya umeme wa jua, kufanya ukarabati wa majengo mbalimbali na kutengeneza mfumo wa maji katika Zahanati ya Kichangani iliyoko Manispaa ya Morogoro kwa gharama Sh. milioni 20.

Awali Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Sabasaba, Dk. Henry Mungia alisema tayari wameanza ujenzi wa jengo la upasuaji tangu mwezi Juni mwaka huu kutokana na kuwapo shida nyingi za uzazi zinazotokea katika kitengo cha wodi ya wazazi na kulazimika kuzipeleka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro.

Alitolea mfano katika kipindi cha mwezi Aprili mwaka huu rufani zilizopelekwa zilikuwa 65, mwezi Mei 68 na mwezi Juni zilikuwa 57.

Alisema ujenzi wa jengo la upasuaji unatarajiwa kugharimu Sh. milioni 37 kwa kutumia fedha za ndani ambapo kwa sasa ujenzi wake umefikia asilimia 80.

Mganga Mkuu wa Manispaa ya Morogoro, Dk. Charles Rashid, alisema kutokana na kupatikana kwa vifaa hivyo, halmashauri imejipanga kuhakikisha inasaidia kumalizia ujenzi wa jengo hilo ili huduma za upasuaji zianze kutolewa mwezi Desemba mwaka huu.

# GGML wadhamini mkutano mkuu wanajiolojia Tanzania

**Na Mwandishi Wetu,**
ARUSHA

KATIKA kuunga mkono ukuaji wa fani mbalimbali nchini, Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) imedhamini mkutano mkuu wa mwaka wa wanajiolojia wa Tanzania unaofanyika mkoani Arusha.

Mkutano huo ambao ulianza Oktoba 4 na kumalizika jana, uliratibiwa na Chama cha Watalaamu wa Jiolojia Tanzania (TGS) kinachokadiriwa kuwa na wanachama zaidi ya 300.

Akizungumza na Nipashe juzi, Mkuu wa Kitengo cha Jiolojia katika Kampuni ya GGML, Eric Kalondwa alisema kampuni ya GGML imetoa Sh. milioni 25 kudhamini mkutano huo uliofunguliwa na Waziri wa Madini, Dk. Doto Biteko kwa niaba ya Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

Alisema katika mkutano huo ambao hufanyika kila mwaka kwenye mikoa tofauti, jumla ya wanajiolojia 11 kutoka mkoani Geita wameshiriki.

Aliongeza kuwa mkutano huo umelenga kubadilisha na uzoefu kwa sababu kuna programu mbalimbali zinazolenga kuwaweka pamoja watu wenye fani zinazofanana.

Alisema wafanyakazi wa GGML ambao pia ni wana fani hiyo ya jiolojia, wamefaidika kwa namna mbalimbali tangu kianzishwe chama hicho.

Alisema mkutano wa mwaka huu unalenga kukazia suala la upatikanaji wa bodi ya wanajiolojia hasa ikizingatiwa fani hiyo inajumuisha watu kutoka maeneo mbalimbali ikiwamo wanaofanya kazi kwenye uchimbaji wa mafuta, kwenye maji na madini ya aina mbalimbali, ikiwamo dhahabu.

Alikiri kuwapo tatizo la uhaba wa wanawake kusomea fani hiyo, akisisitiza kuna haja wanawake kusomea fani ya jiolojia kwa kuwa haihitaji kuwa na nguvu kubwa ili kukidhi vigezo vya kuwa mwanajiolojia.

"GGML kwa kweli inafanya vizuri sana kuendeleza wanajiosayansi toka wanapokuja kujifunza kwa vitendo na wanaokuja kazini.

"Wale wanaopitia kwenye mgodi wetu hakika wanasifika kwa mapokeo makubwa tunayowapatia kulingana na programu ya mwaka ambayo huwa tunawaandalia," alisema.

Wanajiosayansi ni wataalamu waliosomea na wenye uzoefu wa fani za jiolojia (miamba), jiofizikia, jiokemia, jioteknolojia na jiolojia ya mazingira na nyinginezo.

Awali akifungua mkutano huo, Waziri wa Madini, Dk. Biteko alisema wizara iko katika hatua za mwisho za kukamilisha mchakato wa kuanzishwa bodi ya wanajiolojia na kuongeza kwamba baada ya serikali kukamilisha sehemu yake, itatoa nafasi kwa wadau kutoa maoni kuhusu namna gani bodi hiyo iundwe, namna itakavyosimamiwa, masuala yatakayohusisha vyanzo vya fedha na kuangalia masuala ya sheria.

Aliongeza kuwa wakati serikali inakamalimisha mchakato wa kuundwa kwa bodi ya wanajiolojia ni muhimu wajiolojia wakahakikisha wanaiendeleza taaluma ya jiolojia ili kuipatia nchi heshima ikiwamo kuwawezesha wawezekaji kupata taarifa sahihi na hivyo kuvutia uwekezaji zaidi kwenye sekta ya madini.

Rais wa Chama cha Wataalamu wa Jiolojia Tanzania, Prof. Abdulkarim Mruma alieleza hadhira kuhusu utajiri wa kijiolojia ambao Tanzania imebarikiwa kuwa nao na kuelelezea namna bora ya kuitumia taaluma hiyo kwa maendeleo ya nchi na jamii nzima.

## Bashe: Tanzania ina ziada chakula tani milioni mbili

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe amesema nchi ina ziada ya chakula zaidi ya tani milioni mbili, hivyo Watanzania wasiwe na hofu kuhusu uwezekano wa kutokea upungufu wa chakula licha ya baadhi ya vyakula kuuzwa kwa bei kubwa.

Pia amefafanua sababu za mchele kupanda bei kuwa ni kutokana na nchi zinazoizunguka Tanzania kununua mchele kwa wingi nchini wakati awali zilikuwa zinanunua katika nchi za mashariki ya mbali.

"Ninataka niwatoe hofu Watanzania hatutakuwa na upungufu wa chakula na siyo lazima sana kwamba bidhaa zinapopanda bei, basi kuna upungufu wa chakula," alisema Bashe alipozungumza na waandishi wa habari jana mjini hapa kuhusu hali ya chakula nchini.

Alisema katika kipindi cha miaka sita hadi saba nchi haijawahi kuwa na hifadhi ya chakula kubwa kama ilivyo sasa ambapo miaka yote hifadhi iliyokuwa kubwa ilikuwa ni wastani usiozidi tani 50,000.

Akitoa takwimu za uzalishaji wa chakula kwa kipindi cha miaka mitatu, Bashe alisema msimu wa 2019/20 uzalishaji ulikuwa tani milioni 16.293, mwaka 2020/21 ulikuwa tani milioni 18 na msimu wa kilimo wa 2021/22 zilizalishwa tani milioni 17.4.

"Mahitaji ya chakula katika nchi ni wastani wa tani milioni 15.1, hivyo tafsri yake ni kwamba tuna ziada ya chakula zaidi tani milioni mbili ambazo zipo mikononi mwa Watanzania na serikali," alisema.

Bashe alisema mahindi yaliyosafirishwa kwenye nje kuuzwa kuanzia Januari hadi Agosti 2022 ni tani 395,830 yenye thamani ya Sh. bilioni 326.

Kuhusu bei za vyakula, alisema katika kipindi cha kuanzia 2019 hadi 2022 ongezeko la bei ya mahindi ni kutoka Sh. 63,600 hadi kufikia 72,525 ambalo ni ongezeko la wastani usiozidi asilimia 14 wakati mchele bei imeongezeka kutoka 168,800 hadi 194,638, sawa na asilimia 15.3. "Watanzania wanajiuliza kwanini mchele nao unapanda? Ninataka niwaambie kwa muda mrefu nchi zinazotuzunguka kama Rwanda, Uganda walikuwa wananunua mchele nchi za mashariki ya mbali kama Indonesia, Vietnam na kwingineko wakati nchi yetu sera zilikuwa hazitabiriki," alisema.

Bashe sasa hivi baada ya nchi hizo kuona nchi yetu imekaa vizuri na mipaka haifungwi, zimeanza kununua mchele kwa kasi, hivyo inatoa changamoto kuongeza uzalishaji.

Bashe pia alisema bei ya pembejeo katika kipindi cha kuanzia mwaka 2019 hasi 2020 imeongezeka wastani wa Sh. 50,000 ambapo mpaka msimu wa mwaka jana bei ilifikia Sh. 140,000 kwa mfuko ambayo ni ongezeko la asilimia 100.



# DC atangazia kiama wakuu shule watakaozembea ujenzi madarasa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arusha, Said Mtanda, ametangaza mkakati mpya wa serikali wa kuwashusha vyeo wakuu wa shule za umma, watakaoshindwa kutekeleza miradi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika muda usiozidi siku 75.

Mtanda, alitangaza mpango huo jana wakati wa kikao na wakuu wa shule zitakazonufaika na mradi huo wa madarasa, huku akisisitiza uadilifu kwenye usimamizi wa miradi hiyo.

"Pochi la mama (Rais Samia Suluhu Hassan) limefunguka. Ametuletea Sh. bilioni mbili kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 100 kwenye shule 20 za Halmashauri ya Jiji la Arusha.

"Kwa hili hapa, sitakuwa na mchezo na fedha hizi hasa kwa mkuu wa shule atakayeshindwa kutekeleza mradi ndani ya siku zilizopangwa. Yeyote ajiandae maana nitamshusha cheo cha ukuu wa shule," alisema.

Kutokana na uharaka wa vyumba hivyo, mkuu huyo wa wilaya, alimwagiza Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Arusha, Hargeney Chitukulo, kuhakikisha wakuu wa shule wanapewa miongozo ya matumizi ya fedha hizo, ikiwa ni pamoja na kuundwa kwa kamati zote muhimu.

Aidha, Mtanda alitoa tahadhari kwa wakuu wa shule hizo, kutokubali kupokea maelekezo kutoka kwa wakuu wa idara, hasa kitengo cha manunuzi, ya kupokea maelekezo ya wapi wakanunue vifaa vya ujenzi.

"Wakuu wa shule undeni kamati zenye meno, sitaki kamati za kupokea maelekezo ya wapi mkanunue vifaa kwa gharama kubwa. Lengo hapa la kamati ni kupunguza gharama na kusimamia miradi itekelezeke kwa viwango vinavyatakiwa," alisema.

"Nitafanya ziara mahususi pamoja na maofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kwa ajili ya kuwachukulia hatua wakuu wa shule, ambao watakuwa wameshindwa kusimamia miradi hii kikamilifu pamoja na kamati husika," alisema.

Awali, Kaimu Mkurugenzi huyo, alisema ili ujenzi huo ufanyike kwa ufanisi tayari wameshaunda kamati, kama muongozo unavyoelekeza ikiwa ni pamoja na kila shule kupata mkuu wa idara, ngazi ya Halmashauri ambaye atakuwa mlezi kwa ajili ya kurahisha shughuli za ujenzi.



Wafanyakazi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Kanda ya Kaskazini, wakiwa na wadau wa huduma dhibitiwa, wakifurahia keki, kama ishara ya ushirikiano, baada ya kikao cha kukusanya maoni kuhusu huduma zinazodhibitiwa na EWURA, jijini Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# CCM yamvua uanachama mwenyekiti kijiji

**Na Anjela Mhando,** MWANGA

CHAMA cha Mapinduzi (CCM), Kata ya Kileo, Mwanga, mkoani Kilimanjaro, kimemvua uanachama Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Kituri, Thomas Mgalla, kwa tuhuma za kushiriki kumtorosha mtu anayedaiwa kuiba mabomba ya maji.

Mgalla pia, anatuhumiwa kupokea rushwa ya Sh. 500,000 ili kumsaidia mtuhumiwa kutoroka, huku mabomba yanayodaiwa kuibwa yakitajwa kuwa na urefu wa mita 400.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa CCM wa Kata ya Kileo, Norbert Abraham, mwenyekiti huyo ameshindwa kusimamia mali za umma zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni sita.

"Mbali na Mgalla, ni kweli wako wengine pia CCM imewasimamisha kwa miezi sita ambao ni Mwenyekiti wa Kitongoji A, Kara Abel pamoja na Upendo Msuya ambaye ni Mwenyekiti wa Kitongoji B cha Kijiji cha Kituri.

"Hawa wote wanatuhumiwa kushirikiana na mwenyekiti wa kijiji kwa sababu ni bosi wao. Wote hao walisimamishwa juzi na wananchi katika mkutano wa hadhara wa CCM uliofanyika katika kijiji cha Kituri," alisema.

Pia, Abraham alisema mwenyekiti huyo wa kijiji, ameshiriki kwa namna tofauti kujipatia fedha ya wizi wa bomba lililopotea kwa kuwa walimkamata mtuhumiwa aliyeiba bomba na yeye akashiriki kumtorosha kwa kupatiwa fedha hizo.

"Tukiwa wasimamizi wa ilani ya Chama cha Mapinduzi, hatuwezi kuiba. Mheshimiwa Rais ametuletea miradi ya maendeleo, halafu viongozi wanaoisimamia serikali wao wawe mstari wa mbele kuharibu," alisisitiza.

Kabla mwenyekiti huyo kung'olewa na washirika wake kusimamishwa kazi kupisha uchunguzi, wananchi walipiga kura ya kutokuwa na imani naye.

Diwani wa Kileo, Kuria Msuya, akizungumzia suala hilo, amekiri kuwa kiongozi huyo kuvuliwa uanachama, huku wenyeviti wawili wa kitongoji wakisimamishwa kazi kwa muda ili kupisha uchunguzi dhidi yao.

# Waajiri waagizwa upandishaji madaraja matakwa ya kisheria

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Muhagama, ameagiza waajiri wote nchini kutekeleza bila shuruti, suala la kuwapandisha madaraja wafanyakazi wao.

Aidha, amesema kwa sasa serikali kuu yenyewe inaendelea kushughulikia kero za malimbikizo ya mishahara na ajira mpya.

Waziri Mhagama, aliwakumbusha waajiri kufanya hivyo jana, wakati akifungua mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) yanayoendelea jijini hapa.

Muhagama, alimwakilisha Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliyekuwa mgeni rasmi katika ufunguzi huo.

"Waajiri wote hakikisheni mnafuatilia kwa karibu mienendo ya watumishi wa umma na mnakuwa na utaratibu mzuri wa kuhakikisha kila mtumishi anapanda daraja bila kucheleweshwa," aliagiza


Aidha, Waziri Muhagama alisema serikali inaangalia uwezekano wa kushirikisha watumishi wenye mahitaji maalumu kwenye mashindano hayo ya SHIMIWI kuanzaia mwaka ujao.

Alisema kuwa, uwapo wa timu za wenye mahitaji maalumu itasaidia kuongeza wigo wa michezo, lakini na kuwawezesha watumishi wa umma wenye mahitaji maalumu nao kushiriki na kuonesha uwezo.

"Niwaombe SHIMIWI kuangalia uwezekano wa kuwa na timu za wenye mahitaji maalumu ili nao waweze kupata fursa ya kushiriki katika michezo hiyo na kuongeza wigo wa michezo," alisema

Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE) na Katibu Mkuu wa Shirikisho la Wafanyakazi nchini (TUCTA), Henry Mkunda, kwa nyakati tofauti walieleza kuwa jukumu lao ni kuwajengea uwezo wafanyakazi ili kujenga tabia ya kuwekeza hususan kwenye kilimo kabla ya kustaafu.

"Tunafanya mafunzo ya wafanyakazi kuhusu kujiandaa kustaafu kwani wanataka wafanyakazi wasisubiri chama cha wafanyakazi kiendelee kuwafundisha mambo mbalimbali yanayohusu haki zao katika sehemu za kazi wameona ni vyema wawaandae wafanyakazi kujua wataishije hata watakapostaafu," alisema





# Wahamiaji haramu kusafirishwa kwao

**Na Hamida Kamchalla,**
TANGA

MKUU wa Jeshi la Magereza nchini, Kamishna Jenerali (CGP) Mzee Ramadhan Nyamka, amesema serikali inafikiria kuwasafirisha kwenda makwao wafungwa ambao ni wahamiaji haramu ili kuondoa gharama inazotumia kuwahudumia.

Wahamiaji hao watakaosafirishwa ni wale waliomaliza vifungo katika magereza mbalimbali nchini.

Kamishna Jenerali huyo alieleza hayo jana, alipokuwa akizungumza na askari wa Gereza Kuu la Maweni, jijini Tanga.

Nyamka, alisema serikali inatumia fedha nyingi kuwapa mahitaji yao wakiwa gerezani bila wao kuwa na faida yoyote.

Alisema, wahamiaji hao wamekuwa wakiendelea kusababishia shida ambazo zinaizidishia serikali gharama mbali na zile za lazima, ambazo ni kuwahudumia katika Magereza waliyopo.

"Wenzetu kimataifa huwa hawalipendi hili jina lakini sisi kwa lugha yetu ya ndani tunasema ni wahamiaji haramu. Kwa kweli ni tatizo kubwa, ni mzigo kwa Jeshi la Magereza, kwa mafungulio ya leo wako 874 ambao walishatumikia adhabu zao wanasubiri taratibu za usafiri kurudi nchini kwao," alisema.

"Karibu nusu ya gereza ni wao na kama mnavyojua hawafanyi kazi yoyote hawazalishi, kwa hiyo tuna wajibu wa kuwatafutia chakula, ni binadamu. Kuna suala la kuugua, inatubidi tuwatafutie chakula, lakini hata wawapo kwenye magereza ya selo kuna suala la umeme ambao tunabeba sisi mzigo" alibainisha. Pia alisema, matumizi yote wanayotumia wakiwa gerezani kwa kipindi cha miaka miwili yanagharimu zaidi ya shilingi bilioni tatu.

Kwa mujibu wa CGP, fedha hizo kama zingeingizwa katika matumizi mengineyo, zingeweza kuboresha miundombinu ya magereza.

"Fedha hizi ni nyingi sana ambazo zingeweza zikaboresha maeneo mengine ya utoaji huduma kwa wafungwa walioko kwa mujibu wa sheria. Sasa hii bilioni tatu kwa miaka miwili ni kwa Gereza la Maweni pekee, lakini wapo kwenye Magereza mengine nchini ambako wanahitaji kusafirishwa" alisema.

Pia alisema, mbali na gharama wahamiaji hao wamekuwa na usumbufu mkubwa kwa viongozi wa gereza, kwa kuwa kuna wakati wanagoma kula hivyo Magereza hawawezi kuwaacha wagome.

"Lakini inakuwa kitu cha muda mfupi, wanaweza wakagoma leo ukatatua baada ya wiki mbili, wakarudia tena kwenye mgomo wao, lakini njia sahihi ya kuondokana na kero hizi ni kuwasafirisha kurudi nchini kwao" alisema.

Nyamka alisema, wahamiaji kutoka Ethiopia ndio wengi kwenye magereza nchini kuliko nchi nyingine zinazotuzunguuka.

"Kama mamlaka husika hazijakaa zikatambua tatizo hawawezi wakapata ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hili, itakuwa ni kila siku tutaendelea kukabiliana nalo," alisisitiza Nyamka.



Mkuu wa Jeshi la Magereza nchini (CGP), Ramadhani Nyamka (wa pili kushoto), akipata maelezo kuhusu mradi wa kiwanda cha kuponda kokoto kutoka kwa Mkuu wa Gereza kuu la Maweni, Mkoa wa Tanga, Revocatus Kessy, alipotembelea na kukagua miradi ya gereza hilo, juzi. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Afungwa jela miaka 22 kwa kukutwa na nyara

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara imemhukumu kutumikia kifungo cha miaka 22 gerezani, Mkazi wa Kijiji cha Sangaiwe, Sylvester Irusu (51), baada ya kutiwa hatiani kutokana na kukutwa na nyara za serikali.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Victor Kimario.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Kimario alisema amempa mshitakiwa adhabu hiyo baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili na kujiridhisha kwamba alitenda kosa hilo kwa makusudi.

Hakimu Kimario alisema, mshtakiwa alikamatwa na askari wa wanyamapori Septemba 26, mwaka jana, katika Kijiji cha Sangaiwe kilichoko wilaya ya Babati.

Alisema, Irusu pia alikutwa na nyama ya pundamilia, mali ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Buringe.

Hakimu Kimario alisema, mshtakiwa huyo alikamatwa, baada ya kutolewa kwa taarifa kwa askari wa wanyamapori na walifanya msako katika kijiji hicho usiku na wakati wakiendelea, walisikia watu wakikata vitu, ndipo waliona mtu anawamulika kwa tochi (kurunzi) na kwa bahati nzuri Irusu alianguka chini wakati wa purukushani za kumkamata, huku wenzake watatu wakikimbia.

Alisema mshtakiwa alikutwa na mikia mitano, vichwa vitano na miguu 20, pundamilia mmoja ana thamani ya zaidi ya Sh.milioni 13.9

Hakimu alivitaja vielelezo vingine alivyokutukwa navyo ni pikipiki moja, kisu kimoja, baiskeli mbili, shoka na panga.

Kimario alisema Irusu ametiwa hatiani baada ya kukiuka kifungu cha 86 (1) na (2) (b) vya Sheria ya Wanyamapori, Namba 5 ya Mwaka 2009, ikisomwa pamoja na Sheria ya Uhujumu Uchumi Aya ya 14, kifungu cha 57 na 60 cha Sheria ya Uhujumu Uchumi.

Vilevile alielekeza vielelezo vyote alivyokutwa navyo mshtakiwa vitaifishwe na kuwa mali ya serikali ili viuzwe na fedha iingie Mfuko Mkuu wa Hazina.

Kabla ya kutolewa hukumu hiyo mwendesha mashtaka wa serikali, Grace Mgaya, aliiambia mahakama kuwa mshtakiwa ana rekodi ya kukutwa na nyara za serikali.

Mgaya alidai kuwa mwaka jana mshtakiwa huyo, pia alikuwa na kesi Namba 8 ya Uhujumu Uchumi ya Mwaka 2021, ambapo alihukumiwa kifungo cha miaka 30 jela.

Kutokana na rekodi ya matukio ya uhalifu ya mshtakiwa huyo, Mgaya aliiomba mahakama hiyo kumpa adhabu kali ili iwe fundisho kwa jamii.

Mshtakiwa alipopewa nafasi ya kujitetea, aliiomba mahakama kumpunguzia adhabu kwa kuwa ana watoto saba na watoto wanne kati yao, wanasoma shule na anaishi na mama yake mzazi ambaye anamtegemea.

## Makandarasi wazawa wapewa miradi bil. 3.5/-

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

MKOA wa Manyara umeingia mkataba na makandarasi wazawa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya ujenzi wa madaraja na maeneo korofi, yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 3.5

Jana, Mkuu wa Mkoa, Makongoro Nyerere, alisema makandarasi hao wametia sahihi mikataba 20 na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA).

"Mikataba hii inahusu Wilaya za Kiteto, Hanang' na Babati. Mikataba hii ni kwa ajili ya ujenzi wa madaraja, matengenezo kwa kiwango cha changarawe na matengenezo ya sehemu korofi na yale ya muda maalum," alisema.

Alisema TARURA, imepanga kutekeleza mikataba 70 yenye thamani ya Sh. bilioni 20.551 kwa mwaka wa fedha 2022/23 na mikataba 66 sawa na asilimia 82 ya mikataba yote yenye jumla ya Sh. bilioni 16.570.

Alisema, wasimamizi wa miradi katika wilaya na wafatiliaji katika ngazi ya mkoa wajielekeze kufanya kazi kwa uadilifu na weledi ili kazi iwe katika ubora unaotakiwa.

Mkuu wa mkoa alionya tabia ya baadhi ya wakandarasi kufanya kazi chini ya kiwango na wakati mwingine kukimbia maeneo ya mradi baada ya kusaini mikataba au mara nyingine kuwa na visingizio mbalimbali kama vile ukame au mvua kubwa.

"Nitaongea na wakuu wa wilaya waweze kufika mara kwa mara kuwakagua kuona kama mnatekeleza kazi zenu kama matakwa ya mkataba unavyoelekeza," alisema.

Kadhalika, alisema hawatamvumilia mkandarasi atakayefanya kazi chini ya kiwango laa sivyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa pale atakapobainika kufanya kinyume na vigezo na masharti ya mkataba.

Kaimu Meneja wa TARURA Mkoa wa Manyara, Salim Bwaya, alisema walioshinda zabuni hizo ni makandarasi wazawa.

Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara, George Kulwa, alisema makandarasi watekeleze kwa mujibu wa mkataba ili thamani ya fedha iweze kuonekana.

Mwakilishi wa makandarasi walioshinda zabuni hizo kutoka, Gwema Civil Engineering and Building Co Ltd, Kilawila Mboya, aliishukru serikali kwa kuwapa zabuni hizo huku akisema anaamini kila mtu ana hamu ya kwenda kufanya kazi na atamaliza kwa muda uliopangwa.



## Zana za bil. 3.9/- kuongeza kasi ya umwagiliaji JKT

**Na Renatha Msungu,** CHAMWINO

WIZARA ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, imetoa mitambo na zana za kilimo zenye thamani ya Sh. bilioni 3.9 ili kuongeza uzalishaji wa chakula hapa nchini na kuimarisha usalama wa chakula.

Akizungumza jana na waandishi wa habari wilayani hapa, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Innocent Bashungwa, alisema zana hizo ni matrekta ambayo yametoka Italia na kila mmoja lina uwezo wa kulima eka 500 kwa siku.

Waziri Bashungwa, alisema lengo la kufanya hivyo ni kutaka kufanya uzalishaji wenye tija ili kuipunguzia serikali mzigo wa kusaidia chakula katika majeshi.

"Tunaishukuru sana serikali kwa kutoa fedha hizo pia, JKT (Jeshi la Kujenga Taifa) itumie wataalam wa kilimo katika kuhakikisha wanafanya kilimo chenye tija, haya matrekta yana uwezo mkubwa wa kufanya kazi yana mashine za kupandia pamoja na za kuvunia,"alisema Bashungwa.

Pia, alitaka wataalam kutoka Italia waliokuja kwa ajili ya kutoa mafunzo ya zana hizo wafundishe vijana wa hapa nchini ili kubakia na utaalam huo.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Dk. Stergomena Tax, alisema kuna upungufu wa utekelezaji wa miundombinu mbalimbali hususani umwagiliaji wa Chita na Mgeta mkoani Morogoro.

Kutokana na hilo alisema zinahitajika sh Bilioni 10 kwa ajili ya kukamilisha utekelezaji wa mradi huo.

"Kunahitajika fedha kwa ajili ya kutekeleza miundombinu ya Miradi mbalimbali ikiwemo kilimo cha umwagiliaji," alisema Tax.

Awali, Mwenyekiti wa Kilimo Mkakati Mifugo na Uvuvi, Brigedia Jenerali Hassan Mabena, alisema wamejipanga kuhakikisha wanafanya kilimo chenye tija ili kuhakikisha jeshi hilo linajitosheleza kwa chakula.

Kutokana na hilo, alishukuru serikali kutokana na dhana hizo ambazo wanaamini watatekeleza miradi ya kilimo kwa weledi.

Naye Mkuu wa Majeshi Ulinzi, Jenerali Jacob Mkunda, alisema JKT inapaswa kubuni na kuanzisha viwanda ili kuongeza kipato ndani ya jeshi hilo.

# TANESCO yatamba maboresho kuongeza huduma kwa wateja

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoani Dodoma, limetaja maboresho mbalimbali yaliyofanyika kwa lengo la kusogeza huduma kwa wateja wake.

Akizungumza jana kwenye kilele cha Wiki ya Huduma kwa Wateja, Meneja wa TANESCO Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Donasiano Shamba, alisema shirika hilo limekuwa likitekeleza mpango mkakati wa miezi 18 wenye vipaumbele saba ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

Alisema, kuanzia Januari hadi Septemba mwaka huu, kupitia mfumo wa kidigitali wa kuomba kuunganishiwa umeme bila kumlazimu mteja kwenda ofisi (Nikonekt), shirika hilo limepokea maombi ya zaidi ya wateja 19,000 na tayari wananchi 9,000 wameunganishiwa umeme.

"Maboresho katika dawati la barua ambapo wateja wanapiga simu kwenye kituo cha miito ya simu Dar es salaam, na wanapata huduma,"alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, alipongeza shirika hilo kuendelea kutoa huduma bora kwa Watanzania na kwamba maboresho hayo yatakuwa na tija kwa shirika ili kutoa gawio kubwa kwa serikali.

"Niwapongeze kwa kuhitimisha wiki ya huduma kwa mteja, utoaji wa huduma ukiimarishwa hasa kwenye shirika hili muhimu, kutaleta tija kwa jamii, nawapongeza kwa kupiga hatua sana kwenye utendaji kazi wenu," alisema.

Awali, mwenyekiti wa wafanyakazi wa shirika hilo kupitia Chama cha Wafanyakazi (TUICO), Ramadhan Butallah, alisema wamejipanga kuhakikisha wateja wanapata huduma bora.

Alisema wateja wanapewa huduma kulingana na mwongozo wa mkataba wa huduma kwa mteja kwa kuhamasisha wafanyakazi kuwahudumia vyema wananchi.

Naye Mhandisi wa Miradi na Mitambo kutoka kampuni ya Kilimo Pyxus, Muhoja Manane, alisema TANESCO imepiga hatua katika kuwahudumia wateja ikilinganishwa na kipindi cha nyuma.



Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Jacob Mkunda (wa tatu kushoto), akipiga makofi baada ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Innocent Bashungwa (wa tatu kulia) kukata utepe kuzindua zana za kilimo zenye thamani ya Sh. Bilioni 3.9 zilizotolewa na wizara hiyo kwa JKT, Chamwino, mkoani Dodoma jana. Katikati ni Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stargomena Tax na (wapili kulia) ni Mkuu wa JKT, Meja Jenerali Rajabu Mabele. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Mbinu kumaliza ombaomba wenye ulemavu yatajwa

**Na Ibrahim Joseph** ,DODOMA

IMEELEZWA kuwa watu wenye ulemavu nchini wakiwezeshwa vifaa saidizi wataondokana na maisha ya kuwa ombaomba kwenye jamii.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) Mkoa wa Dodoma, Omari Lubuva, aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye hafla ya kukabidhiwa msaada wa vifaa saidizi kwa watu wenye ulemavu vilivyotolewa na ASA Microfinance Tanzania Limited.

Lubuva alisema, kundi hilo likiwezeshwa vifaa saidizi vitawasaidia kuondokana na tatizo la kuomba misaada kwa ndugu na jamii inayowazunguka.

Alibanisha kuwa vifaa hivyo vinawasaidia watu hao wenye ulemavu kuwa na uwezo wa kujitegemea kiuchumi kwa kufanyakazi maeneo mbalimbali .

Kadhalika, alisema baadhi ya watu wa kundi hilo wamekuwa wakionekana mtaani kuombaomba kutokana na kushindwa kuzalisha mali lakini kama wakiwezeshwa kujitegemea hali hiyo itaondoka kwao.

Aliishukuru serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu,Kazi,Vijana Ajira na wenye Ulemavu kwa kuwaunganisha na wadau hao ambao wamewasaidia vifaa hivyo saidizi.

Alisema, kila mwaka taasisi hiyo imekuwa ikiwapatia baadhi ya watu wenye ulemavu wa mkoa huo na mingine na kupunguza utegemezi kwenye jamii kwa kuwa na uwezo wa kufanya kazi. Mmoja wa wanufaika, Mkazi wa Matumbulu, Mary Masambuli, alisema tangu azaliwe hajawahi kupata kifaa saidizi na amekuwa akihangaika kwa kutembelea magoti .

Masambuli alisema, atakitumia kifaa hicho alichokabidhiwa msaada jana kwa kufanya biashara mitaani tofauti na kipindi cha nyuma ambacho alikuwa akiombaomba fedha kwa watu mitaani.

Mkurungenzi Msaidizi wa ASA, Abu Sayed, alisema wamekabidhi vitu mbalimbali kwa ajili ya watu wenye ulemavu vyenye thamani ya Sh. milioni 13.5.

Alisema, taasisi hiyo pamoja na kutoa misaada ya vifaa hivyo pia wamekuwa wakisaidia jamii kwa kutoa mikopo yenye masharti nafuu hasa akinamama wajasiliamali na mamalishe ili kujikwamua kiuchumi ambapo wametenga sh. bilioni 140 kwa ajili hiyo.

Aliongeza kuwa hadi Septemba, mwaka huu, ASA ilikuwa imeshatoa ajira 1,400 kwa wananchi na kati ya hao wanawake ni asilimia 70 katika Mikoa tisa ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye ulemavu, Prof. Jamal Katundu, alishukuru taasisi hiyo kwa msaada huo na kuahidi kuwafikishia walengwa huku akiomba wadau wengine kujitokeza kwa kuunga mkono juhudi za serikali katika kuihudumia jamii maeneo mbalimbali nchini.





# Makamu wa Rais ataka chombo kusimamia maridhiano Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman amesema kuna haja ya kuundwa kwa chombo kitakachokuwa na wajibu wa kusimamia utekelezaji wa mapendekezo kuhusu namna ya kuyafikia maridhiano ya dhati ya kisiasa Zanzibar.

Aliyasema hayo jana wakati akifunga mkutano wa siku tatu wa majadiliano mahsusi ya Zanzibar yanahusu vyama vingi vya siasa katika Hoteli ya Golden Tulip mjini Zanzibar.

Alisema, kuundwa kwa chombo hicho kutasaidia kudumu kwa maridhiano ya kisiasa kabla, wakati na baada ya uchaguzi mkuu.

Othman, aliunga mkono kauli ya Rais wa Zanzibar, Dk. Mwinyi kuwa na dhamira ya dhati katika kufikia kwenye maridhiano ya kweli ambayo dhamira hiyo inapimwa na matendo ya kila mmoja.

"Hayo yote tuliyoyaazimia yanapaswa kuwekewa utaratibu wa namna bora ya kuyatekeleza. Kila mzanzibar anastahiki kufahamu kipi kitafanywa lini na nani. Ni kwa namna hii tu ndiyo tutaondosha kulaumiana na kutiliana shaka," alisema huku akinukuu msemo wa wahenga 'matendo ni fasaha zaidi kuliko maneno'.

Alisema ili kujenga Zanzibar moja, ni lazima kila mmoja kuwa mkweli katika matendo yake.

Alisema, mfano aliouacha marehemu Maalim Seif Sharif Hamad wa kusimamia amani, umoja na mshikamano ni somo tosha kwa sababu alitekeleza hayo hata pale alipokuwa akipingwa na kutishiwa na wafuasi wake mwenyewe.

"Maalim Seif aliamini kuwa hakuna mbadala wa amani na mshikamano, njia pekee ni nchi ifike pahala isimamishe utawala wa haki na utawala uliobora," alisema.

Alisema, dhamira ya kujenga umoja, amani na mshikamano isitikiswe wala kuyumbishwa na kero za ndani au nje ya mirengo ya kiitikadi na kuendelea kuvumiliana.

Othman alisema, ili kujenga nchi ni lazima kujenga misingi inayoakisi maendeleo ya dunia.

"Tunapenda sana wakati mwingine kulalamika mambo yetu ya Zanzibar kana kwamba ni ugonjwa tumeletewa na mtu. Tunayo mifano mizuri ya kuiga katika mageuzi ya kidemokrasia na utawala bora," alisema.

Alisisitiza kutotoneshana vidonda kwa mambo yaliyotokea miaka ya nyuma Zanzibar kuhusu vuguvugu la kisiasa na badala yake vidonda hivyo vipatiwe dawa na kubaki kuwa makovu.

Alikiri wananchi wengi ambao waathirika kila wakati wa uchaguzi wamepoteza imani ya siasa na mfumo wa kuendesha uchaguzi.

"Hili si la kupuuza hata kidogo, wao siyo tu wamekuwa wakitoneshwa vidonda lakini wamekuwa wakipoteza viungo kila uchaguzi. Ni wakati wa kuwafanya kuwa na amani, tukawaaminisha kwa vitendo kuwa yaliyopita si ndwele, sasa tugange yajayo," alisema.

Aliongeza kuwa mageuzi na kurejea katika misingi bora ya kuendesha nchi yatampa amani kila mtu.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais, Hamza Hassan Juma alisema mkutano huo wa majadiliano uliowahusisha wanasiasa, viongozi wa dini na asasi za kiraia, ni wa mafanikio katika kuijenga Zanzibar mpya yenye umoja, upendo, amani na mshikamano bila ya kujali itikadi za kisiasa.

"Pamoja na kuwapo kwa vijembe (kuelezana ukweli) lakini maslahi makubwa yamepatikana na hoja zote zitafanyiwa ufupisho kisha kuwasilishwa serikalini huku akiwaomba wanasiasa kwenda kuwaeleza ukweli wananchi kama ambavyo wamejadiliana," alisema.

Akitoa shukrani kwa niaba ya washiriki wa mkutano huo, Balozi Amina Salum Ali, alisema kumalizika kwa mkutano huo ni historia kubwa ambayo itajenga Zanzibar, hivyo wote kuwa wamoja na kuzidi kuleta uelewano mzuri zaidi na kudumisha maridhiano ya kisiasa.

## Apata mbinu kuongeza ufaulu kwa wanafunzi

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Wilaya ya Kusini kwa kushirikiana na Kamati ya Mwaka Kogwa umeitaka jamii kutoa misaada kwa wanafunzi walio katika matayarisho ya mitihani ili azma ya kuimarisha sekta ya elimu na kuongeza ufaulu katika wilaya hiyo ifikiwe.

Mkuu wa Wilaya ya Kusini, Rajab Yussuf Mkasaba alitoa rai hiyo jana alipopokea msaada wa vyakula kwa ajili ya wanafunzi wanaojiandaa kwa Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne katika Shule za Sekondari Manduchi na Kusini, msaada uliotolewa na Kamati ya Mwaka Kogwa ya Makunduchi.

Alisema hatua hiyo ni miongoni mwa mikakati itakayosaidia kwa kiasi kikubwa kufikia lengo la serikali katika kutokomeza ufaulu mbaya wa matokeo ya kidato cha nne katika wilaya hiyo na mkoa wao kwa ujumla.

Mkasaba alisema Kamati ya Mwaka Kogwa pia imeonyesha mfano mzuri kwa kugeuza matatizo kuwa fursa baada ya kuyaona matokeo ya mitihani hayaridhishi katika wilaya hiyo na kutoa msaada huo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mwaka Kogwa, Mwita Masemo alisema kamati yake imeamua kutoa msaada kwa jamii kwa kutambua jamii ina haki ya kurejeshewa kile kilichopatikana katika sherehe hizo za kijadi zinazofanyika kila mwaka kijijini Makunduchi.

Mwenyekiti huyo aliitaka jamii kuondoa dhana potofu kwamba kamati hiyo imekuwa ikipata fedha na kuzitumia pasipo kuifikiria jamii.



Baadhi ya wanafunzi kutoka shule tofauti Zanzibar, wakiwa katika kongamano la siku ya mtoto wa kike, lililoandaliwa na chama cha waandishi wa habari wanawake Tanzania (TAMWA), jijini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mahakama yabaini janga kwa watoto wa kike Zenj

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Mahakama ya Watoto Zanzibar, Zuwena Abdulkadir amesema, mahakama hiyo imefanya kazi kubwa tangu kuanzishwa kwake, hasa kusikiliza kesi za udhalilishaji wa kijinsia.

Amesema, katika uendeshaji wa mashauri hayo, wamebaini kuwapo kwa tatizo la watoto wa kike wanaoingiwa kinyume cha maumbile yao.

Aliyasema hayo jana mjini Zanzibar, alipozungumza katika kongamano la kuadhimisha siku ya mtoto wa kike lililoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar.

Alisema, wamefanya uchunguzi na kubaini kuwapo tatizo la kuingiwa kinyume cha maumbile watoto wa kike, hasa wenye umri wa chini ya miaka 17 ambao wanafanya hivyo kwa kuogopa kubeba ujauzito na kulinda bikra zao.

Aliwataka watoto wa kike kujitambua na kuijua thamani yao akionya kuwa kujihusisha kufanya mapenzi wakiwa na umri mdogo ni kuwaingiza katika matatizo ikiwamo kushindwa kuendelea na masomo yao.

Mwenyekiti huyo alisema wamejipanga kuhakikisha kesi zote za udhalilishaji wa kijinsia zinashughulikiwa kwa wakati huku akiitaka jamii kuwa tayari kutoa ushahidi.

Alisema, miongoni mwa vikwazo vikubwa katika uendeshaji wa kesi hizo ni kukosekana kwa ushahidi ambao ni muhimu katika kuwatia hatiani watuhumiwa.

Alisema, katika kesi za jinai hakuna hatia bila ya ushahidi, akifafanua kuwa kesi inayokosa ushahidi ni kesi inayopoteza uhalali wa kusikilizwa mahakamani.

Akifungua kongamano hilo, Mkurugenzi wa Idara ya Watu Wenye Ulemavu, Salma Sadatti alisema lengo la maadhimisho ya siku ya mtoto wa kike ni kuikumbusha dunia thamani ya mtoto wa kike ambaye anatakiwa kulindwa na matukio yote dhidi ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

Alisema, huu ni wakati wa kuhakikisha mtoto wa kike analindwa dhidi ya vikwazo vyote vinavyomkabili kwa ajili ya kupiga hatua kubwa za maendeleo, ikiwamo elimu.

Alipongeza juhudi zinazochukuliwa na serikali zote mbili katika kuona maendeleo ya mtoto wa kike yanafikiwa ikiwamo katika kujenga misingi mizuri ya sheria na elimu.

"Ujumbe wangu kwa watoto wa kike, wakiwamo wanafunzi, wajitambue na wawe tayari kukabiliana na vikwazo vinavyowakabili katika maisha huku wakitakiwa kujenga msimamo na kukataa udhalilishaji wa kijinsia," alisema.

Baadhi ya wadau waliohudhuria kongamano hilo, vikiwamo vyombo vya sheria, waliitaka jamii kutoa ushahidi katika kesi za vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

Mwakilishi kutoka Jeshi la Polisi Zanzibar, Egyne Emmanuel alisema wamejipanga kuhakikisha wanafanya upelelezi katika kipindi kifupi na kuzifikisha kesi hizo mbele ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kwa ajili ya kupelekwa mahakamani.

Alisema, Jeshi la Polisi lipo katika kipindi cha mageuzi ambayo ni kukamilisha na kufanya uchunguzi wa kesi zote za udhalilishaji kwa wakati kwa ajili ya kuondosha malalamiko kutoka kwa jamii.

Alisema wakati umefika sasa kuwapo elimu ya ndoa, akiwa na ufafanuzi kwamba kuvunjika kwa ndoa ni sehemu ya mizizi ya kuibuka kwa vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

Akichangia katika kongamano hilo, Ofisa Ustawi wa Jamii, Sabra Mwalimu Mgeni, aliitaka Ofisi ya Mufti kudhibiti matukio ya vyuo vya madrasa kuwa sehemu ya maficho ya ukatili wa kijinsia na udhalilishaji.

Katika kongamano hilo uliwasilishwa utafiti uliofanywa na TAMWA uliobaini kuwapo kwa wimbi la vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia unaofanywa katika ngazi za familia, ukiwahusisha baba mzazi, baba wa kambo, wajomba pamoja na walimu wa vyuo vya madrasa na waganga wa kienyeji.

Akiwasilisha utafiti huo, Zaina Abdalla Mzee alisema kwa udhalilishaji unaofanywa na baba mzazi, wamebaini baba wazazi 13 wamewafanyia udhalilishaji watoto wao kwa kuwabaka, kulawiti na kuwaingilia kinyume cha maumbile watoto wao wa kike.

Alizitaja sababu za kufanyika kwa vitendo hivyo ni kutengana kwa wazazi wawili ambapo watoto wa kike kuishi na baba zao na matokeo yake kuwafanyia ukatili huo.



**NAY**
UKURASA 16

JUMAMOSI OKTOBA 8, 2022



Muonekano wa sasa

Muonekano wa zamani

# VERA SIDIKA

YUKO WAPI ?

# ABDUL PANGAMAWE-2

## Aliajiriwa msondo na miaka17
## Pesa alizotunzwa ziliibua balaa



**Na Adam Fungamwango**

LEO tunamalizia makala iliyoanza wiki iliyopita ya mwanamuziki wa Msondo Ngoma Musica Band, Abdul Ridhiwani Pangamawe, akisimulia jinsi aliyojiunga kwa bahati tu kwenye bendi hiyo akitokea mkoani Iringa kwenda Dar es Salaam kwa kaka yake ili akasome.

Wakati taratibu za shule zikifanyika ilikuwa kama mzaha tu kaka huyo akamwambia jirani yake, Joseph Lusungu kuwa mdogo wake ni mahiri sana kwenye upigaji wa kinanda na kwa sababu wameondokewa na Waziri Ally aliyekwenda kuunda bendi ya Kilimanjaro 'Njenje', basi anaweza kuwafaa.

Kaka huyo alikuwa hana wasiwasi na mdogo wake kwa sababu baba yao mzazi mzee Pangamawe mwenyewe alikuwa mwanamuziki na kiongozi wa bendi ya Highland ya Iringa na vyombo vilikuwa vinakaa nyumbani kwao. Ridhiwani, alikuwa akijifunza kwa kujificha kwa sababau mzee hakutaka afanye hivyo kwa kuhofia kuwa hatosoma.

Haikuwa dawa kwani wakati mtoto wake anatoka Iringa alikuwa tayari anafahamu kupiga vyombo mbalimbali kama vile magitaa yote, solo, rhythm na besi, pia alikuwa mahiri kwa kinanda.

Hata hivyo, baada ya siku ya tukio, Lusungu alipomchukua na kumpeleka Amana Social Hall Club, Ilala alichokikuta huko ni kwamba aina ya kinanda kile kilichokuwa kwao na hicho ni tofauti.

Hiyo ilimfanya ashindwe kufanya kitu chochote. Lusungu alikifungua na kumwambia apige, lakini hakuweza. Ilifika wakati akakasirika na kwenda ukumbini kuendelea na mazoezi na wenzake, huku akiwaambia wenzake tukio hilo.

Akasema kuwa alipokuwa peke yake, alianza kukikagua kinanda na kuangalia sehemu ambazo anaweza kukipiga, na kwa sababu hakuwa na presha ya kusimamiwa na mtu, taratibu kaanza kupiga kwa ufasaha.

"Kuna wimbo wa Msondo ulitwao 'Epuka Tabia Mbaya', nilikuwa najifundisha kupiga nikiwa nyumbani Iringa, nikaanza kuupiga, kumbe kiongozi wa bendi Saidi Mabera alikuwa anakuja mazoezini, alipofika mlangoni kabla hajafika ukumbini akasikia sauti ya kinanda kinapigwa kwa ustadi akawa anajiuliza ni nani. Akaingia kwenye chumba. Mimi sikumuona, naendelea, ghafla nikasikia sauti ikisema 'enhee ongeza hapo kidogo', nikashtuka, nikamuona, akaondoka na kwenda kuwaambia wenzake 'yule dogo anaweza.'"

Pangamawe anasema, baada ya hapo walikuja wote ndani na kumkuta akipiga kwa ustadi kwani tayari alishaanza kukizoea.

"Nakwambia walishangilia kama goli limeingia kwa sababu walikuja wanamuziki wengi sana mahiri lakini wakashindwa majaribio, nikanunuliwa soda, pesa, nikaanza mazoezi ya kupiga wimbo huo na ndiyo uliokuwa wa kwanza kuupiga kwenye kumbi, kwa muda mrefu uliachwa kupigwa wimbo huo baada ya Waziri kuondoka. Nilikuwa na miaka 17, lakini viongozi wa bendi walinizidishia mwaka mmoja mbele, nikaandikwa nina miaka 18, nikaajiriwa na Jumuiya ya Wafanyakazi wa Tanzania (JUWATA) kama mwanamuziki."

Akakumbuka siku ya kwanza kupiga ilikuwa kwenye ukumbi wa Friends Corner, Manzese ambapo watu hawakuamini walipomuona mtoto mdogo akipiga kinanda kwa umahiri kama Waziri Ally.

Kwanza kabisa alitaka kukimbia baada ya kuona idadi kubwa ya mashabiki waliokuwa ukumbini na yeye kutakiwa kwenda kupiga, na kutojiamini na woga, akataka kukimbia, lakini akarudishwa ndani na walinzi wa mlangoni

"Nilitunzwa balaa, pesa zote nikakusanyiwa na wanamuziki wa Msondo wakaniwekea kwenye mfuko wa karatasi, nilirudi usiku wa manane nyumbani na fuko langu, nikalala kwenye kochi, asubuhi nikaamka nikazimwaga kwenye meza na kuanza kuhesabu. Zilikuwa nyingi sana na tangu nizaliwe nilikuwa sijawahi kuona pesa nyingi kama hizo, na eti zilikuwa zangu," anasema.

Akaongeza "Naanza kuhesabu tu, mama yangu mzazi akaingia. Akashtuka kuona nahesabu kiasi kile cha pesa, akadhani kuwa mimi nimeanza kuwa mwizi. Akamwita kaka yetu mkubwa ambaye tulikuwa tunakaa kwake, akamwambia 'hebu mwangalie mdogo wako ameanza kuwa mwizi.Kaka akacheka, akamwambia, mwanao ametoka kupiga muziki Msondo. Mama alishtuka na kushangaa,"

Mama yake akauliza kwa mshangao "Yaani Abdul ametoka kupiga muziki NUTA?',

Akasema huo ndiyo ulikuwa mwanzo na kisa cha kujiunga bendi ya Juwata Jazz akapachikwa jina la 'Toto', na amedumu na bendi hadi leo hii.

# UDAKU TU



## Aliyopitia Masanja yanatosha

MAJIBU ya msanii wa vichekesho na kiongozi wa Kanisa la Feal Free, Masanja Mkandamizaji kuwa hawezi kumuacha mke wake Monica, yameibua mjadala mkali kuhusu msimamo huo.

Hivi karibuni kulikuwa na hali ya sitofahamu baada ya katibu wa kanisa hilo kujinyonga kwa kile kinachodaiwa kushindwa kuhimili baada ya kukatizwa kwa uhusiano wao wa kimapenzi na Monica.

Hata hivyo, Masanja alionekana katika video fupi akiwa katika kanisa lake na kueleza kwamba kamwe hawezi kumwacha mke wake kwa sababu ya kifo cha katibu wao na kuahidi kuishi naye hadi kifo kiwatenganishe.

Hata hivyo, baadhi ya watu walikuwa na maoni tofauti kutokana na msimamo wa Masanja.

Idadi kubwa walimpongeza kwa msimamo huo na kueleza kama mtumishi wa Mungu amefanya uamuzi wa busara na wenye kutoa fundisho kwa jamiii.

Walisema kipindi walichopitia ni kigumu na inatosha kuthibitisha ana imani thabiti hasa kwa kuzingatia kashfa hiyo ilikuwa kama mtihani wa uvumilivu kwa masanja na mkewe.

Baadhia ya waliotoa maoni ni Winnie Boss, ameandika "Sawa pastor upo umewakomesha sana na kauli yako ya hata ningemkuta na nani usingemuacha,"

Naye eneamahenge_praiseminister, ameandika "Kwakweli unaweza dhani ni mtu wangu wa karibu anayefanya hivi, kumbe ni shetani ndani yake anawinda ndoa. Anawinda huduma, anasukuma. OLe wako wewe unaekubali kutumiwa na shetani kumpiga aliyekubaliwa na bwana. Utapigwa mwenyewe kwa jina la Yesu,"

## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**@ireneuwoya8**
Tukisema mwanaume hakimbii matatizo ...hatuna maana ndio uyakimbii

**@dogojanjatz**
Yale mahusiano mliyosema yatanitoa roho, ndio haya sasa yananitoa mashavu





**@bekaflavourdaily**
Kila mtu ana aina ya maisha anayoishi na mpenz wake

**@iam_mziwanda**
Nipo, nilikuwepo na nitakuwepo





**@shamsaford**
Adui akipambana na wewe akiona amekushindwa atageuka kuwa rafiki yako

BASI SAWA

## D Voice kuimba jinsia ya kike sio shida kwake



MSANII wa muziki wa Singeli, D Voice, amesema kuimba kwa kusimama katika jinsia ya kike ni aina ya sanaa ambayo wengi hawawezi kufanya.

Amesema kuvaa uhusika wa mwanamke ni sanaa iliyokuwa ikifanywa na wanamuziki wengi wa zamani na kwamba ujumbe wake ulikuwa ukifika haraka na unaishi muda mrefu.

"Wacha waniseme tofauti, lakini kwangu naona ni moja ya sanaa inayokubalika na kwamba  kinawagusa watu katika wakati huo huo," amesema D Voice.

## Shepu mpya ya Vera hii hapa



MPAMBAJI wa video za muziki na mjasiriamali, Vera Sindika kutoka Kenya, amepunguza muonekano wake wa makalio kwa kile alichodai sababu ya kiafya.

Akitumia Ukurasa wake wa Instagram, Sidika amesema kwa sasa ni kama amezaliwa upya baada ya kufanikiwa kuweka mwonekano mpya.

"Kuzaliwa upya, hii imekuwa awamu ngumu zaidi maishani mwangu kwa sababu ya hatari na matatizo ya kiafya , ilinibidi kufanyiwa upasuaji. Nimekubali na nimejifunza kujipenda bila kujali".ameandika.



## NAY WA MITEGO AKUMBANA MITIHANI

RAPA mwenye utata mwingi, Nay Wa Mitego, amesema mama yake mzazi, watoto wake na familia yake kwa ujumla inatamani aache muziki.

Amesema, familia yake inafikiria njia hiyo ni salama zaidi kutokana na changamoto anazopitia.

Akizungumza kupitia Planet Bongo ya East Africa Radio, amesema, ni suala gumu lakini anaweza kutafakari baada ya kila mtu katika familia yake kumsihi kuachana na muziki kwa sasa.





## Ushauri wa Tausi uzingatiwe

MSANII wa filamu Tausi Mdegela, amesema kulea mtoto kwa upande mmoja ni lazima kupambana na kujitoa kwa kila kitu.

Tausi kupitia ukurasa wake wa Instagram, amesema kila mwanamke anayelea mtoto peke yake ni lazima kumpambania mwanawe hata kama mzazi mwenza hatoi huduma.

"Single mother tujifunze hii sana hata kama hatoi huduma baki na mtoto wako mpambanie. Mimi Pipina wangu nampambania mwenyewe na maisha yanaendelea, Mungu endelea kunipa nguvu kwako kila kitu kinawezekana". ameandika

Tausi Mdegela amepata mtoto wake wa kwanza wa kike mwanzoni mwa mwaka 2020 na mpenzi wake Chriss.

## STAILI 5 ZA BOLINGO ZILIZOTIKISA BONGO

**Na Adam Fungamwango**

Ni ukweli usiopingika kwenye miaka ya '60, '70,'80 hadi '90, muziki wa Congo DR ulikuwa unatawala sana nchini Tanzania kwenye masikio ya mashabiki wa muziki.

Hata hivyo, mwanzoni mwa miaka ya '90, wakati huo televisheni zinaanza kuingia nchini, muziki wa Congo DR, Watanzania wengi walianza kuona hata baadhi ya mitindo ya uchezaji ikichezwa na wanamuziki wenyewe pamoja wacheza shoo.

Hii ilisababisha si tu kuibuka kwa madansa wengi nchini waliofanya vizuri, lakini pia Wabongo wengi kuiga na kucheza staili mbalimbali za mitindo ya muziki iliyokuwa ikipigwa na wanamuziki kutoka Congo DR.

Kwenye matamasha, harusi, au shughuli mbalimbali za kijamii, vijana, wake kwa waume, na hata wazee walikuwa wakijaribu kuiga staili hizo za uchezaji, wakati mwingine wakizicheza kwa ustadi wa hali ya juu hadi kutunzwa pesa.

Leo tunawakumbusha staili za uchezaji zilizovuma zaidi na kupendwa sana na mashabiki wa muziki nchini Tanzania, kiasi cha kuchezwa kwenye hafla mbalimbali za kijamii na hata kitaifa.

**Nzawisa-Bozi Boziana**

Staili hii ya 'Nzawisa' ilipendwa sana hasa na akinadada wakati huo. Ilitokana na nyimbo za Bozi Boziana ambazo ndizo zilikuwa na 'rap' hiyo.  Ilivutia sana hasa kwenye wimbo maarufu wakati huo wa 'Tembe na Tembe'. Ni aina fulani ya uchezaji ambao ni wa kukata viuno, huku mchezaji akipandisha kidogo mguu mmoja na kuushusha, halafu mwingine pia. Huvutia sana hasa wachezaji wanapokuwa wawili au watatu, kwa sababu ulikuwa ukichezwa na waimbaji wa kike kina Scolla Miel na Mukangi Deese.

**Pesa Posa-Kanda Bongoman**

Pamoja na kwamba bendi nyingi za Congo DR zilikuwa 'rap' hii ya 'Pesa Posa', lakini pia staili ya kucheza,  wengi wanaikumbuka zaidi na kuipenda kwenye nyimbo za Kanda Bongoman.

Huyu ndiye mwanamuziki  aliyepiga shoo kwa kiingilio ghali zaidi nchini Tanzania miaka ya '90, aliingiza watu kwa shilingi laki moja na ukumbi ukajaa, wengine wakashindwa kuingia.

Staili yake ya 'Pesa Posa' inayochengua zaidi kwenye nyimbo za 'Inde Monie', na 'Isambe', inachezwa kwa mikono kuifanya kama unapeta mchele kwenye ungo, huku mwili na hasa kiungo kikitikisika. Ilitingisha sana staili hii kipindi hicho.

**Tshamukwale-Defao**

Ingawa bendi nyingi zilipiga mtindo wa 'tshamukwale yako pesa mbongo', lakini ulitangazwa sana na mwanamuziki Defao. Uchezaji wake unawapendeza sana wanaume, hasa wakiwa wengi wamepangana msitari, bega kwa bega.

Wananesa kwenda kulia na kushoto, wanainama chini wakipiga mikono mara mbili, halafu wa kulia unakwenda nyuma ya kichwa kwenye shingo, kama mtu anayetaka kukata kichwa chake.

**Kiwanzenza-King Kester Eameneya**

Pamoja na kwamba hana jina kubwa sana nchini, lakini mtindo wake wa 'Kiwanzenza' ulikuwa maarufu sana Afrika Mashariki na Kati. Emeneya aliyefariki 2014, ndiye mwasisi wa mtindo huo uliopendwa sana na vijana, ambao staili yake ni ya kupiga mguu chini na kuunyanyua kwa zamu, pia mikono nayo inakuwa kama unapiga nyundo na kunyanyua.

**Ndombolo ya Solo-JB Mpiana**

Ni mtindo uliovuma na kupendwa sana na kizazi cha vijana katikati na mwishoni mwa miaka ya '90.



Uliasisiwa na JB Mpiana alipotoa albamu yake ya 'Feux de L'amour ambayo ilikuwa na wimbo wenye jina hilo la 'Ndombolo ya Solo' uliovuma na kupendwa sana. Uchezaji wake unawapendeza zaidi wanaume ambao hautofautiani na mwendo, utembeaji, au uringaji 'nyani dume'.

FILAMU

## Shangazi Joy: Baniani mbaya, kiatu chake dawa

**Na Adam Fungamwango**

Leo tuiangalie filamu iitwayo 'Shangazi Joy' ambayo itakushangaza, kukuhuzunisha, kukufurahisha na kukupa mafunzo kwa wakati mmoja.

Imechezwa na Mahmoud Athumani, kama baba, Aisha Nyange aliyecheza kama mama, Ziberi Bakari yeye ni John, Abdulkarim Mwautanga kama Kenedy, Jasmine Mohamed amecheza kama Kendy, na Mwajabu Majema, huyu alicheza kama Shangazi Joy.

Inaanza kwa kuonyesha Shangazi Joy akishuka kwenye bodaboda. Alikuwa ametoka kijijini kwenda jijini Dar es Salaam kwa kaka yake.

Ghafla, anavamiwa na vijana wawili ambao wanampora kitambaa cheusi ambacho walimuona nacho akikifunga fundo kama kina pesa.

Shangazi huyo ambaye hakuwa mkubwa kiumri ni wastani tu wa miaka 23 mpaka 25 aliamua kuwafukuza, hasa yule mwenye kitambaa mpaka akampata, akamuangusha chini na kukichukua.

Anafika kwa kaka yake na kupokelewa vyema pamoja na wifi yake. Hata hivyo wapwa zake, John, Kennedy na Kendy hawakumpokea vyema. Alionekana ni mshamba ametoka kijijini, hivyo ni mtu dhalili. Hawakumpa kabisa ushirikiano. Walionekana kumyanyapaa na kumpa maneno ya kejeli kiasi cha kumfanya kuwa mpweke. Hata hivyo baba na mama wa watoto hao hawakuipenda hali ile.

Kumbe mmoja wa vijana aliyempora kitambaa cheusi siku ile ni John. Shangazi alimkumbuka alipofika kwa kaka yake, lakini 'akapotezea'. Mwenyewe akadhani amemsahau. John alishajua kuwa ndani ya kitambaa mle hakuna pesa ila ni almasi. Hivyo akaenda kwanza kwa sonara na kuongea naye kuwa ana mzigo. Akataka kumuibia shangazi yake, lakini ilikuwa ngumu. Siku moja akabambwa na dada yake Kendy chumbani usiku. Alipomuuliza akashindwa kujitetea na kumuunganisha kwenye ile dili. Baadaye akamuunganisha na ndugu yao Kennedy. Hao wote lao sasa likawa moja kuisaka almasi ya shangazi yao wakaiuze ili wagawane pesa.

Wakati huo baba yao anapigiwa simu kudaiwa pesa na benki kutokana na mkopo aliokopa na kuuelekeza kwenye biashara ya miti ambayo haikulipa.

Kwa hiyo nyumba ilitakiwa ipigwe mnada kufikia yote hayo. Kabla yote hayajafanyika, watoto wa mzee huyo bado walikuwa wakihangaikia almasi ya shangazi Joy ambayo alikuwa akiificha kama mboni ya macho yake.



Ukapikwa wali na kuwekwa madawa ya kulevya ili ale alewe na wampekue mwili mzima wakaweze kuipata, kwani walitafuta chumbani anakolala na Kendy lakini hawakuiona.

Kabla hajala chakula, baba yao anafika. Akamwambia dada yake Joy akapakue kingine. Akala yeye, akalewa na kulala nusu mfu. Alipozinduka kesho yake akauliza, lakini kuna kitu akakigundua.

Wakati huo Joy na kaka yake walikuwa wametoka. Walirudi na gari jipya, kila mtu alishangaa. Gari lilinunuliwa na Joy. Alikuwa ameshaiuza ile almasi ambayo ilikuwa inatafutwa na wapwa zake. Baba aliiweka familia yake chini na kueleza uchafu wote walioufanya watoto wake. Akamwambia mkewe kuwa dada yake huyo ndiye aliyewaokoa kwani asubuhi alimuamsha wakaenda mbali, ndipo alipomueleza ana almasi wakaenda mjini kuuza na kulipa deni lote benki na pesa imebaki nyingi.

Watoto wakabaki na aibu, wakaambiwa wamuombe shangazi yao msamaha.

BARIZI LA PWANI

# SHAKILA SAID
# Mwimbaji aliyebarikiwa Sauti



SHAKILA Said, ni miongoni mwa wasanii nguli katika miondoko ya muziki wa taarabu Afrika Mashariki na Kati.

Wakati wa uhai wake, aliweza kuonyesha umahiri wake wa uimbaji wa taarabu katika bendi tofauti alizowahi kuzitumikia.

Shakila alifariki ghafla 2016 baada ya kuanguka alipokuwa akifagia nyakati za jioni.

Msanii huyu alikuwa na weledi wa kujuwa jinsi ya upangiliaji wa sauti kupitia maneno ya lugha adhimu ya Kiswahili katika nyimbo zake zote.

Kwa ustadi mkubwa Shakila hakuimba nyimbo za mapenzi pekee, aliweza kuimba nyimbo hata zile zinazoigusa jamii, siasa na Ukombozi.

Shakila alizaliwa Juni 14, mwaka 1947, Wilayani Pangani, mkoa wa Tanga. Jina lake alikuwa akiitwa Tatu Saidi na ndilo lililofahamika na watu wengi kabla ya kuingia katika uimbaji.

Tatu alikubali ushauri wa mumewe wa kuingia katika sanaa ya muziki wa taarabu, hapo alianza kufanya mazoezi ya kutunga na kuimba nyimbo za taarabu.

Baada ya kuonekana kuwa ana uwezo mkubwa, mumewe Khatibu alimshawishi kujiunga katika kundi la Kijamvi taarabu lililokuwepo mjini Pangani mkoani Tanga.

Hakudumu kwa kipindi kirefu na kikundi hicho akalazimika kuhamia mjini Tanga kumfuata mumewe na huko alijiunga katika kundi la Al Watan.

Hata hivyo, Tatu akiwa katika kundi hilo hakupewa nafasi ya kuimba mbele ya kadamnasi, kitendo ambacho kilimkasirisha.

Baada ya hali hiyo, Tatu na mume wake wakahamia kundi Young Novelty mwaka 1961.

Kipindi hicho sinema za kihindi zilikuwa na umaarufu, na watu walimshuhudia mwimbaji wa nyimbo za Kihindi aliyekuwa akiitwa Shakila na hivyo walimpachika jina hilo Tatu kutokana na sauti yake kufanana na msanii huyo.

**Inaendelea wiki inayokuja**



## BATA LA WIKI

**Je una kiwanja cha burudani piga -0717336368**

**Jahazi Modern Taarab**
Kundi hili ambalo liko chini ya uongozi wa mkongwe mwana muziki wa mwambao, Mzee Yusuph, lina onyesho moja tu ambalo litafanyika leo Jumamosi katika ukumbi wa Kwetu Pazuri Mbezi Mwisho Dar es Salam.

**FM Acadeemia**
Wakiongozwa na Rais wao Patcho Mwamba, Ijumaa wapo ndani ya ukumbi wa Butiama 2 Chanika, leo Jumamosi watakinukisha katika ukumbi wa Mawasiliano Park Ubungo na Jumapili wanapumzika.

**Special Band**
Chini ya Mwinjuma Muumin, Ijumaa na Jumamosi hii itaungana na Sayari Band inayoongozwa na Badi Bakule na kutoa burudani katika ukumbi wa UEFA uliopo Kongowe Kibaha mkoani Pwani.

**Tukuyu Sound**
Ijumaa wapo katika ukumbi wa Kipong jijini Arusha, leo Jumamosi watakuwa na shoo maalum jijini humo, Jumapili watamalizia wikiendi katika ukumbi wao wa nyumbani wa Mawasiliano Park Dar es Salaam.

**TOT-Band na Taarab**
Bendi ya muziki wa dansi na taarab wako katika mapumziko ya muda mfupi wakijiandaa kwenda kwenye sherehe za uzimaji wa Mwenge wa Uhuru Oktoba 14 mjini Bukoba mkoani Kagera.

**Msondo Ngoma**
Ijumaa wanatoa burudani katika ukumbi wa Gwambina Lounge Chang'ombe, Jumamosi wapo ndani ya ukumbi wa Mandela Square Lumo na Jumapili watafanya vitu vyao katika ukumbi wa Dar Safari Buza.

**Twanga Pepeta**
Kila Ijumaa wapo Mawasiliano Park Ubungo, Jumamosi ndani ya ukumbi wa Escrow Pub Kigamboni na Jumapili watafanya vitu vyao ndani ya ukumbi wa Gwambina Lounge Chang'ombe (zamani TCC Club).

**Kimokimo Band**
Bendi hii ambayo inaongozwa na mwimbaji wa siku nyingi Khadija Kimobitel, wiki hii inafanya vitu vyake katika ukumbi wa Mariote Hotel External Dar es Salaam, kwa siku mbili za Ijumaa na Jumapili.

**Town Classic Band**
Bendi mpya ambayo imekusanya wanamuziki kutoka bendi mbalimbali, bado inajichimbia kambini jijini Dar es Salaam ikiendelea kujifua ili kuibuka rasmi mwishoni mwa mwaka huu na kuanza kufanya vitu vyake.

**Waluguru Original Band**
Bendi hii yenye maskani yake mjini Morogoro, Ijumaa ipo ndani ya ukumbi wa Kambarage, Jumamosi inatoa burudani katika ukumbi wa Terminal Pub na Jumapili wanamalizia wikiendi katika ukumbi wa F2 Florida.



# WACHIMBANA MKWARA

Ni wazi hali ya hewa imechafuka baada ya mastaa wawili nchini Marekani, rapa Kanye West na mwanamitindo Khloe Kardashian kuibua timbwili mtandaoni na kuwashangaza watu.

Tukio hilo lilitokea Jumatano ya wiki hii, Khloe ambaye ni mdogo wa Kim Kardashian kuandika maoni yake katika ukurasa wake wa Instagram, akimtuhumu West anatumia vibaya jina la familia yake.

Katika ujumbe huo, Khloe amkabili Kanye West baada ya rapa huyo kuzungumza kuhusu aliyekuwa-familia ya Kardashian kumzuia asimuone binti yake Chicago siku ya kuzaliwa kwake.

Katika maoni yake, Khloé alizungumzia kuhusu siku ya kuzaliwa ya mpwa wake Chicago na sherehe ya kuzaliwa ya pamoja na binamu Stormi Webster mapema mwaka huu, siku ambayo rapa huyo amedai mara kwa mara kwamba Kim Kardashian hakumwalika.

"Ye unajua nakupenda na sitaki kufanya hivi kwenye mitandao ya kijamii, ila wewe ndio umeyaleta hapa, wewe ni baba wa wapwa zangu na ninajaribu kuwa na heshima lakini naomba uachane na Kim na uache kuitumia familia yetu unapotaka kuongea uongo," amesema Khole

Akaongeza kwamba kila mtu amechoka na simulizi ya siku ya kuzaliwa ya binti yake, hivyo Inatosha kwa sababu wote wanajua ukweli.

"Unajua ni wapi watoto wako wako kila wakati na ulitaka siku tofauti za kuzaliwa. Nimeona meseji zako zote na nimethibitisha hilo. Na ulipobadilisha mawazo yako na kutaka kuhudhuria, ulikuja," aliongeza kuandika.

Kama haitoshi, Khloe amesema kama ulivyojieleza Kanye, ndiye anayetunza watoto wake kwa asilimia 80.

"Tafadhali muache yeye na familia yake ili watoto walelewe kwa amani. Ninatoka sehemu ya upendo na nina furaha kuendeleza mazungumzo haya faragha ukipenda " akasisitiza

Hata hivyo, Kanye West hakukaa kimya akajibu kwa ukali akisema tatizo la kuwaona watoto limekuwa sugu na hivyo ndivyo wanavyofanyiwa baba watoto wao weusi.

"Huo ni uongo na mlikataa kunipa anuani ya kwenda kumuona mwanangu ingawa nilifanikiwa," Kanye aliandika.

Aidha akasema, Travis Scott, mpenzi wake na Kylie Jenner, ndiye aliyeshiriki naye eneo la sherehe, yeye ndiye aliweka wazi jambo hilo.



# R Kelly fidia yamsubiri

MWANAMUZIKI mkongwe anayekabiliwa na utitiri wa kesi za udhalilishaji, R. Kelly anaweza kuagizwa kulipa zaidi ya dola za Kimarekani 300,000 kwa mmoja wa waathiriwa kama fidia ya kudhulumiwa kingono.

Fidia hiyo inaweza kutolewa baada ya moja ya kesi yake kurejeshwa kwa Jaji wa Wilaya ya Marekani, Ann Connelly, moja aya adhabu yake ni kulipia gharama ya matibabu ya ugonjwa wa zinaa na tiba ya kisaikolojia kwa mtu huyo.

Mwathiriwa huyo, ambaye bado jina lake halijajulikana, amemshutumu mwimbaji huyo kwa kumpa ugonjwa wa zinaa wakati wa kukutana kwao kimapenzi.

Kelly, alihukumiwa kifungo cha miaka 30 jela mwezi Juni, baada ya kukutwa na hatia kwa makosa mengi ya ulaghai, yanayohusiana na rushwa na kuwalazimisha wasichana kushiriki nao kimapenzi.



## Tekno sigara ina madhara mengi

Mwimbaji, mtunzi na mtayarishaji wa Nigeria Tekno Miles, amefichua kuwa ataanza kuikabili changamoto ya siku 30 ya kuacha kuvuta sigara.

Tekno alifichua haya kupitia akaunti yake ya Instagram ambapo amesema amefanikiwa kukaa siku thelathini za kwanza bila kuvuta sigara.

Ameeleza kwamba, kwa sasa yuko ndani ya siku tatu ya awamu ya pili na ameanza kuzoea hali hiyo.

## Oxlade bora wewe unajua hisani

MTUNZI na mwimbaji wa muziki kutoka Nigeria, Oxlade, amemmwagia sifa Wizkid, huku akimsifu kwa kuimarika kwa kazi yake ya muziki.

Katika video yake akiongea na Capital Xtra, Oxlade amesema kuwa, Wizkid ni moja ya wasanii ambaye amekuwa kama mwalimu wa muziki nchini humo.

Amesema, Wizkid alimpa onyesho lake la kwanza katika ukumbi wa 02 huko London, na mwimbaji huyo alivunja rekodi kwa kujaza watu 21000 katika jiji la Paris nchini Uingereza.





## Teni ulichokifanya Mungu atakulipa

NYOTA wa Afrobeats Teni, amemshangaza mwalimu wake wa shule ya sekondari kwa kumpatia zawadi ya gari jipya.

Teni alimpatia zawadi hiyo mwalimu wake wakati alipomtembelea katika kuadhimisha Siku ya Walimu Duniani.

Mwanamuziki huyo alisoma katika Shule ya Sekondari ya Apata Memorial katika Jimbo la Ondo ambako alipokelewa kwa furaha na wanafunzi na wafanyakazi.

## P Diddy awakera watu weusi

RAPA mkali wa marekani, P Diddy amemtetea msanii mwenzake Kanye West, kuvaa fulana zilizoandikwa White Lives Matter wakati onyesho la wiki ya Mitindo ya Paris.

Katika mahojiano mapya kwenye kipindi cha The Breakfast Club' P Diddy alisema kuwa West mara nyingi kabla ya kufanya huwa anafikiri.

Andiko hilo limeibua majadala mkali katika mitandao ya kijamii kutokana na kutetea maisha ya wazungu jambo ambalo wengi wanaona sawa na ubaguzi.



MAKALA

# Kenya inapogeukia GMO kukabili njaa

- Rais Ruto acheza karata kuwaokoa raia wake



**Na Mwandishi Wetu**

KENYA wiki hii imeidhinisha kilimo na uingizaji wa mazao na vyakula vilivyobadilishwa vinasaba maarufu kama GMO ambavyo nchi nyingi duniani zimepiga marufuku.

Kuondoa marufuku hiyo iliyodumu muongo mmoja, inaweza kusaidia hofu ya watu kukosa chakula kutokana na nchi kukabiliwa na ukame mbaya.

Ukame unaoikumba Kenya inaelezwa ni mbaya zaidi katika miaka 40, na unawaweka hatarini mamilioni ya watu kufa kwa njaa.

Serikali ya Rais William Ruto imegeukia mimea iliyobadilishwa vinasaba kama njia ya kusaidia kuongeza uzalishaji wa mazao.

Inasema nchi inahitaji mbegu zinazostahimili ukame, wadudu na magonjwa.

Miaka kumi iliyopita uzalishaji na uagizaji wa mazao ya GMO ulipigwa marufuku kwa sababu ya wasiwasi juu ya hatari zinazowezekana za kiafya.

Katika jambo la wazi ulikuwa uamuzi huo uliichukiza Marekani, ambayo ni nyumbani kwa wazalishaji wakuu wa mbegu zilizotengenezwa kwa vinasaba.

Mnamo Julai, utawala wa Joe Biden ulitangaza ushirikiano mpya na Kenya ambao ulijumuisha dhamira ya kukuza biashara katika sekta ya kilimo.

Licha ya matarajio ya mavuno mengi, baadhi wanahofia kwamba wakulima wanaweza kutegemea sana sheria zilizowekwa na kampuni za kigeni.

**GMO NI NINI?**

GMO ni kiumbe chochote kilicho hai ambacho vinasaba vyake (DNA) vimebadilishwa kwa kutumia uhandisi jeni. Hii inaweza kuwa mmea, mnyama akiwamo binadamu au bacteria.

Kwa kawaida hufanywa ili kutambulisha sifa inayohitajika katika kiumbe, kama vile matunda makubwa au kustahimili ukame.

Wanadamu kwa kweli wamekuwa wakitumia teknolojia ya chini ya mchakato wa GM kwa maelfu ya miaka kupitia ufugaji. Wakulima wa kale walifanya hivyo kwa kutumia mahindi, na wakabadilisha nafaka ngumu isiyoweza kumeng'enywa kuwa punje za manjano zenye utamu, zinazovutia tunazojua leo.

Uhandisi wa jeni huruhusu kubadilisha moja kwa moja DNA ya viumbe bila kulazimika kupitia mchakato wa kuzaliana kwa vizazi vingi.

Jeni kwa sifa inayohitajika imetengwa kutoka kwa kiumbe tofauti na kuingizwa ndani , ama kwa mikono au kwa kuiunganisha kwa virusi njia isiyo na madhara.

Kuna athari vyakula vya GMO?

Licha ya kile ambacho watu wengi wanaweza kudai, hakuna ushahidi kwamba GMO ni vyakula vibaya kwa kula, kutumia, kugusa, kupaka kwenye ngozi yako au kulisha watoto.

Kwa kifupi, kuna tofauti ndogo kati ya kubadilisha DNA kwa njia ya uzazi wa kuchagua na kuibadilisha kupitia uhandisi wa maumbile, mwili hauwezi kutofautisha kati ya vyakula vya GMO na vilivyo na vinasaba halisi.

Uhandisi wa vyakula unaweza kutumika kuongeza msongamano wa virutubishi katika chakula.

Mfano halisi ni Mradi wa Mchele wa Dhahabu.

Wanasayansi wa chakula walibadilisha mchele wa kawaida kuwa na vitamini A kwa wingi na hii sasa inakuzwa katika maeneo ambayo kuna upungufu wa vitamini A.

Mazao pia yanaweza kubadilishwa ili kutoa mavuno mengi na kukua katika maeneo yenye ukame.

Pamoja na kuwa mzuri kwa biashara kwa ujumla, marekebisho haya yanaweza pia kusaidia kupunguza njaa ulimwenguni.



Baadhi ya mazao ya GMO yanabadilishwa kuwa sugu kwa baadhi ya dawa, ambayo inaweza kuongeza matumizi ya kemikali.

Lakini nyingine zimetengenezwa kutoa sifa zao za kuzuia wadudu, na hivyo kupunguza hitaji la dawa za ziada.

Mbinu zote mbili zinaishia kuua wadudu ambao baadhi yao ni wachavushaji muhimu wa mazao.

Mabishano haya yanaweza kuwa na manufaa ya kimataifa ya mazao ya GMO kwa sasa yanazidi hatari, angalau kulingana na uchanganuzi wa mwaka 2014 uliopitiwa upya katika athari zake iliyochapishwa katika jarida la sayansi PLOS One.

**CHANGAMOTO GANI ZINAZOJITOKEZA?**

Ingawa masuala ya afya yanaweza kuwa yamesisitizwa zaidi na vyombo vya habari, bado kuna sababu nyingi kwa nini GMOs zina utata.

Tatizo moja kubwa ni kwamba zao linaweza kuwa miliki ya kampuni binafsi. Kijadi, wakulima huhifadhi baadhi ya mbegu kutoka kwa zao la sasa ili kupanda kwa ajili ya mavuno ya mwaka ujao.

Lakini kampuni inapomiliki haki za zao la GMO, wanaweza kuwakataza wakulima kufanya hivyo, na kuwalazimisha kununua mbegu mpya kutoka kwa wamiliki kila mwaka. Hata kama mkulima hatapanda mazao ya GMO, wanaweza kuvuna kutoka kwa mashamba ya jirani, na hivyo kufanya iwe muhimu kuwanunulia leseni au kutozwa faini.

Wakosoaji wanasema kuwa inayapa makampuni makubwa udhibiti wa kilimo na uwezo wa kuwanyonya wakulima.

Kuna pia wanasayansi wachache ambao bado wana wasiwasi kuhusu athari za muda mrefu zisizojulikana. Mwanabiolojia wa seli anayepinga ni Dk David Williams ambaye anasema si salama na anadai jeni zilizoingizwa zinaweza kubadilishwa kwa njia kadhaa tofauti ambazo zinaweza kutokea vizazi baadaye.

Akiongea na jarida la Scientific American, anasema kwamba mimea inayoweza kuwa na sumu inaweza kupita katika majaribio katika siku zijazo.

Hata kama wataalamu wengi wanaunga mkono teknolojia ya GM, wakosoaji wengine wanasema kuwa wanasayansi wanaweza kuogopa kutoa changamoto kwa wengi na kuchapisha tafiti zinazopinga kwa sababu watakabiliwa na mashambulizi dhidi ya sifa zao na kupokea ufadhili mdogo kwa utafiti wao.

# Tanzania inapokamilisha ndoto Afrika kuunganishwa reli moja



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akishuka kutoka katika treni ya majaribio wakati akikagua ujenzi wa treni ya mwendo kasi.

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA ni miongoni mwa nchi chache barani Afrika ambayo imeweza kukamilisha ndoto ya kuwa na reli ya kisasa kwa ajili ya kurahisisha usafirishaji watu na bidhaa.

Reli hiyo ya SGR yaani Standard Gauge Railway, yenye upana wa mita 1.435, inaweza kusafirisha uzito mkubwa mizigo na kusafiri kwa mwendo kasi.

Serikali ya Tanzania kupitia shirika la reli Tanzania (TRC) imakaribia kukamilisha ujenzi wa reli kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma, itakapokamilika kutakuwa na mtandao usiopungua kilomita 2,561 ikiunganisha mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma, Katavi na nchi jirani za Rwanda, Burundi na DRC.


Tanzania imefanikiwa kuwa na reli ya kisasa na ya kwanza Afrika mashariki na kati itakayokuwa na uwezo wa kupitisha treni zitakazoendeshwa kwa nishati ya umeme na yenye mwendo kasi usiopungua kilometa 160 kwa saa.

Ndoto kama hiyo imekuwa ikitawala Umoja wa Afrika (AU) na inapanga kujenga mtandao mkubwa wa reli kuunganisha miji mikuu barani humo kufikia 2033.

Lakini mradi huo mkubwa unahitaji ufadhili, jitihada na utashi wa kisiasa.

Treni ya kwanza ya mwendo kasi barani Afrika inayoitwa "Al Boraq" inazunguka katika maeneo ya pwani ya Morocco, ikiwa na kasi ya kilometa 320 kwa saa.

Jina la treni hiyo linatokana na simulizi za kidini na hasa yule farasi aliyekuwa na nguvu isiyo na kifani aliyempanda Mtume Mohammed kutoka Makka hadi Jerusalem.



Treni hiyo inatumia muda wa masaa mawili kati ya Tangier na Casablanca. Ilizunduliwa mwaka 2018 na kutimiza ndoto ya Morocco katika sekta ya usafiri.

Ndoto hiyo imo katika kada ya Umoja wa Mataifa lakini katika uwanja mpana zaidi. Miaka tisa iliyopita umoja huo ulizindua mradi mkubwa unaoitwa "Mtandao wa Reli ya Mwendo Kasi Barani Afrika."

Lengo lilikuwa ni kujenga mtandao mpana wa reli kwa bara zima ifikapo mwaka 2033, kuunganisha miji mikuu muhimu na mikoa.

Lakini kwa zingatio la jitihada hiyo, miunganisho zaidi inaweza kuongezwa itakapofikia 2063.




**SAFARI NDEFU**

Sehemu ya kwanza ya mpango huo inajumuisha maungano ya reli 19 ambayo itachukua urefu wa kilometa 16,970.

Younes Touitha kutoka wakala wa maendeleo wa Umoja wa Afrika-NEPAD, anasema kwamba asilimia 25 ya urefu wa reli katika mpango jumla wa mradi huo unapaswa kutekelezwa katika kipindi cha sasa.

Miunganisho mingine 62 inapaswa kufanyika ifikapo 2063, na hivyo kufikia jumla ya kilomita 74,000.

Umoja wa Afrika uliteua maeneo matatu ya miunganisho kama miradi ya majaribio.

Kutoka bandari ya Tanzania ya Dar es Salaam hadi mji mkuu wa Rwanda Kigali, Kampala nchini Uganda hadi Bujumbura nchini Burundi, na kitovu cha uchumi cha Afrika Kusini Johannesburg hadi Walvis Bay, nchini Namibia, kupitia mji mkuu wa Botswana Gaborone.

Miradi mingine kumi na moja itafanyiwa upembuzi yakinifu haraka iwezekanavyo, kwa mujibu wa mpango kazi wa umoja huo, ambao uliwasilishwa huko Kenya mwanzoni mwa 2022.

Ingawa hadi sasa, mpango huo unasalia kwenye karatasi bila ya kuonekana utekelezaji wake, lakini Tanzania imeanza kwa kasi kwa mafanikio.

Hata hivyo ukweli halisi wa ujenzi wa reli mpya barani Afrika unahitaji kushinda vikwazo vingi.

Toutha anasema vikwazo vingi vinategemea kanda au nchi husika.

Hata hivyo, anaendelea kusema kuwa ifikapo 2030 watakuwa wamefanikiwa asilimia 60 hadi 70 ya malengo, jambo hilo litakuwa jema."

**RELI ZILIZOJENGWA KWA FEDHA ZA CHINA**

Katika sehemu nyingi za Afrika, mitandao ya reli ilianza kujengwa nyakati za ukoloni. Katika nyakati hizo hazikujengwa kwa ajili ya abiria, bali kusafirisha malighafi kama vile mbao au dhahabu hadi bandarini na kuzisafirisha Ulaya.

Wakati huu reli hizo hutumikia kwa malengo mengine, kama kuwezesha biashara na usafirishaji wa abiria kati ya nchi za Kiafrika.

Kwa maoni ya Toutha upatikanaji wa fedha katika kuendeleza miradi hiyo imekuwa changamoto.

Hadi wakati huu, miradi mingi mipya katika eneo la Kusini mwa Jangwa la Sahara imefadhiliwa na China. Mfano mmoja ni ule wa treni mpya ya mwendo kasi inayounganisha bandari kuu ya Kenya ya Mombasa na mji mkuu, Nairobi.

Mikopo ya fedha ya China kwa Afrika inayaweka mataifa ya Afrika katika wakati mgumu. Baadhi ya wataalam wanahofia kwamba kuyalipa madeni hayo kutayaweka mataifa ya Afrika katika hali ngumu kwenye bajeti zake.

**Kwa msaada wa mtandao.**

MAKALA

# LHRC ilivyobaini madudu kampuni binafsi

Na Sabato Kasika

IMEBAINIKA kuna ongezeko la asilimia 84 ya wafanyakazi katika kampuni mbalimbali nchini hawana mikataba ya ajira, huku kundi kubwa wakikabiliwa na ubaguzi na kukosa vitendea kazi vyenye usalama.

Hayo yamebainika katika utafiti uliofanywa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na ripoti yake kuzinduliwa hivi karibuni mkoani Dar es Salaam.

Utafiti huo ulioitwa Haki za Binadamu na Biashara kwa mwaka 2021/2022, umeonyesha kuna mbinu chafu zinazofanywa na baadhi ya waajiri kuwakandamiza wafanyakazi.

Ndani ya ripoti hiyo, imebainika kampuni za watu wenye asili ya Asia zinaongoza kwa vitendo vya ubaguzi kwa asilimia 43.

Hata hivyo, Mkurugenzi Mtendaji wa kituo hicho, Anna Henga anasema kuna uimarikaji kiasi wa uzingatiaji wa sheria na viwango vya kazi kwa baadhi ya maeneo.

Anasema katika baadhi ya kampuni, kumekuwapo na mikataba iliyoandikwa kwa Kiingereza kigumu cha kisheria ambacho wafanyakazi hawakijui na hujikuta wamekwama wanaposaini bila kujua maana yake.

Anaongeza kwamba katika ripoti hiyo imebainika kuna mikataba ya mdomo, na pale mfanyakazi anapotaka kudai haki, hutakiwa kuonyesha mkataba wa maandishi ambao hana na kujikuta akipoteza haki zake.

"Pamoja na hayo, baadhi ya kampuni hasa za ulinzi zinawakata wafanyakazi mshahara, kwa ajili ya sare za kazi, lakini kwenye misingi ya haki za binadamu anayekuajiri ndiye anayetakiwa akupe vifaa vya kazi," anasema Henga

Anaongeza kuwa ndani ya vikwazo hivyo, ripoti hiyo inaonyesha kuwa wafanyakazi wanaopewa mikataba kazini imeongezeka na kufikia asilimia 64.6 ya wafanyakazi walioshiriki utafiti huo walijibu kuwa na mikataba ya ajira.

"Hilo ni ongezeko la asilimia 5.6 ikilinganisha na 2021 ambapo asilimia 35.4 ya waliohojiwa hawakuwa na mikataba ya ajira, hivyo angalau kuna unafuu kidogo katika upande huo," anasema.

Akifafanua zaidi, anasema ripoti hiyo ilibainisha kuwa utoaji wa mikataba ya ajira, asilimia 64.6 ya wafanyakazi (6 kati ya 10) walidai wana mkataba wa ajira, sawa na ongezeko la asilimia 5.6 ikilinganishwa na utafiti wa 2019/2020.

Kwa upande wa likizo, anasema idadi ya wafanyakazi wanaodai kupewa likizo ya mwaka imeongezeka kutoka asilimia 48 hadi kufikia asilimia 51 katika utafiti wa mwaka huu,"anasema.

Wakili Henga anaeleza mkoa ambao una idadi kubwa ya wafanyakazi wenye mikataba ya ajira kuliko mingine ni Kilimanjaro kwa asilimia 90, huku Mkoa wa Mara ukiwa na idadi ndogo ya asilimia 30.

Anataja mikoa mingine ambayo kituo chake kilifanya utafiti kuwa ni Mwanza, Dar es Salaam, Pwani, Arusha, Mtwara, Morogoro, Singida, Mbeya, Geita, Iringa, Tanga, Dodoma na Shinyanga.

Wakili Henga anaongeza kwamba kituo hicho kimetoa mapendekezo mbalimbali kwa serikali ambayo ikiyatumia yanaweza kupunguza matatizo ambayo wafanyakazi wamekuwa wakikumbana nayo.

"Tunapendekeza kulindwa kwa haki za wananchi hasa kwenye mikataba, kusimamia haki ya kuwajibika kwa kampuni zinapotekeleza haki za biashara, mazingira safi ya shughuli, lakini pia kuwe na sheria maalumu ya kubana kampuni kuwajibika kutokana na shughili zinazosababisha wananchi kudhurika," anasisitiza.

Anasema hatua hiyo inaweza kusaidia usimamizi wa haki za binadamu katika mazingira mbalimbali yakiwamo ya sehemu za kazi na pia kuepuka ujanja unaofanywa na baadhi ya kampuni kwenye ajira.

"Kimsingi, mambo tuliyogundua katika utafiti wetu ni mengi, lakini tunatoa mapendekezo hayo kwa serikali na wadau ambayo tunaamini kuwa ndio msingi wa kuwabana wenye kampuni na waajiri, ili waheshimu haki za binadamu kwenye kazi," anaeleza Henga.


Anasema inaumiza kumpa mfanyakazi mkataba kwa mshahara mdogo kwa lengo la kumdhulumu au kuwa na kuandikishiana mkataba kwa lugha ya Kiingereza kigumu ambacho hakijui, ili mwishowe anapoona mambo hayaendi vizuri akihoji anabanwa kwa kutumia mkataba ambao aliingia bila kuuelewa.

Ofisa Programu Mwandamizi Masuala ya Biashara na Haki za Binadamu wa kituo hicho, Joyce Komanya, anasema asilimia ya wanawake waliohojiwa walisema hali ya rushwa ya ngono ni mbaya.

Anasema asilimia 40 ya wanawake walisema hali ni mbaya, huku asilimia nne walisema ipo na waliwahi kushuhudia, huku asilimia zaidi ya 10 wakisema hawajui lolote kuhusu rushwa hiyo.

"Rushwa ya ngono ina athari kimwili, kiakili, kwa mfano mfanyakazi anayekwenda ofisini kila siku na bosi anamfanyia matendo hayo hawezi kufanya kazi vizuri, hivyo hata utendaji kazi unaathirika,"anasema Joyce.

Anataja haki nyingine zinazokiukwa kutokana na rushwa ya ngono, ni mtu amekataa kutembea na bosi wake anafukuzwa kazi au halipwi mshahara ama anapewa nafasi fulani ambayo amesoma na kuna nafasi anatakiwa apate, lakini kwa sababu amekataa kutembea na bosi, hapati.




Viongozi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), wakionyesha ripoti ya kituo hicho ya Haki za Binadamu na Biashara mwaka 2021/ 2022, walipoizindua.




Mkurugenzi Mtendaji wa kituo hicho Anna Henga, akizungumza katika uzinduzi huo. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Sindano zilivyokuwa 'mwiba mchungu', zama zile uhuru bado mbichi

**Na Adam Fungamwango**

ELIMU ni kitu kizuri sana duniani na hata baada ya Uhuru, Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere alisisitiza hilo.

Siyo lazima ukipata elimu basi ikusaidie kupata kazi, la hasha, ila kukusaidia kuelewa na kukabiliana na mazingira na vitu vingine vinavyofanana na hivyo.

Leo hii utaona Watanzania wakihamasishana kwenda kwenye vituo vya afya kutoa na kuchangia damu, wakati miaka ya nyuma walikuwa wanaogopa kuchomwa sindano.

Sindano ilikuwa ni 'mwiba mchungu' si kwa watoto tu wa miaka ya nyuma, bali hata watu wazima. Mtu akiumwa na kutakiwa kwenda hospitali kitu cha kwanza anachofikiria si ugonjwa wake, bali ni kuchomwa sindano.

Ilionekana kama ni adhabu kubwa, au mateso na watoto wengi wakati ule walikuwa wakijiuliza mtu aliyebuni kuchoma wagonjwa sindano alikuwa ni mwenye roho mbaya, na si mtenda haki. Wengi walijiuliza kwani hakukuwa na njia nyingine ya mtu kupona mpaka sindano tu?

Wapo waliokwenda hospitali na kukataa katakata kuchomwa sindano, wakitaka wapewe dawa, lakini kasheshe inakuja pale baadhi wanapoambiwa kuwa ugonjwa wao dawa ni lazima ipite moja kwa moja kwenye mishipa.

Hapo ndipo balaa lilipoanza, si kwa watoto wala wakubwa, wengine walitoroka bila kuchomwa.

Itakumbukwa enzi hizo hata ugonjwa wa TB ilikuwa ni lazima udungwe sindano 60, lakini kwa sasa kuna vidonge.

Watu walikuwa waoga mno kudungwa sindano na hospitali ikaonekana kama ni eneo ambalo hata watoto walikuwa wakiliogopa.

Nakumbuka nilikuwa na mdogo wangu ambaye wakati akiwa mdogo ilifika kipindi akaumwa sana. Alikuwa bado mdogo sana ambaye alikuwa hajui kitu chochote kinachoendelea duniani, lakini kutokana na kupelekwa mara kwa mara hospitalini akawa amepata hisia fulani, kwani mama akifika kwenye geti tu la hospitali anaanza kulia na kutupatupa miguu. Ni kwa sababu anajua muda si mrefu atachomwa sindano. Ni kwamba anapofika getini akaanza kukutana na harufu ya dawa za hospitali ambazo zinampa hisia kuwa muda si mrefu atachomwa sindano, hivyo anaanza kulia.

Ukitaka kujua kuwa hata watu wazima wakati huo walikuwa waoga wa sindano ni kwenye foleni tu. Hospitali za zamani ambazo nyingi ni za serikali, kwenye chumba cha daktari mlango wa kuingilia ulikuwa mwingine na wa kutokea mwingine. Kutokana na hali hiyo mezani mwa mchoma sindano kulikuwa na kengele ambayo ilikuwa inatumika kumwita mgonjwa kuingia ndani.

Mgonjwa anapotoka kwenye mlango mwingine kengele inagongwa, aliyekuwa wa mbele ndiye anaingia. Sasa kasheshe ni kwamba watu walikuwa wanategeana kuingia.

Foleni ya kwenye sindano ndiyo pekee ambayo mtu hadai mahala pake, au kutaka kukaa mbele. Anaweza kufika mbele, anajifanya anakwenda msalani, halafu akirudi anapanga tena foleni nyuma.

Wengi wanasema unapoingia kwenye chumba cha sindano na kukuta nesi anaiandaa kutaka kukuchoma, ndiyo woga unapozidi.

Mmoja wa wauguzi wakati mada hii naiweka kwenye mtandao wa kijamii ili kukusanya maoni ya wadau aliandika jinsi ambavyo mgonjwa anapaswa afanye kabla ya kuchomwa na hata muuguzi anavyotakiwa kumfanyia mgonjwa kabla ya baada ya kumchoma.

"Mgonjwa anatakiwa awekwe sawa kisaikolojia na kulegeza misuli kabla ya kuchomwa sindano.

Kabla ya kumchoma mgonjwa sindano nesi anatakiwa kumtaarifu mgonjwa eneo sindano inapoenda kutua ili asikaze misuli ya sehemu hiyo ili kutosababisha maumivu yasiyo ya lazima.

Sindano inapochomwa inatakiwa kuwa engo ya nyuzi 90 na iingizwe kwa haraka kidogo kiasi cha nusu kichuma cha sindano kuzuia kugusa mfupa, na dawa inaposukumwa inatakiwa iingizwe taratibu mwilini tofauti na jinsi sindano ilivyo ingizwa mwilini ili kupunguza maumivu.

Utoaji wa sindano unatakiwa itolewe mwilini engo ile ile ya nyuzi 90 kama jinsi ilivyoingizwa na baada ya hapo mgonjwa kupewa pole na kupongezwa kwa uvumilivu."

Haya ni maneno ya nesi huyo akielezea jinsi wao wanavyotakiwa kufanya kwa mgonjwa yoyote yule anayeingia kwenye chumba cha sindano mpaka anapotoka.

Sasa tunakwenda kwa wadau wenyewe ambao wametiririka jinsi gani ilivyokuwa ni mtihani mkubwa kuchomwa sindano zamani kwa watoto na hata wakubwa pia, tofauti na sasa.

"Mimi nilikua muoga wa sindano, niliumwa nikapekwa hospitalini na mama. Ile nimeanza kuchomwa imeingia tu hivi nikaona maumivu ni balaa nikafanikiwa kukimbia nje ya chumba huku sindano imening'inia, nesi na mama yangu wakanikimbiza na kunikamata hapo nje ambako kulikuwa na watu wengi waliokuwa kwenye foleni, wakamalizia kunichoma sindano hapo hapo kwenye benchi mbele za watu, nilisikia aibu sana," anasimulia mdau mmoja ambaye alikuwa mtoto wakati huo lakini kwa sasa ni mtu mzima sana. Mwingine naye nguo zilimdondoka

"Kuna siku niliambiwa jiandae na sindano, basi kwa kutetemeka huku nikifungua mkanda, suruali ilianguka hapo hapo chini." Kuna mmoja yeye alisema kuwa alilazwa, lakini aliposikia sindano akatoroka.





"Mimi nilikuwa mgonjwa nikalazwa kwenye hospitali, kosa ambalo daktari alilolifanya ni kuniambia kwamba nitachomwa sindano za makalio saa saba kamili ya usiku. Ilipofika saa sita na nusu nikatoroka."

"Ila mimi pia sindano hapana aisee mara ya mwisho sindano ya kwenye makalio nilichomwa mwaka 1998." Aliandika mama mmoja.

Yupo aliyekumbushia jinsi sindano za masaa nazo zilivyokuwa changamoto kwa sababu unachomwa saa hizi, lakini baada ya masaa sita unarudi tena hospitalini kuchomwa nyingine.

"Mimi nilipokuwa naumwa na kuandikiwa sindano za masaa, nilikuwa nikienda wakinichoma kalio moja, nikija tena baadaye nawaambia hili nilichoma, naomba nibadilishe, chomeni huku, manesi hawakuwa na tabu, wanasikiliza tu mimi nataka nini, wao ili mradi tu watekeleze kazi yao ya kuchoma."

**Tuma meseji 0716 350534**

# Virusi vya Ebola vyabadili umbo

**KAMPALA, Uganda**

WATAFITI wa Uganda wanasema virusi vya Ebola vinavyosambaa nchini humo vimebadilika.

Prof Pontiano Kaleebu wa Taasisi ya Utafiti wa Virusi vya Ebola aina ya Sudan, alisema hata hivyo hakuna ushahidi kwamba inaweza kuambukizwa zaidi ya aina ya awali.

Walichambua sampuli kutoka kwa kisa cha kwanza kinachojulikana kupimwa wakati wa mlipuko wa sasa ambao umeenea hadi wilaya tano za katikati mwa Uganda.

Kufikia jana kulikuwa na visa 44 vimeripotiwa na watu 10 wamekufa kutokana na ugonjwa huo.

Watafiti wanaofuatilia kuenea kwake walisema maumbile ya virusi hivyo yanafanana na yale yaliyosababisha mlipuko mwingine zaidi ya muongo mmoja uliopita katika eneo hilo hilo.

Tafiti zilizofanywa katika nchi jirani ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo zinaonyesha kuwa milipuko ya mara kwa mara inaweza kutokea, lakini si zaidi ya miaka miwili baada ya ile ya kwanza kutangazwa kuwa imeisha.

Kwa hivyo wanasayansi wanaamini kuwa mlipuko huu unaweza kuwa uliletwa kwa wanadamu na mnyama. Sasa wanatafuta mtu wa kwanza kuwa na ugonjwa huo au mawasiliano yao ya moja kwa moja.

Hiyo ingesaidia timu zinazojibu kuelewa vyema jinsi milipuko hiyo ilivyoanza.

**BBC**

**Watafiti wanaofuatilia kuenea kwake walisema maumbile ya virusi hivyo yanafanana na yale yaliyosababisha mlipuko mwingine...**

# Marekani yahofia kuzuka vita ya nyuklia

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani Joe Biden amesema tishio la kiongozi wa Russia, Vladimir Putin la kutumia silaha za nyuklia linatishia kuleta hatari kama ilivyokuwa mgogoro wa kombora la Cuba.

Alisema nchi yake ilikuwa inajaribu kubaini njia ya Putin ya kujiondoa.

Ikulu ya White House ilisema mara kwa mara kwamba haijaona dalili zozote Russia inajiandaa kutumia silaha za nyuklia licha ya kile inachokiita ugomvi wa nyuklia wa Putin.

Hata hivyo, Biden aliweka wazi juzi kuwa alikuwa akimwangalia kwa makini Putin na jinsi anavyoweza kujibu wakati jeshi la Ukraine likipata mafanikio dhidi ya wavamizi wa Russia.

"Kwa mara ya kwanza tangu mgogoro wa kombora la Cuba, tuna tishio la moja kwa moja kwa matumizi ya silaha za nyuklia, ikiwa mambo yataendelea kama yalivyokuwa," Biden aliwaambia wafadhili wa Democratic huko New York.

Pia alisema, nchi yake haijakabiliana na matarajio ya kuangamiza tangu rais Kennedy na mgogoro wa makombora wa Cuba.

Katika mgogoro huo wa Cuba mwaka 1962, Marekani chini ya Rais John Kennedy na Umoja wa Kisovieti chini ya kiongozi wake, Nikita Khrushchev, ilikaribia kutumia silaha za nyuklia kutokana na kuwepo kwa makombora ya Soviet nchini Cuba.

Biden alisema Putin hafanyi mzaha anapozungumzia uwezekano wa matumizi ya silaha za nyuklia za kimbinu au silaha za kibaiolojia au za kemikali, kwa sababu jeshi lake halifanyi kazi vizuri.

"Sidhani kama kuna uwezo wa kutumia kwa urahisi silaha za kinyuklia na sio kuishia na kuangamiza kutumia nyuklia," alisema Biden.

Biden aliongeza kwamba yeye na maofisa wa Marekani wanatafuta njia ya kidiplomasia. Wakati huo huo, Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, akizungumza kwa njia ya video katika kituo cha wataalam cha Australia, alisema NATO lazima ianzishe mashambulizi ya mapema ili kuondoa uwezekano wa Russia kutumia silaha za nyuklia.

Hakufafanua ikiwa alimaanisha mashambulkizi ya nyuklia au anazungumzia matumizi ya silaha za kawaida.

"NATO inapaswa kufanya nini? Zelensky aliuliza, na akajibu mwenyewe. "Ondoa uwezekano wa Russia kutumia silaha za nyuklia."

Alisisitiza kwamba jambo la muhimu anatoa wito kwa jumuiya ya kimataifa, kama ilivyokuwa kabla ya Februari 24, kuzuia mashambulizi ili wajue nini kitatokea kwao ikiwa nyuklia itatumiwa.

Taarifa hiyo ilitolewa ufafanuzi na msemaji wa serikali ya Ukraine Sergei Nikiforov, ambaye alisisitiza kuwa Ukraine haitoi wito wa matumizi ya kuzuia silaha za nyuklia.

"Rais alizungumza kuhusu kipindi hadi Februari 24. Kisha ilikuwa ni lazima kuchukua hatua za kuzuia ili Russia isianzishe vita. Acha nikukumbushe kwamba hatua pekee ambazo zilijadiliwa wakati huo zilikuwa vikwazo vya kuzuia," alisema Nikiforov kupitia ukurasa wa Facebook.

Zana za Russia zasaidia Ukraine

Zana za Russia zinachangia kwa sehemu kubwa katika akiba ya ghala la silaha la Ukraine, imesema taarifa ya kila siku ya ujasusi wa Uingereza.

Ukraine iliteka vifaru vya kijeshi 440 na magari ya kijeshi yapatayo 650 tangu vilipoanza vita vya uvamizi.

Uingereza inakadiria zaidi ya nusu ya vifaru vya Ukraine kwa sasa huenda vikawa ni vile vilivyotekwa.

Ukosefu wa uwezo wa wanajeshi wa Russia wa kuharibu vifaru hivyo kabla ya kurejea kwenye ngome zao unaonyesha mafunzo duni na kiwango cha chini cha nidhamu katika mapigano.

***BBC***



Mwanaume akimfariji mke wake akiwa ameshikilia chupa ya maziwa ya mtoto wao nje ya chumba cha watoto baada ya kuuawa na ofisa wa zamani wa polisi huko Klang mashariki mwa Thailand jana. Jumla ya watoto 38 waliuawa katika tukio hilo. **PICHA: AFP**

# Marekani,Korea Kusini zafanya luteka za majini

**SEOUL, Korea Kusini**

MAREKANI kwa kutumia manowari yake ya kubeba ndege USS Ronald Reagan, na Korea Kusini zimeanza luteka nyingine ya majini.

Luteka hiyo inajiri siku moja baada ya Korea Kaskazini kufyatua makombora zaidi na pia kurusha ndege za kivita, hali inayozidisha mvutano na wapinzani wake.

Wanajeshi wa Marekani wanaotumia manowari ya Reagan walirejea baharini karibu na rasi ya Korea baada ya Korea Kaskazini kufanya majaribio ya kurusha kombora lenye uwezo wa kubeba nyuklia kuelekea Japan.

Korea Kaskazini inatizama luteka za Marekani na Korea Kusini kama mazoezi ya kuivamia.

Hata hivyo taarifa kutoka wakuu wa majeshi wa Marekani na Korea Kusini ilisema lengo la luteka hizo ni kuimarisha uwezo wa washirika hao kijeshi na zitaendelea

***DW***

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Bukoba, Kituo cha Bukoba Mjini Mkoa Kagera**
**Usimamizi wa mirathi Na......55 /2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU LIAQUATALI FAZAL ALMOHAMED WA MIEMBENI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SARAH LYAKAT FAZAL**

Watu wote mnaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 07 Mwezi 11 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia:-** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo tarehe 05 Mwezi 10 Mwaka 2022

................................
**HAKIMU**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**KAGERA LILILOPO BUKOBA**
**RUFAA NA. 60/2021**
**MAGNUS RWELAMILA ..........MUOMBA RUFAA**
**DHIDI YA**
**1. ABDULKHERI AHMADA**
**2. HAMIDA AHMADA...............MJIBU RUFAA**

**KWA:- ABDULKHERI AHMADA NA HAMIDA AHMADA POPOTE MLIPO**

Mnaarifiwa/unaarifiwa kuwa Rufaa Na. 60/2021 yamepangwa kutajwa tarehe 03/11/2022 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza P. J Makwandi saa 2:00 asubuhi.

Hivyo, mnaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Msipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yenu na hukumu kutolewa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa Baraza hili leo tarehe 03/10/2022.

................................
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**BUKOBA**

---

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MWANZA**
**SHAURI LA MAOMBI NAMBA 26 LA 2022**
**DAVID GWABARA MRONDORO..........MDAI**
**DHIDI YA**
**SITA NYIGA..............MDAIWA**

## KUITWA SHAURINI

**KWA: SITA NYIGA**

OMBI LIMEPANGWA KUSIKILIZWA TAREHE 13/10/2022 SAA 04:00 ASUBUHI MBELE YA MH JAJI ITEMBA, KWA HIVYO UNATAKIWA KUSIKILIZA SHAURI LILILOTAJWA HAPO JUU LILILOFUNGULIWA NA MDAI DHIDI YAKO.

KAA- UKIJUA KUSHINDWA KUFIKA SHAURI LITASIKILIZA OMBI HILO NA KUTOA UAMUZI BILA WEWE KUWEPO.

**IMETOLEWA NAMI KWA AMRI NA CHAPA YA MAHAKAMA LEO TAREHE 28/09/2022**

NAIBU MSAJILI
MWANZA.

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) MBINGA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 95/2022**
**FULKO C. KAPINGA..................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**MATHIAS NCHIMBI..................MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**MDAWIA: MATHIAS NCHIMBI – POPOTE ULIPO.**

BW. FULKO C. KAPINGA amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo (Boma). Shauri husika limepangwa kusikilizwa tarehe............ Hivyo basi unatakiwa kuleta utetezi wako ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya tangazo hili kutolewa. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika masijala ya wazi Bazara la Ardhi na Nyumba (W) Mbinga. Endapo hutatekeleza haya shauri litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa.

**AMRI** hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 25 Mwezi wa 10 mwaka 2022.

................................
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) MBINGA

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JUMANNE RAMADHANI MTENDA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 396 DNH- MITSUBISHI FUSO.** Chassis namba **FK628K540188.** Engine namba **6D17920043.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **MKB//RB/TR/135/2022.**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KONGWA DISTRICT AT KONGWA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 13 OF 2022**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE MUSSA MARCO MASHENENE**
**DECEASED OF KONGWA DODOMA**
**AND**
**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**MATHIAS KANYATTA GAMBISHI...............PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES G.N NO.369 OF 1963)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made the above named petitioner. Objections to the grant should be field on or before the 10 day of **OCTOBER 2022.**

The will of the said deceased is deposited and open for inspection at the Court Date 26 day of **SEPTEMBER 2022.**

................................
**District Resident Magistrate**

---

**FORM 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 877 OF 2022**
**In the matter of the Estate of the late**
**ELINAMI MONYO SIFUEL**
**And**
**In the matter of Application for letters of Administration by**
**JANEDINAH EDWARD KIWIA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above –named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate( or letters of administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 21 day of November 2022

**Dated at DAR ES SALAAM this 29 day of September 2022.**

................................
Registrar/Senior Resident Magistrate

---


*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HADITHI

MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani. Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni huyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo alisimama na msimamo wake ule ule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa. Matokeo ya haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.

# KAMA IPO, IPO TU-26

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Nilichotaka hapa ni mambo mengi tu. Kwanza sapraizi, halafu nijue kama kweli mtu huyu ananipenda kwa dhati, achilia mbali tulivyokuwa tukiishi kule, lakini je yuko tayari kuolewa nami? Nikawachukua hawa wafanyakazi wangu, Billy na Daudi, nilianza kuja nao hadi barabarani pale nikawapa ramani yote, halafu nikawaachia kazi. Walirudi na kuniambia barua imekubaliwa. Nilishtuka kidogo, lakini wakaniambia habari ya Siwatu kuwa ameshakataa waanaume wengi sana, lakini ameikubali hii kwa sababu amekaa sana na amepatwa na matatizo ya kubakwa, na ameshachoka kukaa kwenye kijiji, hivyo ameamua kuondoka, na kukubali kuolewa. Hiyo ilimpa nguvu kuwa kumbe alikuwa ananisubiri, ila amechoka baada ya kutokea matatizo. baadaye mimi mwenyewe nikaja sasa hapa kama Bakari. Nikamtamkia kuwa nataka kumuoa, wakati najua kuwa barua imekuja na ni yangu. Ilikuchanganya sana bibie, niliona hali uliyokuwa nayo, mpaka ukaniambia tutoroke. Hapo nikajua kabisa kuwa unanipenda, na uko tayari kuachana na barua ya mtu ambaye humfahamu. Kwa hili nasema ni kweli nimepata mke wa kweli. Kingine ambacho kabla sijamaliza sikutaka kukisahau ni kwamba nimewasiliana na polisi wa kituo cha Chalinze waje kufanya uchunguzi wa kubakwa kwako. Niliposikia tu hili jambo nilipokuja hapa, niliwasiliana nao, na wiki hii yote walikuwa kwenye uchunguzi, muda si mrefu wataniambia wamefikia wapi. Sasa nathibitisha rasmi kuwa ile barua mliyopokea ilikuwa yangu, na mimi ndiye mchumba pekee wa Siwatu, nataka uwe mke wangu sasa, mama na dada zangu wanakusubiri Dar. Nataka kukufanya uwe malkia."

Kila mtu alionekana kutokwa na jasho. Ilikuwa ni kama hadithi fulani ya kufikirika, lakini ukweli ndio ulibaki kuwa huo.

Sam, kijana wa kitajiri ndiye Bakari. Bakari huyo ndiye yule aliyetupwa porini kijijini na kuokolewa na Siwatu. Siwatu huyo ni yule msichana yatima aliyemsaidia mtu asiyemjua na kutengwa na kijiji. Kumbe aliyemsaidia si Bakari ambaye wao walimfahamu kijiji ni kuwa ni kijana hohe hahe aliyetoka kusikojulikana. Ni kijana aliyerithi mali ya marehemu baba yake na akatekwa kwa kutupwa kwa husuda za wafanyabiashara wenzake.




**"Sawa, lakini hapa kijijini uliporejea na fahamu tunakuuliza jina ulisema unaitwa nani? Siwatu akauliza.**

Siwatu alimuacha Sam na kumfuata kaka yako, Dibwela ambaye naye alisimama, akamkumbatia. Siwatu akaanza kulia kwa nguvu.

"Usilie Siwatu, hatimaye mizimu ya baba na mama yako imekuona."

"Siamini mimi kaka, nimedhalilika kwenye kijiji hiki, nimefanyiwa kila aina ya vitimbwi. Nilikuwa naomba Mungu kila siku, leo amejibu kilio changu." Aliongea Siwatu kwa hisia kali na ilionekana akili yake sasa ilianza kuamini kile kinachoendelea.

"Dada siku zote kama ipo ipo tu. Mungu akisema ndiyo binadamu si dawa, wanachofanya ni kuchelewesha tu."

Siwatu akiwa kama aliyechanganyikiwa kwa furaha, alimuacha tena kaka yake na kumfuata Sam.

"Bakari, hivi kwa nini siku zote uliamua kunificha? Kwa nini usiniambie? Mimi naishi kwa mashaka, kumbe wewe mwenzangu unajua kila kitu. Tumeishi hapa miezi mitatu watu wanatunyanyasa mpaka wanakataa kutuuzia chakula kumbe wewe ni mtoto wa kitajiri na sivyo walivyokuwa wakikuchukulia."

"Mpenzi, ulikuwa ni mpango mkakati niliouweka mwenyewe. Ulikuwa ni kama mtihani kwangu na kwako. Mimi nilitaka niishi kama mwanakijiji ili nijue aina ya maisha ambayo watu wengine wanaishi. Na kweli nimepita kwenye tanuri la moto. Leo hii nataka kukuoa, najua naoa mwanamke wa aina gani. Kama umeweza kuniokoa kwenye kifo kufa porini, umenilinda na mashambulizi ya wanakijiji ambao walikuwa wanataka niondoke kabla sijapona. Ukakubali kuondolewa ule upendeleo uliokuwa unaupata kama msichana yatima kijijini na kukuona ni kituko, lakini hukujali. Hukujali dharau, kejeli, vitisho, ukaendelea kuwa na mimi mpaka mimi mwenyewe niliposema sasa naondoka, ni kitu gani sasa kitatutenganisha? Kwa sasa utakwenda kuishi maisha mengine kabisa. Maisha ya mjini, ya kisasa ambayo yatakutoa kuwa msichana yatima na kuwa kama malkia."

"Nakuahidi nitakuwa malkia wako mwema na mtiifu. Kama tulivyoishi na wewe hapa miezi mitatu mwanzo na wiki hizi mbili tulizoishi na wewe ulivyorudi tena ndiyo hivyo tutakwenda kuishi. Uwe mfalme wangu mwema."

Ni kipindi ambacho Dibwela, Billy na Daudi waliamua kutoka nje na kuwaacha wapenzi hao walikuwa kwenye kilele cha furaha.

Dibwela alikwenda hadi kwa Mwenyekiti wa Kijiji na kuhadithia maajabu yaliyotokea. Kumbe yule Bakari waliokuwa hawamtaki aishi pale kijijini ndiye huyo huyo aliyeleta barua ya kumchumbia Siwatu.

Na kumbe hakuwa mtu wa kawaida tu kama walivyofikiri bali ni kijana wa kitajiri aliyetupwa porini na wafanyabiashara wenzake kabla Siwatu hajamuokoa. Kumbe alimuokoa mtu muhimu ambaye leo amelipa fadhila kwa kuamua kumuoa.

"Ila kuna kitu unaniudhi."

"Nini tena mpenzi Bakari?"

"Si hivyo kuniita Bakari?" Alipomaliza kusema hivyo wote walijikuta wakiangua vicheko.

"Mimi jina langu kamili ni Sam."

"Sawa, lakini hapa kijijini uliporejea na fahamu tunakuuliza jina ulisema unaitwa nani? Siwatu akauliza.

"Kwa hiyo Bakari ndiyo jina la kijiji?"

"Ndiyo mimi nimelizoea hilo, yaani leo tu ndiyo nimelijua hilo la Sam, sasa ngoja kwanza tukiondoka hapa kwenda Dar es Salaam ndiyo nitaacha kukwita Bakari kwa sababu lilikuwa la hapa." Yalikuwa ni mazungumzo ya mzaha baina ya wachumba hao wawili.

"Kesho ndiyo tunaondoka Dar, sasa huko ndiyo utaanza kunita Sam?

"Hapana."

"Kumbe utaniita nani?"

"Mume wangu." Akajibu Siwatu na wote wakakauka kwa vicheko, wakiwa kwenye kilele cha furaha.

**MWISHO**

# KIPANGA YAOTA KUCHEZA MAKUNDI MICHUANO CAF

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Kipanga FC imesema wachezaji wake wana hamasa kubwa kuhakikisha wanautumia vyema uwanja wa nyumbani katika mchezo wa kimataifa wa mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika utakaochezwa leo dhidi ya Club Africaine kutoka Tunisia kwenye Uwanja wa Amaan.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Kipanga, Khamis Hassan, alisema kuelekea mchezo huo tayari wamekamilisha maandalizi muhimu na wanachosubiri ni kuona wanapambana ili kupata matokeo mazuri.

Hassan alisema hata kama timu itacheza vizuri lakini ikikosekana shauku na hamasa itapunguza ladha ya kupata ushindi.

Kocha huyo alisema walitumia kipindi cha mapumziko mafupi ya Ligi Kuu Zanzibar ili kujiandaa vyema na kuhakikisha wanatimiza malengo yao ya kutinga hatua ya makundi ya mashindano hayo.

"Tumejipanga kufanya vizuri ikiwamo kuvuka salama hatua hii na kufikia makundi, najua utakuwa mchezo mgumu, sisi tunahitaji kutamba kwenye uwanja wa nyumbani na wenzetu wanahitaji kutumia vyema uwanja wa ugenini," alisema Hassan.

Naye Kocha Mkuu wa Club Africaine, Bentrand Manchand, alisema anahitaji kushinda mchezo huu wa ugenini kwa sababu ni mchezo muhimu zaidi katika hatua hii waliyopo.

Manchand alisema katika mpira chochote kinawezekana kutokea ama iwe ugenini au nyumbani, hivyo kwake atahakikisha wachezaji wanajituma na kuhakikisha wanapata ushindi katika mechi hii ya kwanza.

"Najua mchezo utakuwa mgumu kwa sababu wapinzani wetu wanahitaji kupata matokeo mazuri wakiwa nyumbani kwao lakini na sisi tunahitaji kupata matokeo ugenini," alisema kocha huyo.

Aliongeza wakipata ushindi katika mechi ya leo itawasaidia kuelekea mchezo wa marudiano ambao utakuwa ni wa kumalizia kazi waliyoianza Zanzibar.

"Tunahitaji kuanza vizuri mashindano haya, lengo letu ni kusaka ushindi bila kujali tunacheza ugenini, katika mpira wa kisasa ushindi unapatikana kokote, tumekuja kutafuta matokeo mazuri," aliongeza kocha huyo.

Kipanga ambayo inamilikiwa na Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), ilifanikiwa kusonga mbele kucheza hatua ya kwanza ya mashindano hayo kwa mara ya kwanza baada ya kuwaondoa Al Hilal Wau kutoka Sudani Kusini.

Maafande hao ndio wawakilishi pekee wa Zanzibar waliobakia kwenye mashindano ya kimataifa baada ya KMKM kuondolewa katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.



Kiungo wa Winners Academy, Talkh Ngwata (kulia), akiwania mpira dhidi ya mchezaji mwenzake wa timu ya kituo hicho, Richard Sheba katika mazoezi ya kujiimarisha yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Oysterbay jijini, Dar es Salaam jana. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# KMKM yabanwa, Chipukizi safi

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAKATI mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Zanzibar, KMKM wamelazimishwa sare ya bao 1-1 na Jamhuri ya Pemba, Chipukizi imepata ushindi wake wa kwanza wakiwa ugenini katika ligi hiyo inayoendelea visiwani hapa.

Chipukizi ilifanikiwa kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Maafande wa JKU katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mau ze Dong, mfungaji pekee akiwa ni Faki Mwalimu.

Kocha Mkuu wa Chipukizi, Ali Bakari 'Mngazija' alisema bado jitihada za wachezaji zinahitajika ili kufikia malengo ya kushinda michezo yote ya ugenini watakayocheza Unguja.

Mngazija alisema Ligi Kuu Zanzibar sasa ina ushindani mkubwa kwa sababu kila timu inahitaji kufanya vizuri hasa ikicheza kwenye uwanja wa nyumbani lakini pia hata wakiwa ugenini ili kujiweka kwenye nafasi nzuri katika msimamo wa ligi hiyo. Aliongeza baadhi ya timu zimeshaanza kujiweka kwenye mbio za ubingwa hivyo wao pia wanahitaji kufika katika nafasi hiyo na kujilinda na kushuka daraja kwa kufanya vizuri katika mzunguko huo wa kwanza.

"Tumepata ushindi wa kwanza tukiwa ugenini, ushindi huu utaufanya mchezo wetu ujao kuwa mgumu sana kwa sababu wapinzani wetu watajiandaa kuzibakisha pointi, ndio maana nimewasisitiza wachezaji wangu waongeze juhudi na jitihada katika michezo hii ya ugenini,"alisema Mngazija.

Polisi Zanzibar walipata kichapo cha mabao 3- 0 kutoka kwa Mafunzo katika mchezo mwingine wa ligi hiyo uliochezwa kwenye Uwanja wa Amaan juzi jioni.

## Kanu abadilishiwa majukumu Singida

**Na Shufaa Lyimo**

BODI ya Wakurugenzi wa Singida Big Stars imemteua aliyekuwa Mkurugenzi Idara ya Masoko wa klabu hiyo, Muhibu Kanu kuwa Kocha Mkuu wa timu ya vijana wa umri chini ya miaka 20 (U-20), imeelezwa.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Singida Big Stars, Hussein Masanza, alisema nafasi iliyokuwa ya Kanu sasa itakuwa chini ya Tabitha Kidawawa.

"Lengo la kufanya mabadiliko haya kwenye safu yetu ya uongozi tunataka kuongeza nguvu kwenye Idara ya Masoko pamoja na kuwa na kikosi bora cha vijana," alisema Masanza.

Akizungumza uteuzi huo, Tabitha alisema anaushukuru uongozi wa klabu hiyo kwa kumwanini kupata nafasi hiyo na anaahidi atasaidia kutafuta wadhamini mbalimbali wa ndani na nje ya nchi ili kuitafutia fursa zaidi timu yao.

"Nimejipanga kutafuta wadhamini kutoka sehemu mbalimbali, iwe nje au ndani ya Tanzania ili klabu yetu izidi kukua," alisema kiongozi huyo.

## Kagera Sugar SC, Polisi majaribuni

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Kagera Sugar itamkosa nyota wake, Kassim Seka katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Polisi Tanzania itakayochezwa leo baada ya kuumia mguu akiwa mazoezini juzi.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Francis Baraza, alisema mchezaji huyo jana alishindwa kufanya mazoezi ya pamoja na wenzake kutokana na maumivu aliyokuwa nayo.

"Kesho (leo) nitamkosa mchezaji wangu huyo mmoja kutokana na kuumia mguu, hawezi kucheza mpaka atakapokaa sawa," alisema Baraza.

Kocha huyo alisema pia wachezaji wengine wanaendelea vizuri kuelekea mchezo huo ambao unatarajiwa kuwa na ushindani.

"Ninashukuru kuona kila mchezaji ana morali ya kufanya vyema katika mchezo huo ingawa hatujafanya vizuri katika michezo iliyopita, maandalizi mengine yanaendelea vizuri na tumeyafanyia kazi makosa ambayo tuliyabaini kwenye michezo iliyopita," Baraza alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### HAALAND MSHAHARA JUU

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Norway, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 22, anapokea mshahara wa pauni 865,000 kwa wiki katika klabu ya Manchester City. ***(Mail)***

### GUARDIOLA AFUNGUKA

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amekanusha uvumi kwamba Erling Haaland ana kipengele cha kuondoka na kuruhusiwa kujiunga na Real Madrid. ***(Mirror)***

### RONALDO ANUKIA GALATASARAY

KLABU ya Galatasaray inataka kumsajili mshambuliaji wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37 wakati wa dirisha la Januari. ***(Fotomac)***

### KANTE MAMBO MAGUMU

KIUNGO wa kati wa Ufaransa, N'Golo Kante mwenye umri wa miaka 31, anaamini Chelsea hawataki kumwongezea mkataba, huku mkataba wake wa sasa ukikamilika msimu ujao wa joto. ***(Footmercato)***

### ARSENAL YAMTAKA TAREMI

ARSENAL inavutiwa na mshambuliaji wa Porto, raia wa Iran mwenye umri wa miaka 30, Mehdi Taremi. ***(A Bola, via TEAMtalk)***

### SILVA ATAJWA MADRID

REAL Madrid wanamfuatilia beki wa Benfica, Mreno Antonio Silva mwenye umri wa miaka 18. ***(Calciomercato)***

### CALHANOGLU, INTER KITAELEWEKA

KLABU ya Inter Milan ina matumaini kupata mustakabali wa muda mrefu wa Hakan Calhanoglu mwenye umri wa miaka 28. ***(TEAMtalk)***

### BOURNEMOUTH SOKONI

BILIONEA wa Marekani, Bill Foley ambaye anamiliki kampuni ya NHL ya Vegas Golden Knights, ana makubaliano ya mdomo ya kuinunua Bournemouth ya Uingereza. ***(Athletic)***

### BAYERN ILIMTAKA RONALDO

OFISA Mtendaji Mkuu wa Bayern Munich, Oliver Kahn, amesema miamba hao wa Bundesliga walifikiria kumnunua mshambuliaji wa Manchester United, Cristiano Ronaldo katika majira ya joto ***(Bild, via Mail)***

### LOPETEGUI, WOLVES KUTETA

KLABU ya Wolves inatarajia kufanya mazungumzo na Julen Lopetegui wikendi hii, baada ya kutimuliwa kama kocha mkuu wa Sevilla. ***(Sky Sports)***

### BELLINGHAM APELEKWA UNITED

MCHEZAJI wa zamani wa Manchester United, Rio Ferdinand ameitaka klabu yake hiyo kumsajili kiungo wa kati wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19, ambaye pia analengwa na Real Madrid na Liverpool. ***(Mirror)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI: KOMBE LA DUNIA QATAR NI MWISHO WANGU

Mshambuliaji huyo asema angependa kulibeba kombe hilo lakini amekiri...

**PARIS, Ufaransa**

LIONEL Messi amethibitisha michuano ya Kombe la Dunia ya mwaka huu itakayofanyika nchini Qatar itakuwa ya mwisho kwake kucheza.

Sasa akiwa na umri wa miaka 35, Messi bado hajafanikiwa kutwaa taji la Kombe la Dunia, alishindwa katika fainali dhidi ya Ujerumani mwaka 2014 na kuondolewa katika hatua ya robo fainali mwaka 2006 na 2010.

Nafasi pekee ya Messi kulibeba kombe hilo ni mwaka huu nchini Qatar na amethibitisha kuwa michuano hiyo ni ya mwisho kwake.

"Ndio, hakika ndio," alijibu wakati alipoulizwa na Star+ kama Kombe la Dunia la Qatar litakuwa la mwisho kwake kucheza.

"Ninahesabu siku hadi Kombe la Dunia. Ukweli ni kwamba, kuna wasiwasi kidogo, ukisema: 'Vyema, tuko hapa, nini kitatokea? Ni yangu ya mwisho, itakuwaje?'. Kwa upande mmoja, siwezi kungoja ifike lakini pia ninatamani sana iende vizuri."

Argentina ni miongoni mwa timu zinazopigiwa upatu kabla ya michuano hiyo, lakini Messi amesisitiza haoni hivyo.

"Tuko katika wakati mzuri sana, na kundi lenye nguvu sana, lakini lolote linaweza kutokea kwenye Kombe la Dunia," alieleza.

"Mechi zote ni ngumu, hilo ndilo linalofanya Kombe la Dunia kuwa la kipekee sana kwa sababu wanaopewa nafasi kubwa si mara zote wanashinda au hata kufanya vizuri unavyotarajia.

"Sijui kama sisi tuna nafasi hiyo, lakini Argentina yenyewe daima ni mgombea wa historia. Sisi sio wenye nafasi kubwa, nadhani kuna timu nyingine ambazo ziko juu yetu."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,037,3

MECHI KALI
BORUSSIA DORTMUND
VERSUS
BAYERN MUNCHEN
1 | 4.25
X | 4.45
2 | 1.61

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa · vodacom m-pesa · airtel money · ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KIWANGO ARSENAL CHAMKERA ARTETA

**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta anahisi timu yake "ilikosa udhibiti" licha ya kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Bodo/Glimt na kupaa kileleni mwa Kundi A katika Ligi ya Europa.

Eddie Nketiah na Rob Holding walifunga kipindi cha kwanza kabla ya Fabio Vieira kufunga goli la tatu dakika ya mwisho kwa washikabunduki hao.

Washikabunduki hao sasa wanaongoza kwa pointi mbili dhidi ya na PSV walio nafasi ya pili katika kundi hilo, huku pia wakiongoza kwenye msimamo wa Ligi Kuu England baada ya kuanza vyema kwa kushinda michezo tisa kati ya 10 ya kwanza katika michuano yote kwa mara ya tatu pekee katika historia ya klabu hiyo.

Lakini Arteta alikuwa na hisia tofauti juu ya uchezaji wa timu yake dhidi ya Bodo, akiiambia BT Sport: "Nimefurahia sana ushindi, pointi sita na mabao safi, lakini tulikosa uhusiano kati ya wachezaji, tulikosa udhibiti kwenye mchezo wote.

"Kulikuwa na mabadiliko nane na wachezaji wengi ambao hawajacheza dakika nyingi. Katika tatu ya mwisho tulionekana hatari sana, mabao tuliyofunga yalikuwa mabao mazuri."

Kipindi cha pili walianza vyema na Arteta alifanya mabadiliko kadhaa, akiwaingiza Bukayo Saka na Gabriel Jesus akatoa pasi nzuri kwa Vieira.



# Rashford: United haikuwa bora

**MANCHESTER, England**

MARCUS Rashford amesema "nilipenda Manchester United ingecheza vizuri zaidi" licha ya kutoka nyuma na kupata ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Omonia Nicosia kwenye Ligi ya Europa, Alhamisi.

United walikwenda mapumziko wakiwa nyuma ya bao moja baada ya Karim Ansarifard kuifungia timu yake, lakini Erik ten Hag akimwanzisha Rashford aliyebadilisha mchezo huku akifunga mabao mawili na kutoa asisti kwa Anthony Martial na kuwafanya Mashetani Wekundu hao kuwa mbele kwa 3-1.



Licha ya kufungwa tena na kufanya matokeo kuwa 3-2, United walifanikiwa kupata ushindi wao wa sita katika mechi saba zilizopita za Ligi ya Europa wakiwa ugenini na kuwaacha kwenye nafasi ya pili katika Kundi E, pointi tatu nyuma ya vinara, Real Sociedad.

Rashford anahisi timu yake haikucheza vyema katika uwezo wao kamili dhidi ya Omonia, akiiambia BT Sport: "Ndio, ni kazi iliyofanywa, lakini tungependa kucheza vizuri zaidi.

"Siwezi kusema tulikuwa vibaya sana, nadhani ni makosa na makosa yanatokea kwenye soka, hivyo tunataka kusonga mbele. Makosa machache tunayoweza kufanya, ndivyo bora zaidi.

361,877/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 08/10/22 | 17:00 | Millwall vs Middlesbrough | 2.63 | 3.13 | 2.73 |
| 02. 08/10/22 | 17:00 | Swansea vs Sunderland | 2.33 | 3.28 | 3.03 |
| 03. 08/10/22 | 17:00 | Wigan vs Cardiff | 2.35 | 3.18 | 3.08 |
| 04. 08/10/22 | 17:00 | Birmingham vs Bristol City | 2.59 | 3.24 | 2.69 |
| 05. 08/10/22 | 19:30 | Brighton vs Tottenham | 2.90 | 3.35 | 2.37 |
| 06. 08/10/22 | 19:30 | Sevilla FC vs Athletic Bilbao | 2.69 | 3.19 | 2.64 |
| 07. 08/10/22 | 22:30 | Pacos Ferreira vs Vitoria Guimaraes | 3.00 | 3.10 | 2.48 |
| 08. 09/10/22 | 14:00 | Huddersfield vs Hull City | 2.36 | 3.33 | 2.93 |
| 09. 09/10/22 | 15:00 | Valladolid vs Betis | 3.03 | 3.33 | 2.30 |
| 10. 09/10/22 | 16:00 | Salernitana vs Verona | 2.53 | 3.37 | 2.68 |
| 11. 09/10/22 | 16:00 | Udinese vs Atalanta | 2.63 | 3.37 | 2.58 |
| 12. 09/10/22 | 16:00 | Angers vs Strasbourg | 2.44 | 3.33 | 2.78 |
| 13. 09/10/22 | 17:15 | Cadiz CF vs Espanyol | 2.88 | 3.18 | 2.48 |
| 14. 09/10/22 | 18:30 | Arsenal vs Liverpool | 2.64 | 3.45 | 2.53 |
| 15. 09/10/22 | 18:30 | Hertha BSC vs SC Freiburg | 3.02 | 3.41 | 2.25 |
| 16. 09/10/22 | 19:30 | Real Sociedad vs Villarreal | 2.53 | 3.23 | 2.78 |
| 17. 09/10/22 | 20:30 | Stuttgart vs Union Berlin | 2.61 | 3.15 | 2.71 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 08/10/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 11:45 | 2775 | Sydney FC vs Melbourne Victory | 2.54 | 3.48 | 2.54 |
| 13:00 | 2368 | Spartaks Jurmala vs FC Riga | 17.47 | 7.18 | 1.11 |
| 14:00 | 2358 | Slutsk vs BATE Borisov | 4.07 | 3.78 | 1.70 |
| 14:00 | 3000 | Fakel vs Zenit St Petersburg | 9.15 | 5.57 | 1.26 |
| 14:00 | 4954 | Nkwazi vs Zanaco | 2.67 | 2.58 | 2.96 |
| 14:00 | 5856 | Sonderjyske vs Hobro | 1.42 | 4.37 | 6.02 |
| 14:30 | 3012 | St Johnstone vs Celtic | 11.92 | 6.56 | 1.19 |
| 15:00 | 3296 | Almeria vs Rayo Vallecano | 2.95 | 3.15 | 2.42 |
| 15:30 | 2324 | Tripoli SC vs AL Ahed | 5.07 | 3.66 | 1.59 |
| 16:00 | 1888 | Mladost Lucani vs FK Napredak | 2.41 | 3.21 | 2.67 |
| 16:00 | 2069 | Torpedo Zhodino vs Gomel | 1.96 | 3.30 | 3.49 |
| 16:00 | 2267 | Sabayil vs FK Sumgayit | 2.62 | 3.11 | 2.52 |
| 16:00 | 2431 | FK Zlatibor vs FK Loznica | 2.17 | 2.92 | 3.36 |
| 16:00 | 3843 | FK Jedinstvo UB vs Metalac | 3.15 | 3.05 | 2.36 |
| 16:00 | 4213 | Power Dynamos vs Kansanshi Dynamos | 2.03 | 2.90 | 4.30 |
| 16:00 | 4433 | Sassuolo vs Inter | 4.15 | 4.05 | 1.69 |
| 16:00 | 4751 | Mbeya City vs Ihefu FC | 2.12 | 2.95 | 3.85 |
| 16:00 | 4929 | Prison Leopards vs Chambishi FC | 2.05 | 2.95 | 4.20 |
| 16:15 | 5533 | Al Wasl Dubai vs Al Dhafra | 1.46 | 4.47 | 5.25 |
| 16:30 | 1843 | Augsburg vs VfL Wolfsburg | 2.83 | 3.28 | 2.37 |
| 16:30 | 2611 | Bayer Leverkusen vs Schalke 04 | 1.43 | 4.75 | 5.94 |
| 16:30 | 3226 | TS Galaxy FC vs Moroka Swallows FC | 2.24 | 2.72 | 3.76 |
| 16:30 | 3308 | VfL Bochum vs Eintracht Frankfurt | 3.71 | 3.71 | 1.85 |
| 16:30 | 3566 | Mainz vs RB Leipzig | 2.93 | 3.37 | 2.26 |
| 16:30 | 5106 | CSKA Moscow vs Dinamo Moscow | 1.66 | 3.97 | 4.46 |
| 17:00 | 1177 | Livingston vs Ross County | 1.94 | 3.33 | 3.87 |
| 17:00 | 1435 | Newcastle vs Brentford | 1.76 | 3.77 | 4.07 |
| 17:00 | 1622 | Antalyaspor vs Konyaspor | 2.40 | 3.20 | 2.90 |
| 17:00 | 1834 | Bournemouth vs Leicester | 3.27 | 3.47 | 2.06 |
| 17:00 | 2175 | Chelsea vs Wolverhampton | 1.36 | 4.66 | 7.73 |
| 17:00 | 2684 | Manchester City vs Southampton | 1.13 | 7.76 | 15.19 |
| 17:00 | 5239 | Hradec Kralove vs Teplice | 1.79 | 3.60 | 4.46 |
| 17:00 | 5509 | Ballymena Utd vs Portadown FC | 1.51 | 4.08 | 5.24 |
| 17:00 | 5691 | Rangers vs St Mirren | 1.21 | 5.97 | 11.94 |
| 17:15 | 2400 | Atletico Madrid vs Girona | 1.47 | 4.20 | 6.60 |
| 17:30 | 2271 | Santa Clara vs Sporting Lisbon | 5.56 | 4.07 | 1.54 |
| 17:30 | 3817 | FC Volendam vs Ajax | 11.85 | 7.70 | 1.16 |
| 18:00 | 1231 | SCR Altach vs RB Salzburg | 7.97 | 5.45 | 1.26 |
| 18:00 | 1624 | Marseille vs AC Ajaccio | 1.33 | 4.78 | 8.57 |
| 18:00 | 2528 | LASK Linz vs TSV Hartberg | 1.31 | 5.03 | 7.36 |
| 19:00 | 1291 | Sochi vs Lokomotiv Moscow | 1.72 | 3.97 | 4.07 |
| 19:00 | 5713 | AC Milan vs Juventus | 2.05 | 3.27 | 3.47 |
| 19:30 | 3256 | Borussia Dortmund vs Bayern Munchen | 4.25 | 4.45 | 1.61 |
| 19:30 | 3483 | Sevilla FC vs Athletic Bilbao | 2.94 | 3.24 | 2.37 |
| 19:30 | 5403 | Brighton vs Tottenham | 2.67 | 3.36 | 2.45 |
| 21:00 | 3996 | Orlando Pirates vs Richards Bay FC | 1.76 | 3.32 | 4.77 |
| 21:30 | 2499 | BSC Young Boys vs St. Gallen | 1.63 | 4.29 | 4.39 |
| 21:45 | 1247 | Bologna vs Sampdoria | 2.02 | 3.43 | 3.43 |
| 22:00 | 1185 | Reims vs Paris St Germain | 7.69 | 5.31 | 1.32 |
| 22:00 | 4117 | Getafe vs Real Madrid | 6.39 | 4.39 | 1.46 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# TZ PRISONS, SINGIDA BIG STARS MARUFUKU KUSAJILI

**Adam Fungamwango na Hadija Mngwai**

KAMATI ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), imezifungia kusajili klabu za Singida Big Stars na Prisons baada ya kubainika kuingia mikataba na wachezaji ambao bado walikuwa mali katika timu nyingine.

Taarifa iliyotolewa jana na Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Clifford Ndimbo, ilisema timu hizo zilisajili makipa kutoka klabu nyingine za Ligi Kuu Tanzania Bara ambao hawakuwa huru na walitakiwa kuvunja kwanza mikataba ya awali.

Ndimbo katika taarifa yale alisema Prisons imekumbana na kifungo hicho baada ya kumsajili golikipa, Mussa Mbise kutoka Coastal Union wakati ikifahamu bado alikuwa na mkataba na klabu yake hiyo ya jijini Tanga.

Alisema Singida Big Stars yenyewe imekutana na adhabu hiyo baada ya kumsajili kipa, Metacha Mnata huku akiwa bado ana mkataba hai na Maafande wa Polisi Tanzania.

"Kamati imesema imefanya uamuzi huo kwa kuzingatia Kanuni ya 47 (21) ya Ligi Kuu na adhabu hiyo ni kwa dirisha moja la usajili," alisema Ndimbo.

Aliongeza kutokana na adhabu hiyo, Singida Big Stars na Prisons hazitasajili mchezaji yoyote kwenye dirisha dogo la usajili linalotarajiwa kufunguliwa ifikapo Desemba, mwaka huu.

Alisema kamati hiyo imezikumbusha klabu zote nchini usajili wachezaji unatakiwa kufanyika kwa kuzingatia kanuni na timu itakayokiuka itachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizowekwa.

Wachezaji hao wote walisajiliwa mwanzoni mwa msimu huu na wamekuwa wakionekana wakizichezea timu zao mpya.




Mshindi wa Multibet, Ezra Paul kutoka Tabata, Dar es Salaam akishikilia mfano wa hundi ya Sh. milioni 31.1 kama zawadi yake baada ya kubashiri kwa usahihi mechi za Multibet kutoka SportPesa. Ukibashiri Multibet inakupa nafasi ya kujishindia bonasi hadi asilimia 750 ya fedha yako. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Simba yakamilisha ramani ya ushindi

INATOKA UK. 32

hayo.

"Utayari wa vijana uko juu sana, tunaenda kuwaheshimu wapinzani wetu, mipango yote ya kucheza ugenini inaanzia mazoezini, tumewafatilia wapinzani wetu na tayari tumejua ubora na madhaifu yao," Mgunda alisema.

Simba inatarajia kuondoka leo kwa ndege maalum ya kukodi na itarejea nchini baada ya kumaliza mechi hiyo tayari kuendelea na michezo yake ya Ligi Kuu Bara kabla ya kurudiana na Premeiro

## Iwe jua, iwe mvua

INATOKA UK. 32

ikicheza tofauti na mechi walizocheza awali kwa sababu watafanya mabadiliko makubwa na huku kocha wao, Florent Ibenge, akiwa na faida ya kuwahi kuwafundisha baadhi ya wachezaji wake.

"Muda mwingi umepita tangu alipowahi kuwafundisha Fiston Mayele, Shaban Djuma, Yannick Bangala, wamekuwa wana mabadiliko makubwa ya viwango tofauti na awali," alisema Nabi. Pia, ameitaka safu yake ya ulinzi kuhakikisha inakuwa makini kwa kuwaonyesha baadhi ya video za Al Hilal wanavyojua kutumia vizuri mipira ya kona na faulo.

Naye kiungo wa Yanga, Gael Bigirimana, alisema wamejiandaa vizuri na muhimu kwao ni kushinda mechi ya nyumbani kwa ajili ya kupata urahisi katika mchezo wa marudiano.

"Kwa uzoefu wangu mashabiki ni sehemu ya hamasa na ni mchezaji wa 12, wajitokeze kwa wingi ili kuwaongezea wachezaji nguvu ya kupambana kwa ajili ya kupata matokeo mazuri," Bigirimana alisema.


Fiston Mayele pia amewataka mashabiki wa Yanga wasibakie nyumbani na badala yake wafike uwanjani kwa wingi kuwapa nguvu ya kutimiza malengo ya kuondoka na ushindi.

**Michezo**

Jumamosi Oktoba 8, 2022

**Nipashe**

UKURASA 29



**Messi: Kombe la Dunia Qatar ni mwisho wangu**

# Iwe jua, iwe mvua Al - Hilal hawatoki

## ●●●Yanga yadhamiria kumaliza kazi hapa nyumbani ili kujiweka katika...

**Na Saada Akida**

HATIMAYE ile siku iliyokuwa inasubiriwa na mashabiki wa soka nchini imefika kwa Yanga kuwakaribisha Al Hilal kutoka Sudan katika mechi ya kwanza ya hatua ya kwanza ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Yanga imefika hatua hiyo baada ya kuwaondoa FC Zalan ya Sudan Kusini katika mechi ya hatua ya awali kwa ushindi wa jumla wa mabao 9-0.

Akizungumza jijini jana, Kocha Mkuu wa Yanga ambaye ni raia wa Tunisia, Nesreddine Nabi, alisema amekiandaa vyema kikosi chake na sasa kipo tayari kwa ajili ya mchezo huo.

Nabi, alisema Al Hilal ni timu nzuri na yenye uzoefu mkubwa katika mashindano ya kimataifa na wamekuwa na rekodi nzuri kwenye michuano hiyo inayofanyika kila mwaka.

Alisema timu hiyo ambayo aliwahi kufundisha imezidi kuimarika kila mwaka na imekuwa ikifika katika hatua nzuri za michuano hiyo ingawa anafahamu wao pia wanaihofia Yanga.

"Kitendo cha kwenda DRC (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo), kucheza mechi ya kirafiki ni moja ya kujiweka sawa. Nimeongea na wachezaji na kuwahimiza wawe makini, wasibweteke kwa kuona wapinzani wetu wamepoteza mechi ya kirafiki, tumejiandaa vizuri ili kufikia malengo yetu ya kuvuka katika hatua hii," alisema Nabi.

Aliongeza, amewataka nyota wake kuongeza utulivu wanapokaribia lango la wapinzani na kutumia vizuri nafasi ambazo watazitengeneza.

"Wachezaji wapo tayari kupambana katika mchezo wa kesho (leo), wanatakiwa wajiamini na wanafahamu mechi hii haitakuwa rahisi, tunatakiwa kupambana kupata matokeo mazuri kwa sababu mechi haitaishia hapa, baada ya kwa Mkapa itaenda kuchezwa tena Khartoum," alisema Nabi.

Mtunisia huyo alisema katika siku mbili hizi hali ya wachezaji iko vizuri na wako tayari kwa ajili ya kujitoa katika mchezo huo kwa lengo la kupata ushindi wa nyumbani na kujiweka katika nafasi nzuri kuelekea mchezo wa marudiano.

"Tunaenda kukutana na timu iliyofanya usajili mkubwa kwa kutumia Dola za Marekani milioni tano, na kuajiri kocha mwenye uzoefu mkubwa, wachezaji wangu wanalifahamu hili na wamejiandaa kwa ajili ya kupata matokeo bora kwenye mchezo wetu wa kesho (leo).

Kuhusu kikosi cha kesho (leo), sitaweka wazi kwa sababu ya kuogopa kujiua, hii mechi Al Hilal imejiandaa vizuri kwa sababu walitufatilia na hata sisi pia tumewafuatilia baada ya kuwatuma watu kwenda DRC katika michezo yao ya kurafiki," alisema kocha huyo.

Aliongeza, anatambua Al Hilal inawaogopa kwa sababu waligoma kuonyesha mubashara mechi yao ya mwisho dhidi ya St. George ya Ethiopia katika michuano hiyo ili Yanga isipate nafasi ya kuwaangalia, lakini mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara walifanikiwa kuichambua kutokana na kutuma watu Sudan kuwaangalia.

Alisema pia, anatarajia kuiona Al Hilal

INAENDELEA UK. 31



Kiungo wa Yanga, Feisal Salum 'Fei Toto' (kulia), akifanyiwa mazoezi na kocha wa viungo wa timu hiyo kuelekea mechi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Hilal kutoka Sudan itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

## Simba yakamilisha ramani ya ushindi

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI Simba ikitarajiwa kuondoka leo kuelekea Luanda, Angola kwa ajili ya mechi ya mkondo wa kwanza ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya wenyeji Primeiro de Agosto, Kaimu Kocha Mkuu wa timu hiyo, Juma Mgunda amesema atatumia akili zaidi ili kuondoka na ushindi.

Waangola hao wanatarajia kuikaribisha Simba kesho kwenye Uwanja wa 11 de Novembro, kuanzia saa 12:00 jioni kwa saa za Tanzania.

Mgunda alisema pamoja na wapinzani wao kuonekana ni wazuri mno wanapocheza nyumbani, lakini kwake amejiandaa kuwadhibiti kikamilifu na hawana hofu yoyote.

Kocha huyo alisema wamewafuatilia wapinzani wao katika mechi zake mbalimbali na kubaini wana timu nzuri ambayo haistahili kubezwa na hasa wanapocheza kwenye ardhji yao.

"Tumewafuatilia baadhi ya mechi zao, tumejua nguvu yao iko wapi na udhaifu wao upo wapi, kilichobaki kilikuwa ni kuandaa mpango mkakati wa kuyatumia mapungufu yao na kuwadhibiti kwenye maeneo ambayo wao ni hatari, kwa jinsi nilivyowaona ni wakorofi sana wanapokuwa kwao, ni watata sana, lakini yote tumeyaangalia na tumeyadhibiti kwa sababu wachezaji wa timu yangu wanaonekana wanaitaka sana hii mechi," alisema Mgunda.

Aliongeza kuelekea mechi hiyo ameshirikiana na wachezaji wazoefu na michuano hiyo ya kimataifa kuwajenga wenzao wapya na wenye umri mdogo kujiandaa kisaikolojia kuipambania klabu hiyo.

"Vijana wapo vizuri na hawa wachezaji wakongwe na wenye wazoefu nimewaona wanajaribu kuwatia moyo wachezaji vijana ambao hawana uzoefu wa michuano hii, kifupi ni kwamba wanaitaka mechi. Nimekaa na wachezaji nikawaambia uzuri wa kocha yoyote unaonyeshwa na wachezaji, hivyo wajiandae kuonyesha ubora wao kwa sababu mimi hapa unaponiona ni mshindani, napenda kushindana ili nipate kitu kizuri na mafanikio, na wao pia wajiandae kutimiza malengo yao kwa klabu na nchi kwa ujumla," alisema Mgunda.

Alisema katika kikao chake na wachezaji waliwaambia kuwa malengo ya klabu ni kufika nusu fainali, hivyo wakiungana kwa pamoja, viongozi, wachezaji na benchi la ufundi na kufanya kazi kwa kujituma wanaweza kufikia malengo

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >